## BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Arobaini na Tatu – Tarehe 13 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za *Consolidated Holding Corporation* kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2006 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Consolidated Holding Corporation for the year ended 31st December, 2006).*

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The Annual Report of the Tanzania Revenue Authority for the year ended 30th June, 2006).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi kwa Mwaka 2005/2006 *(The Annual Report and Accounts of the National Board of Accountants and Auditors for the year 2005/2006).*

Taarifa ya Mwaka ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa Mwaka 2005/2006 *(The Annual Report of the Institute of Finance Management for the year 2005/2006).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 395

**Uhitaji wa Barabara Kata ya Kahe**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Kata ya Kahe wanalima mazao kama mpunga, mahindi, maharage kwa wingi lakini hakuna barabara nzuri kwa ajili ya usafirishaji wa mazao hayo kwenda sokoni:-

(a) Je, Serikali itajenga lini barabara katika kijiji cha Mawalla-Oria-Mwangaria-Soko mpaka Whona na kuunganisha na barabara kuu ya Moshi-Dar es Salaam?

(b) Je, Serikali italijenga daraja la Soko mwaka huu ambalo wananchi wamekuwa wakilihitaji kwa miaka mingi sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Benti Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara inayopita katika kijiji cha Mawalla-Oria-Mwangaria-Soko mpaka Whona na kuunganisha na barabara kuu ya Moshi-Dar es Salaam ni sehemu ya barabara ya Kahe-Kyomu yenye urefu wa kilomita 11 na daraja la Soko lililoko kwenye barabara hiyo ambalo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia vipo katika Kata ya Kahe Jimboni Vunjo. Hii ni mojawapo ya barabara zinazounganisha barabara za Wilaya *(Feeder Roads)* ambayo haijawahi kutengenezwa kitaalamu *(Non Engineered Road),* lakini ni muhimu sana kwa wananchi wa Kata hiyo na maeneo mengine ambamo wana mashamba katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Mawalla-Oria-Mwangaria hadi njia panda ya Moshi-Dar es Salaam inahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa, yaani *(Rehabilitation)* kutokana na uharibifu uliopo na hasa baada ya mvua za mwezi Novemba, 2006 hadi Januari 2007. Gharama za ukarabati wa barabara inakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi 128,345,000/=. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kupitia Mfuko wa Matengenezo ya Barabara *(Road Fund)* inatarajia kuingiza barabara hii katika mpango wake wa mwaka 2008/2009, ili ianze kutengenezwa kwa awamu mpaka hapo itakapokamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, daraja la Soko ni moja ya kiungo muhimu sana katika barabara niliyoitaja. Gharama ya ujenzi wa daraja hili inakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi 40,000,000/= mpaka kukamilika. Hata hivyo, baada ya Bajeti ya matengenezo ya barabara kuongezeka, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi inatarajia kuliingiza daraja hili katika mpango wake wa matengenezo ya barabara kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Kata ya Kahe kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya, kwa kujitolea kuifanyia barabara hiyo matengenezo madogo madogo ili iweze kupitika.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Kimaro kwa juhudi zake za kuwahamasisha wananchi bila kujali itikadi za kisiasa. Namwomba pia kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi azidi kuwahamasisha wananchi wake waendelee kujitolea zaidi na kuifanyia matengenezo madogo madogo barabara hiyo mpaka hapo tutakapoitengeneza na pia kutumia barabara ya *TPC-Chekereni* na Chekereni-Kahe zilizo katika maeneo haya na ambazo zinafanyiwa matengenezo, wakati tukisubiri matengenezo ya barabara na daraja hilo.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kata ya Kahe ni moja ya Kata ambazo zinazalisha mpunga kwa wingi. Kuna mashamba kwenye kijiji cha Mawalla makubwa na yana uzalishaji nzuri sana wa mpunga. Barabara hiyo ambayo ninaizungumzia ya kutoka Mawalla-Oria-Soko mpaka kuunganisha barabara kuu ya Moshi-Dar es Salaam ni barabara muhimu kwa ajili ya kusafirisha haya mazao siyo kwa wananchi wa Kahe tu hata kwa Tanzania nzima.

Sasa swali la kwanza, je Serikali haioni umuhimu wa kuipa kipaumbele barabara hiyo kwa sababu hailishi tu wananchi wa Kahe bali pia na Watanzania wote kwa ujumla?

Swali la pili, katika utekelezaji wa miradi ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na barabara. Watendaji wa Halmashauri ndiyo wanaotangaza tenda, Watendaji hao hao ndiyo wanaofanya *valuation,* Watendaji hao hao ndiyo wanao-*award tender,* Watendaji hao hao ndiyo wanaosimamia na kulipa bila kuwahusisha Madiwani ambao miradi hiyo ndiyo iko kwenye Kata zao. Je, Serikali haioni huo mpango siyo mpango endelevu ambao unawafanya Madiwani, ambao miradi inafanyika kwenye Kata zao wasiweze kusimamia kikamilifu. Swali, Serikali itarekebisha lini mpango huo ili kuwapa meno Madiwani wasimamie miradi ndani ya Kata zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli sehemu za Mawalla wanazalisha sana mpunga na nikubaliane naye kwamba kweli barabara hii ni muhimu na kweli inaunganisha Moshi hadi Dar es Salaam kwa manufaa ya Tanzania nzima na siyo kwa manufaa ya Moshi peke yake. Ndiyo maana Serikali ina mpango kabambe wa kuitengeneza barabara hii katika Bajeti yake ya mwaka 2008/2009. Kwa mwaka huu Serikali imetenga fedha kidogo tu shilingi milioni 14.2 ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. Naomba tu nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa fedha hizo kidogo ambazo zimetengwa na kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Kahe na wanavyokuwa na moyo wa kujitolea naomba waendelee kutumia hizo hela chache na wenyewe kujitolea ili barabara hii iweze kupitika kwa mwaka nzima.

Kuhusu suala la watendaji. Ni kweli Sheria mpaka sasa hivi watendaji hao hao ndiyo wanaotangaza tenda, ndiyo wanaofanya *evaluation* na ndiyo wanao-*award tender* za Halmashauri. Madiwani wako pale kwa ajili ya kuhoji. Sheria hiyo mpaka sasa hivi haijarekebishwa. Madiwani wanashirikishwa pale katika vikao vya fedha na mipango pale wanaweza wakahoji tenda yoyote na katika Baraza la Madiwani wanaweza wakahoji

suala lolote ambalo wanaona linaenda kinyume na Sheria. Mpaka sasa hivi Madiwani wanashirikishwa kwa njia moja au nyingine katika tenda zote za Halmashauri, wao ndiyo wasimamizi wa miradi katika Kata zao. Kwa sasa Sheria hii bado haijarekebishwa na kwa kweli hakuna umuhimu wa kuirekebisha sasa hivi kwa sababu Madiwani wanashirikishwa kikamilifu kupitia kwa Mwenyekiti wao wa Halmashauri au Meya wa Halmashauri.

Na. 396

**Kero inayosababishwa na mgambo wa Jiji**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam na Mwanza kumekuwepo na watu wanaojulikana kama mgambo wa jiji ambao wamekuwa kero kwa wananchi kwani wanazichukua bidhaa zao, kuzipora au kuzigawana na wakati mwingine husomba magari kwa kisingizio kwamba yameegeshwa kimakosa na kutoza wahusika shilingi 80,000/= kwa jiji la Dar es Salaam na kwa kuwa zoezi hilo limependwa sana kwa sababu wanapewa asilimia fulani kutokana na kukamata magari hayo, hivyo hulifanya zoezi hilo kwa kutotumia sheria na busara hasa nyakati za sikukuu za kidini:-

(a) Je, watu hao wanafanya hivyo kwa mamlaka na sheria gani ya nchi?

(b) Je, ni magari mangapi yaliyokamatwa katika Jiji la Dar es Salaam na Mwanza kwa kosa la kuegesha vibaya (kwa takwimu) kati ya tarehe 1/4/2007 na 7/4/2007 kabla ya sikukuu ya Pasaka?

(c) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wanaodhulumiwa mali/biashara na wale wanaotozwa faini na wanamgambo wa jiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa Mijini hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 6 ya mwaka 1999 na Sheria Na. 13 ya mwaka 2006.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 62 cha Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) kikisomwa pamoja na Jedwali katika Sheria hiyo, Halmashauri za Miji zina jukumu la kudhibiti na kuratibu matumizi ya barabara na mitaa ndani ya eneo lake la Utawala.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mamlaka hiyo, Halmashauri za Miji zina wajibu wa kuhakikisha kuwa mtumiaji mmoja mmoja wa Barabara au Mtaa haleti bughudha au kero kwa watumiaji wengine wa barabara hiyo.

Hivyo basi, kwa kuzingatia wajibu huo wa Kisheria na kwa kuwa tatizo la kuegesha magari katika sehemu zisizoruhusiwa ni kero kwa watumiaji wa barabara hasa watembea kwa miguu, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (na siyo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam) iliamua kutekeleza Sheria Ndogo Ndogo ya Maegesho kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 60 la mwaka 1988, Kifungu cha 10 (2) kwa kuyakamata magari yote yanayoegeshwa katika sehemu zisizoruhusiwa.

Kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza, wanatekeleza Sheria Ndogo ya Jiji (Ada ya Maegesho) ambayo ilipitishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 448 la tarehe 29/9/2002. Zoezi la kuvuta magari yanayoegeshwa kwenye sehemu zisizoruhusiwa hufanywa na Mawakala ambao waliingia Mkataba na Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaokamatwa kwa makosa ya kuegesha vibaya na magari yao kuvutwa na Wakala wa Halmashauri, mwenye gari hupaswa kulipa shilingi 30,000/= (kama gharama ya uvutaji) na shilingi 10,000/= kwa gharama ya kutunza gari *(Impound Charges)* kwa siku kwa Jiji la Mwanza.

Kwa Manispaa ya Ilala Wakala anaingia Mkataba na Halmashauri kwa malipo ya shilingi 25,000/= kwa kila gari linalovutwa ambapo Halmashauri hupata shilingi 60,000/= na hivyo kufanya jumla ya malipo kuwa shilingi 85,000/= kwa kila gari linalovutwa. Askari wanaosimamia zoezi hili ni waajiriwa wa Halmashauri pamoja na vibarua ambao malipo yao ni shilingi 3,000/= kwa siku.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza jumla ya magari tisa (9) yalikamatwa kwa makosa mbalimbali yakiwemo kuegesha vibaya, kuegesha maeneo yasiyoruhusiwa pia kwa kukwepa ushuru wa maegesho. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kupelekwa Mahakamani na kupigwa faini kati ya shilingi 20,000/= hadi shilingi 50,000/= kwa gari moja. Jumla ya shilingi 250,000/= zilipatikana. Kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, kati ya tarehe 1-7/4/2007 jumla ya magari 53 yalikamatwa na kuliingizia Halmashauri ya Ilala jumla ya shilingi 3,475,000/= kama ifuatavyo:- Tarehe 2/4/2007 yalikamatwa magari 12, tarehe 3/4/2007 yalikamatwa magari 14, tarehe 4/4/2007 yalikamatwa magari 14 na tarehe 5/4/2007 yalikamatwa magari 13. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 6/4/2007 ilikuwa siku ya Ijumaa Kuu na tarehe 7/4/2007 ilikuwa siku ya Jumamosi. Zoezi hilo halifanyiki siku za sikukuu na siku za mwisho wa wiki, hivyo hakuna takwimu zinazoonyeshwa kukamatwa kwa magari.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kunyang'anywa au kuporwa mali zao, hali wakiwa wanafanya kazi hizo katika maeneo yaliyotengwa, hali hiyo haipo. Halmashauri inachofanya ni kwamba wafanya biashara wanaokiuka Sheria ndio wanaokamatwa na

kupelekwa Mahakamani na uamuzi wa adhabu hutolewa na Mahakama na sio wanamgambo wa Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wananchi kutoa taarifa kwa Mamlaka zinazohusika endapo kuna mgambo wa Halmashauri watagundulika kufanya kazi yao kinyume na Sheria. Aidha, natoa wito kwa wananchi kuheshimu Sheria za nchi kwa kufanya biashara zao na kuegesha magari yao katika sehemu zilizoruhusiwa tu.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa miji na majiji mengi na manispaa gharama za barabarani *traffic signs* pamoja zile zinazoonyesha mitaa zinakuwa hazionekani kwa mfano unaweza kukuta jina la mtaa lina kibao kina futi moja na nusu badala ya mita moja ambao dreva wa gari anaweza kuona kwa urahisi na kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunafanya madereva wageni wa miji hiyo kutojua alama na sehemu za maegezo pamoja na *traffic lights*. Je, Serikali iko tayari kuziagiza mamlaka hizo za majiji, na miji na manispaa kuweka alama za barabarani na mitaa ili zionekane ili dreva mgeni aweze kuona kwa urahisi kama wanavyofanya *TANROADS?*

Swali la pili, kwa kuwa kuna malalamiko mengi sana katika Jiji la Mwanza na Dar es Salaam kwamba wamachinga wakati wa zoezi la kusafisha majiji hayo wameporwa mali zao na watu wengine. Je, Serikali iko tayari kufungua Ofisi za kusikiliza malalamiko hayo na madai kuanzia Jumatatu ijayo ili watu walionyang'anywa mali zao waweze kurudishiwa mara moja kwa Mwanza na Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli kuna sehemu za miji yetu au majiji yetu kuna *traffic signs* ambazo hazionekani. Zoezi hili kwa Dar es Salaam sasa hivi limefanyiwa kazi na kama kwa watu mnaoishi Dar es Salaam au mnaokwenda Dar es Salaam mmeona Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeanza kuweka *traffic signs* katika sehemu zote na mitaa yote. Naona kwa upande wa Mwanza nao wataendelea na zoezi hili na miji mingine kadhalika, kwa sababu hizo *traffic signs* zisipoonekana ina maana kwamba ajali nyingine zitakuwa zinatokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Wamachinga kuwa mali zao huwa zinaporwa na hao wanaokamata. Kwa mujibu wa Sheria mali yoyote ya Wamachinga ikikamatwa inapelekwa Mahakamani. Ikipelekwa Mahakamani kule ndiko kunakotolewa uamuzi kwamba alipe faini kiasi gani. Kama ameshindwa kulipa faini ile mali yake Mahakama inaamua kwamba iuzwe. Kwa hiyo, sehemu ambayo inaenda kinyume na hayo imevunja sheria ndiyo maana kwenye swali la msingi nimesema kwamba tunawaomba wafanya biashara wakiwemo Wamachinga wafuate sheria na taratibu za nchi pamoja na wananchi au hao wanamgambo pia wafuate sheria na taratibu za nchi. Ni kinyume cha sheria kuchukua mali ya Mmachinga halafu kugawana au kuipeleka sehemu isikojulikana. Kwa

upande wa Dar es Salaam Mahakama ya Jiji inashughulikia masuala hayo kila siku mali zinapokamatwa na kwa jiji la Mwanza Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mkoa inalishughulikia suala hilo. Lakini kwa Dar es Salaam kuna *specific* Mahakama ya Jiji la Dar es Salaama ambayo inashughulikia malalamiko na matatizo ya Wamachinga na wafanya biashara wadogo wadogo.

Na. 397

**Watalaam wa Mipango Vijijini**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka mingi ya Maendeleo ya nchi yetu, Serikali imekuwa ikijitahidi kila mara kutafuta njia nyingi za kuwaletea wananchi Maendeleo lakini mafanikio yake yamekuwa si makubwa kuliko ilivyotarajiwa:-

(a) Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha mafunzo ya wataalam wa mipango vijijini na kuagiza kila wilaya isomeshe wataalam hao?

(b) Je, Sera ya idadi ya watu inaelewekaje vipi na wananchi na uhusiano kati ya uchumi na ongezeko kubwa la watu na uchumi mdogo unaoongezeka kidogo kidogo?

(c) Je, kuna mashindano gani kati ya utendaji kazi wa Wilaya kwa Wilaya ili wanaofanya kazi nzuri ya kiutawala/kiuchumi wazawadiwe na wale wengine waadhibiwe?

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Kayombo hujajibu, Mheshimiwa Naibu Waziri. Napenda tutambue kurejea kwako. Pengine *Presiding Officers* wengine walikwishakukaribisha. Lakini kwa kuwa mimi ni mara ya kwanza baada ya siku kadhaa, napenda kusema tumefurahi sana umerudi salama baada matibabu. Ahsante sana. Baada ya hapo sasa majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, kwa kweli nawajibika kukushukuru sana kwa kutambua kurejea kwangu na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Spika ambaye alikwishafanya hivyo tarehe 9 siku ya Alhamisi.

Lakini pia nichukue muda huu pia kuwashukuru Madaktari wa Hospitali Kuu ya Dodoma kwa juhudi walizofanya na Madaktari wa Muhimbili ambao walifanya kazi kubwa sana. Naomba Mungu awabariki waendelee kufanya hivyo kwa wananchi wote. Lakini pia namshukuru Mungu ambaye ndiye alikuwa Daktari Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali na Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatoa umuhimu mkubwa wa kuimarisha mafunzo ya wataalam wa mipango vijijini na wilayani, na ndiyo maana Serikali ina chuo chake maalum kinachoendesha mafunzo yanayolenga kuimarisha na kuboresha ujuzi, ufahamu na umahiri, kwa maafisa watendaji katika ngazi ya vijiji, kata, wilaya, mikoa na taifa. Mafunzo haya huendeshwa na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kilichopo Dodoma katika ngazi zifuatazo:-

Ngazi ya Cheti katika Mipango ya Maendeleo Vijijini – Mafunzo haya ni ya mwaka mmoja na nusu na yanalenga maafisa watendaji wa vijiji, mitaa, vitongoji na (Sheria kule Tanzania Zanzibar).

Ngazi ya Stashahada ya juu katika Mipango ya Maendeleo – Mafunzo haya ni ya miaka miwili na yanawalenga maafisa watendaji wa kata na tarafa.

Ngazi ya Shahada ya kwanza – Mafunzo haya ya miaka mitatu, yanalenga maafisa watendaji wa wilaya, mikoa na taifa kwa maana ya (Wizara).

Ngazi ya Stashahada ya Uzamili – Mafunzo haya ya mwaka mmoja yanawalenga maafisa waratibu, wasimamizi na viongozi wa Maendeleo kwa jumla.

Aidha, Serikali kupitia programu za maboresho ya Serikali za Mitaa na ile ya Utumishi, imeelekeza kuajiri na kuimarisha sekta ya rasilimali watu kupitia mafunzo ya mara kwa mara na ya muda mrefu pamoja na vitendea kazi katika kila Halmashauri ya Wilaya ili kuwa na watendai wenye ujuzi, maarifa na sifa zinazotakiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi walio wengi hawakufahamu vyema Sera ya Taifa ya idadi ya watu ya mwaka 1992. Aidha, Sera iliyoboreshwa, yaani Sera ya Taifa ya idadi ya watu ya mwaka 2006 imewekewa mikakati maalum ili iweze kufahamika na kutekelezwa kikamilifu.

Mkakati wa kutekeleza Sera hiyo umekamilika ambapo umezingatia maeneo yaliyopewa kipaumbele na Sera ikiwa ni pamoja na ujumuishaji wa vipengele vya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo, ajira, matatizo ya makundi maalum, jinsia, afya ya uzazi, UKIMWI, mazingira, kilimo, chakula na lishe, kuondoa umaskini, elimu, takwimu na mawasiliano.

Ili kuhakikisha sera hii inafahamika kikamilifu Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji imeandaa mikakati mbalimbali ya kuwaelimisha Wabunge, Viongozi na watendaji wakuu wa Serikali, Maofisa wa Mipango na Uchumi katika mikoa na wilaya, wananchi na wadau wengine kwa masuala ya idadi ya watu na maendeleo ili kuhakikisha kuwa mipango ya maendeleo na bajeti katika maeneo yao yanazingatia vipaumbele vya sera hii.

Jitihada zitafanyika zaidi ili kutangaza zaidi sera hii kupitia mikutano mbalimbali ya kitaifa na vyombo vya habari.

Aidha, sera, mkakati na tafsiri ya sera katika lugha nyepesi *(Popular Language)* zitasambazwa na mafunzo maalum kutolewa kwa watendaji wa ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna mahusiano ya karibu kati ya ukuaji wa uchumi na ongezeko kubwa la watu ambapo kunaweza kukaathiri kwa kiasi fulani ukuaji wa pato la Taifa na hasa wastani wa pato halisi la mtu mmoja mmoja *(income per capita).*

Hivyo ni muhimu kuweka mikakati maalum ili kuhakikisha kuwa ongezeko la idadi ya watu linaendana na ukuaji wa uchumi. Hivi sasa ongezeko la idadi ya watu nchini ni asilimia 2.9 ambapo kiwango cha pato la Taifa *(GDP)* ni asilimia 6.2. Aidha, wastani wa pato l a Taifa kwa kila mtu *(per capita GDP)* bado ni chini ambapo ni shilingi 400,000/= (US $ 319) kwa mwaka.

Kwa kuwa vipaumbele vilivyopo katika Sera ya idadi ya watu vinajumuisha ushirikishaji wa sekta na asasi mbalimbali, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji itahakikisha inaratibu na kuhusisha sera, mikakati na programu za sekta zingine ili kufikia Maendeleo endelevu.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa hakuna sera ya kuzishindanisha Wilaya mbalimbali kiutendaji.

Hata hivyo, Serikali imekuwa ikihimiza utendaji mahiri kwa kila Halmashauri ya Wilaya ambapo zile zinazopata hati safi za matumizi bora ya fedha za Serikali zimeendelea kupatiwa fedha za ruzuku ya Maendeleo, ambapo zile zinazopata hati chafu yaani matumizi mabaya ya fedha za Serikali zimekuwa zikinyimwa fedha za ruzuku ya Maendeleo.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na mimi nimefurahi ya kwamba amerudi salama. Nina imani kabisa tutaendelea kushirikiana naye.

Swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa takwimu zinatuambia ya kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa asilimia 2.9 wakati uchumi kama taarifa niliyokuwa nayo imeongezeka kwa asilimia 6.2.

Je, Mheshimiwa Waziri haoni ya kwamba katika msingi huo tulionao nchi yetu itaendelea kuwa ni maskini kwa kipindi kirefu ana mipango gani ya kuhakikisha ya kwamba kasi ya ongezeko la watu katika nchi hii inapungua ili kuleta ufanisi wa Maendeleo ya watu wetu yalingane na uchumi uliopo ukilinganisha na nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumejibu katika swali la msingi, iko Sera ya Idadi ya Watu ya mwaka 2006 ambayo imeainisha mambo mbalimbali ya kufanya ikiwa ni pamoja na kuhimiza familia, kwa hiari yao kupanga ni idadi gani ya watoto watakaopata na ambao unaweza kumudu katika familia.

Jambo hili likifanyika ni hatua kubwa katika kuhakikisha kwamba ukuaji wa idadi ya watu unaenda sambamba na uchumi.

Lakini la pili, ziko hatua za kiuchumi ambazo zinachukuliwa kuhakikisha kwamba uchumi unakua, kama hivi ambavyo tunatarajia uchumi wetu utakuwa kwa asilimia 10 itakapofika baada ya miaka mitano.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Ahsante Ndugu Spika, kwanza nakupa pole kwa kufiliwa na Mjomba wako, Mzee wetu Chief Abdallah Fundikira, pole sana.

Napenda kuuliza swali kwamba nchi inaweza ikawa na kukua na uchumi yaani *economic growth* lakini isiwe na Maendeleo, kutokana na ukweli kwamba unaweza kuwa unatengeneza mabomu au dhahabu na madini mbalimbali ambayo yanashikwa na makampuni machache lakini haigusi watu wa kawaida.

Kwa hiyo, kuwa na *economic growth* siyo lazima kiwe ni kigezo cha Maendeleo ya uchumi kwa watu katika nchi. Je, katika hiyo mikakati ya asilimia 10 inayowekwa nguvu inaelekezwa vipi kwa watu ili kuweko na kukua na uchumi na Maendeleo, *economic growth with development. (Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani hili sasa ni Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Jakson Makwetta, swali lake kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba kama mkijielekeza katika kukuza uchumi peke yake bila kuzingatia *income distribution* lazima utafikia mahali ambapo unaendeleza vitu badala ya kuendeleza watu. Na ndiyo maana *vision* yetu 2025 inavyotekelezwa kwa mipango ya MKUKUTA tunataka tuendeleze na tukuze uchumi lakini papo hapo tuboreshe maisha ya wananchi ndiyo maana MKUKUTA una (*cluster*) makundi/maeneo matatu.

Liko kundi la kwanza la kuendeleza uchumi *(economic growth* pamoja na kushughulikia suala la *income poverty)* lakini la pili ni (*well being)* kuboresha maisha ya wananchi ambayo hiyo tunashughulikia masuala ya elimu, maji na afya. Hapo tunapoanza ku-*distribute*.

Lakini eneo la tatu na la mwisho ni lile eneo la utawala bora na uwajibikaji. Haya yote yana malengo ya kufanya Maendeleo yawe kwa jumla ili wananchi wote waweze kunufaika katika jamii. (*Makofi*)

Na. 398

**Kutelekezwa kwa Kituo cha Kitaraka.**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati wa kubinafsishwa kwa Kiwanda cha Nyama cha *Tanganyika Packers Limited* mali nyingi za Kituo cha Kitaraka zilionekana kuwa zimetekelezwa:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya mali hizo zilizotekelezwa?

(b) Je, Serikali ilimuuzia nani Kituo hicho cha Kataraka na kwa bei gani?

**NAIBU WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo. Lakini kabla ya kujibu swali, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha kuhifadhia mifugo cha Kitaraka ni baadhi ya vituo vya *Tanganyika Packers Limited* (*TPL*) vilivyokuwa katika sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya shughuli za kununulia, kutunza, kutibu na kunenepesha ng'ombe kabla ya kuwasafirisha kwenda Kiwanda cha Dar es Salaam kwa ajili ya kuchinja na kusindika nyama katika mikebe.

Vituo vingine vilivyokuwa vinamilikiwa na *TPL* ni pamoja na Pugu (Dar es Salaam), Mloganzila (Dar es Salaam), Mtetela (Dodoma), Chibe (Shinyanga), Shiushiu (Shinyanga) na Bukene (Tabora).

Mheshimiwa Spika, Vituo vyote vilivyotajwa hapo juu ukiacha cha Kitaraka, vilirudishwa Serikalini (Wizara iliyohusika na Mifugo) kwa nyakati tofauti baada ya uzalishaji wa Kiwanda cha Nyama *TPL*, *Dar es Salaam* kushuka. Aidha, eneo la kituo cha Mloganzila liliombwana Chuo Kikuu cha Tiba, Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, *Kitaraka Holding Ground* ilibaki chini ya *TPL* kwa ajili ya kuhifadhia mifugo ya usindikaji mdogo kwa Kiwanda cha Kawe, Dar es Salaam. Mwaka 1992 usindikaji wa nyama katika Kiwanda cha *TPL Dar es Salaam* ulisimama na Serikali kutoa uamuzi kwamba Kiwanda cha *TPL* Kawe,(Dar es Salaam) Mbalizi (Mbeya), Mwalugoye (Shinyanga) na *Holding Ground* ya Kitaraka (Singida Wilaya ya Manyoni) vibinafsishwe.

Hata hivyo ilipofika mwaka 2002 Serikali ilibadilisha matumizi ya Kiwanda cha Kawe kuwa eneo la maduka makubwa na Hoteli za Kitalii. Kufuatana na uamuzi huo. Kawe ikabinafsishwa peke yake bila ya kituo cha Kitaraka. Kituo cha Kitaraka iliamuliwa kibinafsishwe peke yake, kwani matumizi yake yalilengwa kuhudumia Kiwanda cha Kawe.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kinamilikiwa na Kampuni ya *TPL* kama shamba Na. 35 lenye ukubwa wa Hekta 14,351 likiwa na thamani ya shilingi 113,500,000/- kufuatana na tathimini ya 1990. Mali zilizopo kwenye shamba ni jengo la ofisi, jengo la mzani, nyumba saba za wafanyakazi; vyote hivi vikiwa na thamani ya jumla ya shilingi 13,250,000/- Hivyo kufanya jumla ya thamani ya mali zote kuwa ni shilingi 126,750,000/-.

Eneo hili pamoja na mali zilizopo zinalindwa/kutunzwa na Serikali kupitia *PSRC* zikisubiri ubinafsishwaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatayo:-

(a) Mali zote za Kituo cha Kitaraka, hazijatelekezwa bali zinalindwa na wafanyakazi wachache waliobaki *TPL* chini ya usimamizi wa *PSRC*.

(b)Kituo cha kutunza mifugo cha Kitaraka hakijauzwa wala kubinafsishwa *PSRC* ina mkakati wa kubinafsisha kama shamba la kunenepesha mifugo (*ranch*) na kwa ajili ya mradi wa kufugia wanyama pori kibiashara.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hizo nyumba saba zinaendelea kuharibika na kwa kuwa kuna shida ya nyumba za walimu na wauguzi. Je, katika muda huu mpaka hapo itakapobinafsishwa si vema kwamba nyumba hizo zingekabidhiwa kwa Serikali ya Kijiji ili walimu waweze kukaa? (*Makofi*)

**NAIBU WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, hilo ni wazo zuri linazungumzika tunamwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane naye ili tulizungumze. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Kimbita nilikuwa napenda kumshukuru Mheshimiwa John Lwanji ameniandikia barua ya kusahihisha yale yaliyoandikwa na gazeti linaloitwa Tanzania Daima yaliyokuwa yanajaribu kudhalilisha kiti cha Spika. Alimnukuu vibaya na gazeti hilo limemnukuu vibaya na nadhani kwa makusudi. Tunayo magazeti mengi hivi sasa kazi yao kuchochea, kuchomeka hadithi zisizokuwepo na ni utoto ambao hauna hata maana.

Kwa hiyo, siku za usoni tutajua namna ya kuchukua hatua. Lakini nakushukuru Mheshimiwa Lwanji na pengine nakala ya barua hiyo lipelekewe gazeti lielewe kwamba Spika anaendelea na kazi yake na ukimwagia matope, shilingi haipotezi thamani. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 399

**Serikali kuwa na Format ya Mikataba**

**MH. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa, tumeona kasoro nyingi katika mikataba mbali mbali ambayo nchi imeingia na kampuni mbali mbali:-

Je, Serikali ina mipango gani ya kuwa na *Format* mbali mbali za mikataba *(blue print)* ambayo itakuwa imetayarishwa kama *sample* ili kwa yeyote atakayetaka kuwekeza hapa nchini afahamu kinagaubaga yapi yatakuwa ni maslahi yake, yapi yatakuwa ni maslahi ya wafanyakazi pamoja na Taifa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mikataba ni kitu kinachohitaji majadiliano baina ya pande mbili zinazohusika na kila upande huwana maslahi yake inayotaka kuyalinda. Mkataba wowote hulenga kuwianisha maslahi ya pande zote zinazohusika. Katika kuwianisha maslahi hayo, inawezekana baadhi ya masharti yakawa tofauti na yale ambayo upande mmoja ungependa yawe.

Hali hiyo inapotokea, tafsiri si kuwepo kasoro bali ni hali ya kawaida katika utaratibu wa kufanya mikataba baina ya mtu mmoja na mtu mwingine, kampuni na kampuni nyingine, Serikali na Serikali nyingine au Kampuni na Serikali. Katika mikataba inayohusisha Serikali, jitihadahufanyika ili kulinda maslahi ya Taifa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwa na *Format* mbalimbali za mikataba kama moja ya njia ya kulinda maslahi ya wafanyakazi na Taifa kwa jumla, tunayo *format* ya mikataba mbali mbakli kama vile Ukuzaji na Ulindaji wa Rasilimali *(Standard Format Agreement on the Promotion and Reciprocal Protection of Investment)*. *Format* hii ya mkataba hutumiwa katika kuendesha majadiliano ya m,kataba wa kukuza na kulinda rasilimali kati ya Tanzania na nchi nyingine Duniani.

Vile vile kuna *format* ya mikataba ya uchimbaji wa madini, uchimbaji wa mafuta na katika maeneo mengine na hutumika kama msingi wa majadiliano. *Format* hizo ziliandaliwa kwa kushirikisha wataalam mbali mbali ndani na nje ya nchi. Napenda kuwashukuru *Commonwealth Secretariat* ambao walitusaidia katika uandaaji wa *format* ya mikataba ya uchimbaji wa madini na mafuta.

Aidha, Serikali ya awamu ya nne iliunda Kamati inayoumuisha wataalam wa fani mbali mbali kuona ni jinsi gani Taifa linaweza kufaidika zaidi na rasilimali ya madini yaliyopo nchini. Kamati, imekwishawasilisha mapendekezo Serikalini na ni imani yangu kuwa mapendekezo hayo yatasaidia kuboresha zaidi *format* za mikataba ya uchimbaji wa madini na mafuta iliyopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mbali na *formats* katika mikataba ya aina mbali mbali, napenda kueleza pia kuwa baadhi ya masharti yanayotakiwa kuzingatiwa na wawekezaji yameainishwa katika sheria mbalimbali zikiwemo sheria ya madini, sheria za kodi ya mapato, sheria ya ushuru wa bidhaa, sheria ya forodha, sheria ya uwekezaji na sheria za kazi sheria ya mikataba na sheria ya utafiti wa mafuta ya petroli.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba maslahi ya taifa yataendelea kulindwa na kila inapoonekana kuna haja ya kuzirejea sheria au *format* zilizopo, Serikali haitasita kufanya hivyo.

**MH. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Naipongeza Serikali kwa kupitia mikataba hii mikubwa ya madini labda na ya mafuta na kuwa na *format* ya nchi na nchi. Lakini ipo mikataba mingine ya makampuni binafsi ambayo wale wawekezaji walipewa nafasi ya ku-*draft* ile mikataba ambayo kwa uwazi kabisa ni kwamba yalijipendelea.

(a) Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuipitia pamoja na hii mikataba ya makampuni ili kuirekebisha pale ambako maslahi ya Taifa hayakuwekwa mbele?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kurekebisha vile vipengele vya mikataba ya nyuma ambavyo maslahi ya Taifa kwa uwazi kabisa kwamba hayakuzingatiwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ingawa naona ni swali moja tu hilo naona amesisitiza tu kwa sababu sehemu ya pili ya swali inasisitiza sehemu ya kwanza.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu katika jibu la msingi mikataba yote hii tunayoingia sisi na Serikali ni ya kujadiliana kati ya huyo mtu tunayeingia naye mkataba na sisi kwa hiyo hakuna makampuni ambayo yamepitisha wao wenyewe wame-*draft* peke yao mkataba sisi tukasaini tu. Hapana mikataba yote tunazungumza nao na tunajadiliana na tunakubaliana kwa kuzingatia maslahi ya Taifa letu.

Sasa kama kuna mahali huko nyuma kumetokea mikataba ambayo haikutupa maslahi ya kutosha ndiyo maana tukasema katika jibu la msingi kwamba Serikali imeunda timu ya watalaam imeipitia mikataba hiyo na wamewasilisha ripoti yao Serikalini na Serikali inatafakari namna gani ya kuboresha mikataba hiyo. Kwa hiyo, yote haya yanashughulikiwa.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kabla ya sijauliza swali langu pamoja na udhaifu wa kanuni zetu za Bunge hili lina imani kubwa sana unavyoendesha Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Spika. (*Makofi*)

Baada ya kusema hilo naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa dhana ya kwamba ukiwa na mkataba ambao ni wa Umma *(public contract)* kwamba mkataba huu ni wa umma na Serikali inaingia mkataba kwa niaba ya Umma kwa nini Serikali sasa baada ya kujua nchi nyingi pamoja na vyombo vya taasisi za kimataifa kama *World Bank* zinaweka mikataba yake wazi mpaka kwenye *website* ni lini Serikali yetu itachukua mifano hiyo mizuri na kuweka mikataba yao katika *website* ili Watanzania wote waweze wakaona na kuzuia mashaka mashaka ya rushwa katika mikataba ambayo Serikali inaingia? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kuna mikataba ya aina mbili ambayo nchi inaingia. Kuna mikataba ya nchi na nchi au *multilateral* ya nchi na mashirika kama *World Bank* na mengine kama hayo.

Lakini kuna mikataba ya biashara ambamo humo kila nchi ina maslahi yake ambayo inajaribu kuilinda. Pengine kuiweka wazi maslahi hayo badala ya kuwa yanalindwa zaidi yakaathirika.

Kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu likubali kwamba kuna aina nyingi za mikataba na ile ambayo inabidi isiwekwe kwenye *website* itaendelea kutowekwa kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. (*Makofi*)

Na. 400

**Umuhimu wa Kiwanja cha Ndege cha Kisasa Dodoma**

**MHE. MOSSY S. MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Dodoma ni Mji Mkuu wa Tanzania na unakua kwa kasi sana hasa kwa Taasisi kubwa za kimataifa, hivyo kuufanya kuwa na ulazima wa kuwa na kiwanja kidogo cha Ndege cha kisasa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza suala hilo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa kiwanja cha ndege katika kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na shughuli za kitaifa na kimataifa, Wizara yangu imefanya usanifu wa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, kwa lengo la kukipanua. Kutokana na usanifu huo imegundulika kwamba eneo lililopo ni dogo na halitoshelezi kuendeleza kiwanja kufikia hadhi ya kimataifa. Ili kiwanja hicho kipanuliwe itabidi kuvunja baadhi ya nyumba na kuhamisha miundombinu mingine hivyo gharama yake itakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, mamlaka ya Viwanja vya Ndege ikishirikiana na *CDA* wamepima eneo jipya kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya chenye hadhi ya kimataifa na chenye uwezo wa kuchukua ndege kubwa kama ya *Boeing* 737. (*Makofi*)

Hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Kwanza eneo la kujenga kiwanja kipya limepatikana sehemu ya Msalato, ndani ya Manispaa ya Dodoma. Hati miliki imekwishatolewa. (*Makofi*)

Zimepatikana fedha za msaada kutoka *BADEA* kiasi cha dola za Kimarekani 440,000 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Usanifu huo utahusisha miundombinu yote inayotakiwa kwa ajili ya kiwanja kipya cha ndege ikiwemo njia ya kutua na kurukia ndege, maegesho ya ndege, njia za viungio, barabara ya magari kwenda kiwanjani na maegesho ya magari upande mwingine utahusisha jengo la abiria, jengo kwa ajili ya matengenezo ya ndege, jengo la mizigo, mifumo ya usalama na uongozaji ndege na hali ya hewa. Miundombinu yote itasanifiwa kwa kiwango kitachowezesha kutumika kwa ndege kubwa.

Mheshimiwa Spika, *BADEA* imeonyesha nia ya kufadhili ujenzi wa kiwanja hiki mara upembuzi yakinifu, usanifu na makadirio ya gharama za ujenzi kukamilika. Mamlaka ya viwanja vya ndege itaendelea kukifanyia ukarabati Kiwanja cha Ndege cha Dodoma, kilichopo ili kiweze kutoa huduma nzuri. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 mamlaka ya viwanja vya ndege imetenga kiasi cha Tshs. 650 milioni kwa ajili ya kuweka mfumo wa taa kwenye njia ya kurukia na kutua ndege ili kuwezesha safari za usiku.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea nadhani jibu linajitosheleza kabisa.

Na. 401

**Barabara ya Dodoma – Manyoni na Singida – Manyoni**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza

Kwa kuwa, nia ya Serikali ni kujenga barabara ya Dodoma – Manyoni na Singida – Manyoni kwa lami; na kwa kuwa Wakandarasi wanajenga kwa kusuasua mno na kusababisha kuwa nyuma ya wakati, na kwa kuwa barabara hizo zimekuwa ni kero sana nyakati za masika.

Je Serikali inasema nini juu ya wakandarasi hao walioshindwa kukamilisha ujenzi kwa barabara hizo kwa wakati uliokubalika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Manyoni na Manyoni hadi Singida umechelewa. Kulingana na ratiba ya utekelezaji, ujenzi wa miradi hiyo ulitakiwa kukamilika mwezi Agosti na Septemba, 2006.

Kutokana na tatizo hilo Serikali kupitia Wizara yangu imepitia na kuchambua mapungufu yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mikataba hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Kwa upande wa barabara ya Dodoma – Manyoni (km.127), Ucheleweshaji wa mradi huu ulitokana kwa kiasi kikubwa na mapungufu ya ushauri wa kitaalam wa mhandisi mshauri wa mradi. Mhandisi Mshauri huyo ameondolewa kwenye mradi mwezi Aprili 2007. Tayari Mhandisi Mshauri mwingine wa mradi ameajiriwa na ameanza kazi mwezi Mei 2007. Kazi ya ujenzi inaendelea na hadi sasa kilometea 70 za barabara zimekwisha jengwa kwa kiwango cha lami na mradi unatarajiwa kukamilika Disemba 2008

(ii) Kwa Upande wa barabara ya Singida – Manyoni (km.118), Ucheleweshaji ulitokana na mapungufu ya uongozi kwa upande wa mkandarasi. Serikali imechukua hatua ya kukatisha mkataba na kampuni iliyokuwa inajenga barabara hii na sasa mkandarasi huyu atajengea kilometa 63 tu kuanzia Mjini Singida hadi Kijiji cha Issuna. Sehemu hii ya barabara inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa sehemu iliyobaki kati ya Issuna – Manyoni yenye urefu wa kilometa 55 zimeitishwa mwezi Aprili 2007 na zimerudisha mwezi Juni 2007.

Uchambuzi wa zabuni hizi unaendelea na tunatarajia kwamba mwezi huu Agosti 2007 mkandarasi atakuwa amepatikana tayari kuanza ujenzi wa sehemu hii kwa lengo la kukamilisha mradi huu ifikapo mwaka 2010.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri mapungufu yaliyojitokeza katika barabara zote za kutoka Dodoma mpaka Shelui na kwa kuwa barabara ya Shelui – Singida yenye mkandarasi mmoja lakini imegawanywa katika mafungu matatu kwa maana ya mainjinia watatu imeonyesha kasi kubwa ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo. Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya barabara ambayo imetangazwa *tender* hivi karibuni ya kutoka Issuna kwenda Manyoni, kuwa na mainjinia wawili kwa maana mmoja atoke Issuna kuelekea Manyoni na mwingine atoke Manyoni kuelekea Issuna ili kasi ya kukamilika kwa barabara hiyo iwepo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo yenye kilometa 55 tayari zabuni zilishatangwa zilishapokelewa zinafanyiwa *valuation* kwa sasa na kwa kweli ilivyotangazwa ni kwamba ni mkandarasi mmoja atafanya kazi hiyo, kurudi nyuma na kuanza kuigawa tutakuwa tunarudi nyuma zaidi ambapo nia yetu kwa kweli ni kukamilisha barabara hii mapema iwezekanavyo. Tuhakikishe tu kwamba tutasimamia vizuri utekelezaji wa mradi huu ili barabara hii iweze kukamilika kama tulivyopangwa kabla ya mwisho wa mwaka 2010. *(Makofi)*

Na. 402

**Mgawanyo wa Fedha za Mfuko wa Barabara.**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Je, ni vigezo gani hutumika katika kugawa fedha zinazokusanywa na Mfuko wa Barabara nchini kwa ajili ya barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri za Jiji, Manispaa na Wilaya nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka 2006/2007 vigezo vilivyokuwa vinatumiwa na TAMISEMI katika kugawia Halmashauri zake fedha wanazopewa na mfuko wa barabara ilikuwa kama ifuatavyo:-

Asilimia 85 (85%) ya fedha hizo hugawiwa kwa uwiano unaolingana na Halmashauri zote za Wilaya na Miji. Kigezo hiki hujulikana kama *equity criteria*.

Asilimia 3.5 (3.5%) ya fedha hizo hugawanywa kwa Halmashauri kulingana na idadi ya watu *(proportion to population).*

Asilimia moja (3.5%) nyingine hugawanywa kwa Halmashauri kwa kuzingatia ukubwa wa mtandao wa barabara.

Asilimia 1 ya fedha hizo hutengwa kwa ajili ya Programu ya Ukarabati wa miundombinu ya miji (*Urban Sector Rehabilitation Programme).*

Asilimia nne (4%) ya fedha hizo hugawiwa Halmashauri za Miji *(Municipal Council)* kwa uwiano unaolingana.

Asilimia mbili (2%) ya fedha hizo hugawiwa kwa Halmashauri za Miji Midogo *(Town Councils)* kwa uwiano ulio sawa.

Asilimia moja hubakia Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kugharamia uratibu na usimamizi wa shughuli zote chini ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, vigezo hivi vililalamikiwa na baadhi ya Halmashauri kwa kuwa Halmashauri zote zilikuwa zinapata mgao ambao ulikuwa unakaribiana bila kujali mahitaji halisi ya Halmashauri husika. Bodi ya Mfuko ilikubaliana na suala hili na hivyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ilikubalika kwamba kuanzia mwaka huu wa 2007/2008 kigezo kikubwa zitakachotumika kugawa fedha za Mfuko wa Barabara ni mahitaji ya matengenezo ya barabara kwenye kila Halmashauri. Kigezo hiki kinazingatia urefu wa barabara aina ya barabara yaani lami, changarawe ama udongo na hali ya barabara (*road condition*). Kwa misingi hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa mwaka huu wa 2007/2008 itagawa fedha za Mfuko wa Barabara kwa kuzingatia mahitaji ya matengenezo ya barabara kwenye kila Halmashauri.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na kwamba wameliona na kwamba kulikuwa na malalamiko kuhusu mgawanyo wa fedha za Halmashauri. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa sababu tatizo kubwa bado ni kiasi cha fedha ambacho kinapelekwa kwenye Halmashauri nchini ambazo kwa kweli ndizo zina mtandao mkubwa wa barabara nchini na kwa kuwa ni asilimia 30 tu ambayo hupelekwa Halmashauri za Wilaya nchini kote na katika hiyo asilimia 30 bado asilimia moja hubaki kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa ajili ya kushughulikia mambo mengine madogo madogo.

Je, ni lini sasa Wizara itafikiria kuongeza walau kiwango hicho kwa asilimia ili Halmashauri ziweze kupata walau asilimia 40 na kwa maana hiyo ziweze kutengeneza barabara vizuri zaidi nchini? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, anayosema ni kweli kwamba Halmashauri zinapata asilimia 30 na asilimia 70 hubaki *TANROADS* kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za Mikoa ingawaje na huko vile vile fedha za usimamizi vile vile kuna asilimia inayobaki. Lakini niseme tu kwamba ni ukweli ulio wazi matengenezo ya *(trunk road)* barabara kuu na *regional roads* zinahitaji fedha nyingi sana ingawaje mtandao wake ni mfupi kuliko ule wa vijijini. Kwa maana hiyo, hesabu hiyo hii ilichukuliwa kwa kuzingatia umuhimu wa kufungua nchi yetu kwa barabara kuu na kuzitengeneza barabara hizo ambazo ni za lami na vile vile kurekebisha barabara za Mikoa. Hiyo, kwamba asilimia ni ndogo kwa sasa tunachoweza kufanya ni kuongeza fedha kwa kweli ambacho nadhani ni muhimu ni fedha kuongezeka za matengenezo kuliko kusema asilimia iweze kupanda. Ndiyo maana mwaka huu katika Halmashauri badala ya shilingi bilioni 25 za mwaka jana, safari hii wamepata bilioni 65 ni ongezeko ambalo linaweza likaleta *impact* kwenye Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Na. 403

**Ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji Muhukuru**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA**: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka huu Serikali imeshaonyesha azma ya kutoa hiyo milioni 20 ili kituo cha Uhamiaji kijengwe kwa mwaka huu wa 2007/2008 sioni umuhimu wa swali hili kuendelea kujibiwa ila nasubiri utekelezaji wa Serikali. Hivyo naliondoa swali langu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, umetupunguzia na muda. Lakini Naibu Waziri alishakuja mpaka huku basi mtasikilizana namna ya kumlipa fidia kwa kuhangaika mpaka huku halafu wala asijibu swali. *(Kicheko)*

Na. 404

**Mipango ya Kuinua Michezo Nchini**

**MHE. EZEKIEL MAGOLYO MAIGE** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali ya awamu ya nne imepania kuinua michezo nchini na kwa kuwa, Serikali ilishatoa agizo kwa kila Halmashauri kuchangia asilimia tano (5%) ya mapato yake kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza vijana:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuziagiza Halmashauri zitumie sehemu ya fungu hilo kununulia vifaa vya michezo kama mipira na jezi ili kuwapa vijana fursa ya kuonyesha vipaji vyao kuliko hivi sasa ambapo Serikali haina kabisa mfumo rasmi wa kusaidia vifaa vya michezo na hivyo kuwafanya vijana kutegemea zaidi misaada toka kwa wafadhili hasa Wabunge?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuanzisha mfuko wa Maendeleo ya michezo katika wilaya kwa ajili ya kulipia gharama kama za kujenga au kukarabati viwanja vya michezo na kununulia vifaa vya michezo ili kusaidia kuinua kiwanda cha michezo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi naomba nichukue nafasi hii, kukupa pole kwa kufiwa na babu yetu ambaye wewe ni Mjomba wako.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige (Msalala) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali tayari ilikwishatoa agizo kwa Halmashauri zote nchini kuchangia asilimia tano (5%) ya mapato yake kwa ajili ya Maendeleo ya vijana, ni wajibu wa Halmashuri zenyewe kukaa na kupanga jinsi ya kuzitumia fedha za mfuko huo.

Naomba Waheshimiwa Wabunge wote, akiwemo Mheshimiwa Maige, wahimize Halmashauri zao kutenga fedha kwa asilimia fulani kwa kukuza na kuendeleza michezo katika Wilaya zao. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuendelea kuwasaidia vijana katika kuinua michezo pindi wanapohitaji, kwani Wabunge pia ni wafadhili wa wananchi kwa namna moja ama nyingine.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzisha mfuko wa Maendeleo ya michezo katika wilaya ni jambo linalowezekana limo ndani ya uwezo wa wilaya vile vile wilaya kwa kupitia vikao vyake inaweza kuamua kuwa na mfuko kwa ajili ya Maendeleo ya michezo na miundombinu ya kueneza michezo katika wilaya zao.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Naibu Spika hasa kifungu kinaelekeza kwa halmashauri ndio ifanye uamuzi jibu ambalo mara kadhaa limekuwa ndio jibu la Serikali Kuu na kwa kuwa mara kadhaa kwenye Halmashauri kwa kuwa kunakuwepo na miongozo mbalimbali ambayo inakuwa imetoka Serikali Kuu na kwa maana hiyo wanakuwa na uwezo mdogo sana wa kuamua vinginevyo zaidi ya vile ambavyo wanakuwa wameelekezwa.

Je, Serikali kwa ajili ya kuhimiza michezo inaonaje ikitoa mwongozo maalum kwamba uwepo mkakati fulani wa kusaidia wanamichezo katika maeneo ya mwanzo kabisa ili kukuza vipaji vya vijana wetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO- MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezekiel Maige kama ifuatavyo. Swali lake ni la msingi sana na tunakubaliana naye kabisa lakini ni vizuri tukatambua kwamba katika mwongozo mzima wa Maendeleo ya michezo nchini wilaya ina sehemu yake kwa sababu utaratibu mzima wa uongozi wa *sports administration* kwamba Halmashauri zinayo Kamati ya Maendeleo ya Michezo ambayo *DAS* yeye ndiye Mwenyekiti, halafu Katibu ni Mkurugenzi Mtendaji pamoja na wajumbe wake.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kwa kuzingatia kwamba michezo ni sehemu mojawapo muhimu sana wao wanatakiwa wawe na mikakati ya kuendeleza michezo mkakati wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Lakini kwa jinsi alivyosema sisi kama Wizara tunasisitiza na tutawaletea mwongozo ili muweze kuona kwamba kuna umuhimu wa michezo au ni muhimu kupangiwa mikakati yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa wote upande wa kushoto, kulia waliouliza swali wanataka nyongeza inaonekana mmenong’onezana. (*Kicheko*)

**MHE. VITA M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi naomba niungane na wenzangu kwa kukupa pole kwa kufiwa na mjomba wako na ambaye ni babu yetu Marehemu Mzee Chifu Abdallah Fundikira.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika suala la michezo wa mpira wa miguu tumepania kuukuza hapa nchini na kwa kuwa tunao hazina ya wachezaji wa zamani wa Timu yetu ya Tafa *(Taifa Stars)* ambao waliweza kuifikisha nchi yetu katika kiwango cha juu cha mpira na kutuletea sifa, nikiwataja wachache kama Peter Tino na wengineo. Je, serikali inaweza kuwafikiria katika mpango wake wa kurudisha mashindano ya michezo shuleni wachezaji hao wa zamani wakapata *special training* na kuweza kufundisha mchezo huo na kutoa fursa ya kufundisha na kutoa ujuzi wao walioupata wakati huo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Vita Kawawa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, wazo lake ni zuri ni kwamba wachezaji hao ni wachezaji ambao tayari wameshapata uzoefu wa kutosha na kawaida mchezaji ambaye anafikia hatua ya kucheza Timu ya Taifa ni rahisi kufundishika kwenye nafasi ya ukocha. Kwa hiyo, tunayo mikakati na tunawaomba wachezaji hao wajitokeze kunapokuwa na mafunzo ya ukocha katika ngazi mbalimbali ngazi ya awali, ngazi ya kati na *advanced* wajitokeze ili waweze kupata mafunzo na nataka nimhakikishie kwamba kwa ujuzi wao ni rahisi kuwatumia.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili alilolizungumza ni kwamba tayari Serikali ina mkakati mzuri tu wa kurudisha michezo ya Shule za Msingi, Shule za Sekondari na Vyuo. Kwa hiyo, hawa watakaopata mafunzo ni rahisi kuwatumia kama nchi nyingine wanavyofanya na ninafurahi jana tumecheza na timu ambayo iliingia fainali mwaka 1980

wametufunga goli moja kwa tabu sana. Lakini wote walikuwepo na tuliweza kuwa na mchezo mzuri pale kiwanjani jana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa muda wa maswali umeisha na maswali yameisha yaliyobaki ni matangazo tu. Kwanza kwa niaba ya familia yetu napenda niwashukuru wote wale ambao kwa namna moja au nyingine wametugusa katika wakati mgumu wiki iliyopita nilipofiwa na mjomba Chifu Abdallah Fundikira. Napenda nimeshukuru sana Mheshimiwa Rais Mama Salma Kikwete, ambao walikuja Tabora wakavunja shughuli za ziara walipokuwa wakaja Tabora wakashiriki nasi wakakaa mpaka usiku na kwa kweli walilala hadi wakaondoka siku ya pili. Kwa hiyo, walikuja msibani kweli kweli. Pamoja na hao napenda niwashukuru sana wazee wetu wafuatao Mzee Rashid Kawawa na Mama Kawawa, walishiriki nasi kule. Mzee *Sir* George Kahama na Mheshimiwa Mama Janet Kahama, ambaye ni Mbunge mwenzetu hapa tulikuwa nao huko. Bila kumsahau Mzee John Malecela ambaye naye tulikuwa naye wakati wote. (*Makofi*)

Pia kipekee niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliowakilisha Wabunge wa aina zetu tofauti kutoka Chama cha Mapinduzi, kutoka Kambi ya Upinzani, kuzingatia jinsia tulikuwa pamoja kule na walitufariji sana. Pia, Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna mbalimbali wengine mmefika nyumbani mmetuona, wengine walikiri hawajui hata uhusiano kwa nchi yetu usishangae hata kidogo usidhani kwamba katika ukoo kunaweza kuwa na dhehebu moja tu. Sisi ni ukoo ni mpana tuna madhehebu mengi na ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, tunashukuru sana wale wote waliofahamu kwamba mzee huyu ni mjomba wangu na baadhi ya wale tuliosoma nao kama Waziri wa Afya, Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, anafahamu kabisa jinsi alivyokuwa ananiletea vitabu pale *Tabora School* wakati huo, ili nijiendeleze kwa kiingereza. Kwa hiyo, ni pigo kwetu lakini tunafarijika kwamba wengi mmetufariji na kutugusa kwa namna nyingi, salaam nyingi za rambirambi hadi leo, tunachoomba tu ni kwamba tuendelee kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili amsitiri mzee huyu mahali pema peponi. *Amen*.

Mheshimiwa Capt John Chiligati Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana anao wageni mashuhuru wafuatao ambao nadhani wako hapa ni ujumbe mzito wa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto kutoka *SMZ* kule Zanzibar, unaongozwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, Waziri huyu ndiyo Waziri mwenyewe, pamoja nae yupo Katibu Mkuu Bwana Harid Salum Mohamed. Naona hapa wana harakati wa *gander* wanafurahia kabisa Waziri ni Mwanamke na Katibu Mkuu ndiyo mwanaume. Pia yupo Ndugu Idd Mapuri Kamishna wa Kazi, Mohamed S. Ally, Mkurugenzi wa Vijana, Bi Rahma Ali Khamis, Mkugenzi wa Wanawake na Watoto.

Wengine ni Ndugu Haji Sinai Machano, Mrajisi wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri, Ndugu Maua Rajab Makame, Afisa Mdhamini, Bi. Fatma Mohamed Juma, Afisa Maendeleo ya Jamii, Bi. Radhia Rashid Haroub, Afisa Maendeleo ya Wanawake na Watoto na Bi. Fatma Omary Mohamed, Afisa Habari. Karibuni sana Ndugu zetu kutoka Zanzibar tunafurahi mara kwa mara tunapotembeleana kwa sababu inazidi kutuimarisha katika umoja wetu. (*Makofi*)

Wapo wageni wa *TAPAC* ambao Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o, Mwenyekiti wetu wa *TAPAC* wamekuja kututembelea ameniarifu hao wametoka *Germany Foundation for World Population* na wanaitwa *the Young Decision Makers from European Union* kwa majina kutoka Finland ni Ndugu Simon Hamalainen, kutoka Hispania Ndugu Mark Jumaness, kutoka Ufaransa Ndugu Aloyce Ligou, kutoka Ubelgiji Ndugu Bi. Anny Pascal Momerance, kutoka Moldova ni Ndugu Grigole Petrenco na C*ountry Director* ambaye ni Mtanzania ni Ndugu Peter Munene. *Our visitors we are very happy to welcome you here into the chamber of the houses of Parliament of Tanzani. Send our greetings when you go back and please come back next time and inform others about the beauty of Tanzania and people of Tanzania and keep on coming back*. *(Makofi*)

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Phillip Marmo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora ana wageni wafuatao Bwana M. Matie ni Afisa Tawala wa Mbulu, huyu ni mtendaji kwa hiyo hajajua mikogo nikitambulisha Madiwani mtaona tu wanakawia kidogo ili kamera iweze kuwavuta sasa huyu amesimama na kukaa hapo hapo *the Publics Loyal Servant*. Bwana Mayomba wa Haidom, Bwana J. Anael wa Gehandu, hao wameambatana na walimu wakuu wa Shule za Msingi zilizofanya vizuri katika mitihani ya mwaka 2006 ni vizuri tuwatambue Mwalimu P. Munisi shule yake inaitwa Getayamba, Mwalimu Nogoria, shule yake inaitwa Dongobesa, Mwalimu Geheri, wa Shule ya Kuta, Mwalimu T. Ally wa Guneneda, Mwalimu Nayo wa shule ya Gindaba, Mwalimu Muraida ni Mwalimu Mkuu wa Endachagadaki, Mwalimu Daniel ni Mwalimu Mkuu wa Kamatananati, Mwalimu Mmasi wa shule ya Waama, Mwalimu Nicolas wa shule ya Titiwi na Mwalimu Amnai wa shule ya Gehandu. Mheshimiwa Phillip Marmo nadhani nastahili angalau soda baada ya hapa kwa sababu haya majina magumu sana, karibuni sana wageni wetu kutoka Mbulu. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Miundombinu, ni Mheshimiwa Asaa Simba, Diwani wa Kata ya Vingunguti na Katibu wa Baraza la Diwani wa CCM Manispaa ya Ilala, Ndugu Lucy Isidori, Katibu wa wazazi Wilaya ya Moshi Mjini. Wageni wa Mheshimiwa Bernadeta Mushashu ni Upendo Mushashu ambaye ni mwanaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Hilbert Kairuki Dar es Salaam na Bi. Diana Mushashu mwanafunzi *Saint Augustine Univesrsity, Mwanza.* Yeye mwenyewe kama bingwa katika kufundisha na ni mwalimu maarufu naona anaendeleza watoto katika taaluma mbalimbali, tunakupongeza sana Mheshimiwa Bernadeta Mushashu. *(Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Raphael Mwalyosi ni mkewe ambaye hakumtaja jina, Mrs Mwalyosi nadhani udhuru kidogo, wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari Msalato Dodoma kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge mnafahamu Shule ya Msalato ni Shule ya vipaji maalum. Kwa hiyo, hapo kuna m-*scientist* wetu wa baadaye, wahandisi, madaktari na hata wanasiasa ingawa haihitaji taaluma kubwa sana kuwa mwanasiasa. (*Makofi/Kicheko*)

Pia kuna wanafunzi 40 kutoka Shule ya Msingi Makole naona wamekosa nafasi, wanafunzi 30 kutoka Shule ya Sekondari Viwandani Dodoma, wanafunzi 35 kutoka Shule ya Awali na Msingi Chemchemi Dodoma nadhani ni hao kulia pamoja na walimu

bado ni wadogo kweli wako shule ya awali basi kuanzia shule ya awali, msingi na sekondari tunafurahi sana walimu muwe na utaratibu huu huu wa kuwaleta watoto wetu kuweza kuona moja kwa moja au Kiswahili cha sasa *live* Bunge linavyoendesha shughuli zake, wapo pia wanafunzi 10 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tunawatakia mema katika mafunzo ya Chuo Kikuu ni magumu sana lakini Mungu atawasaidia tunawahitaji sana. Naomba nitambue sasa wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mkewe Stellah Cheyo nadhani yupo *Speakers Gallery*, wapo watoto wao nao ni Momose Cheyo na Mange Cheyo, natumaini mtafuata nyayo za Mzee Cheyo angalau mmoja wenu basi nyie vijana mtafuata katika nyayo za baba yenu lakini muende Chama cha Mapinduzi. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa leo kutakuwa na kikao cha Kamati ya Utendaji ya *TAPAC* kama mlivyoona tuna wageni wetu hapa. Kwa hiyo, ni kikao muhimu sana saa tano asubuhi katika ukumbi Namba 133, wajumbe wa Kamati ya Uongozi Tume ya Huduma za Bunge Kamati ya Kanuni za Bunge na Kamati ndogo iliyopitia kanuni za Bunge wanarifiwa kuwa kutakuwa na kikao cha pamoja, Kamati ndogo ya Mheshimiwa Ndugai ingawa yeye mwenyewe hatakuwepo kwa sababu atakuwa anafanya shughuli nyingine muhimu. Ningeomba kama itawezekana kiwe saa sita na nusu katika Ukumbi wa Spika kwa sababu kuna mikutano mingine. Kuhusu tangazo hili tu ningetangaza Waheshimiwa Wabunge muangalie kwenye *pigeon hole* mtagawiwa rasimu ya Kanuni mpya, nasema rasimu kwa makusudi kabisa kwa sababu bado ni mapendekezo tu. *(Makofi)*

Naomba kila Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu kesho kutwa siku ya Jumatano tutaanza kuzingatia masuala ya Kanuni za Bunge. Kumekuwa na malalamiko mengi jambo hili limekuwa ni jitihada ya kurahisisha rejea na kuziweka katika mtiririko mzuri ili Kanuni zetu ziweze kufanya kazi rahisi ya kusimamia na kuishauri Serikali, tunaomba msome ili tuwe na mjadala mzuri kuanzia Jumatano.

Mheshimiwa George Lubeleje sina hakika kama kumetokea ajali kule Wilaya ya Mpwapwa wachezaji waliokuwa katika malori mawili nadhani kwa sababu idadi ni 70 waliojeruhiwa na wawili wamefariki Dunia. Kwa hiyo, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa George Simbawene, wameniomba ruhusu waondoke, lakini niseme tu Mheshimiwa George Lubeleje, ameomba kuwe na mkutano mfupi saa saba mchana katika ukumbi namba 219 wa Kamati hii ya Katiba. Sheria na Utawala Makamu Mwenyekiti analielewa suala lenyewe.

Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wafahamu kutakuwa na kikao cha Kamati ya chama leo saa saba mchana Ukumbi wa Pius Msekwa, kuna sahisho hapa mkewe Mheshimiwa Cheyo ni Elizabeth Cheyo na siyo Stella Cheyo kama ilivyotamkwa awali, au unao wawili? *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Stella ni mwanangu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Samahani sana Mheshimiwa John Cheyo, kwa hiyo Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi saa saba mchana, Ukumbi wa Pius Msekwa, taarifa hii nimeletewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa niaba ya Katibu.

Juzi timu yetu ilienda Mpwapwa na kama kawaida ikapata ushindi. Timu ya soka ya mpira wa miguu ikawafunga ma-*veterinary* wa Mpwapwa goli moja bila. Ninamshukuru Mheshimiwa George Lubeleje hakutaharuki sana kwa sababu nadhani pia ni Mbunge. Kwa hiyo, aliona basi ndiyo tena. Jana Naibu Waziri Bendera alitangaza matokeo ya mpira lakini kwa kweli mpira huu ni wa ajabu sana kwa sababu ulichezwa dakika 45 tu. Kwa hiyo, kwa kuwa kawaida ya Bunge ni kufunga magoli ya kushtukiza katika *half* ya pili nadhani matokeo haya ni batili kabisa itabidi timu yetu irudiane na hawa ma-*veterinary* na *Captain* Adam Malima ananiambia kwamba katika hiyo dakika 45 mchezo ulipovunjwa hawa ma-*veterinary* wa Timu ya Taifa ya zamani walikuwa ulimi nje, walikuwa wamechoka kabisa. Kwa hiyo, ni dhahiri lazima turudiane ili kuendeleza ile *record* yetu ya kuzifunga timu tunazokutana nazo. Waheshimiwa Wabunge baada ya hayo matangazo, nitamwomba Mwenyekiti Job Ndugai aweze kuja kushika kiti kwa sababu nina mikutano mingine kule ofisini.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2007
### *(The Finance Bill, 2007)*

(*Majadiliano Yanaendelea*)

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y.MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi katika Wizara ya Fedha ambaye pia ni kiongozi wa Kambi ya Upinzania Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2007 pamoja na marekebisho kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43 (5c) toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kambi Upinzani kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Spika na familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa Hayati Chifu AMarehemu mahali pema peponi. *Amen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Fedha ni moja ya sheria muhimu sana, hii ni sheria inayohusika na mapato ya Serikali, sheria nyingine muhimu ni ile ya matumizi ambayo ndiyo inaidhinisha kufanya matumizi ya Serikali. Juzi tumepitisha matumizi ya Serikali kabla ya kupitisha mapato, Kambi ya Upinzani inashauri hili liangaliwe kama ni sahihi kwani maoni ya Kambi ya Upinzani si vema kuanza kujadili na kukubaliana kutumia kabla hatujajua tunatumia kutoka wapi, utaratibu wa siku zote ni wa kupitisha Sheria ya Fedha kabla ya Sheria ya Matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia kupitia Muswada wa Fedha inapendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria wa bidhaa sura namba 147 kwa kuweka kifungu kipya cha 124 (1a) kifungu hiki kinarasimisha ndani ya sheria utaratibu wa kuirejesha Seriakali ya Mapinduzi Zanzibar, makusanyo ya ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kuuzwa au kutumika Zanzibar. Lengo la kurasimisha huku ni zuri sana na litaisaidia Seriakali ya Mapinduzi Zanzibar kupata fedha za kodi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 35 (1) inataka fedha zote za Jamhuri ya Muungano kuingia katika mfuko mkuuwa Hazina ninaomba kunukuu, Ibara ya 135 (1) fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa fedha za aina iliyoitwa katika Ibara ndogo ya 2 ya Ibara hii zitawekwa katika mfuko mmoja maalum ambao unaitwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, Ibara ya 135 (2) fedha ambazo hazitawekwa kwenye mfuko mkuu wa Hazina ya Serikali ni zile zote ambazo zimetajwa na sheria zitumike kwa shughuli maalum au ziwekwe katika mfuko mwingine kwa ajili ya matumizi maalum, mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nyongeza ya kwanza ya Katiba inayotaja mambo ya Muungano orodha namba 10 inataja ushuru wa bidhaa, hii inadhibitisha kuwa fedha zinazotajwa na mabadiliko haya ya sheria hii yanayoletwa na Waziri wa Fedha ni fedha ya Jamhuri ya Muungano ambayo lazima iingize kwanza mfuko mkuu wa Hazina kabla ya kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita tumepitisha sheria ya matumizi ili kutoa fedha katika mfuko mkuu wa Hazina kwa matumizi mbalimbali ya Serikali, fedha zilizopitishwa ni pamoja na zile zitakazokusanywa kutoka katika ushuru wa bidhaa kama fedha hizi zikipelekwa Zanzibar kabla ya kuingia mfuko mkuu Hazina tutakuwa tumekiuka sheria ya matumizi ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wasiwasi kuwa mabadiliko haya ya sheria hii yanavunja katiba ya nchi Ibara ya 35, tunaomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri ili Bunge lako lijiridhishe kuwa hatujavunja katiba.

Kambi ya Upinzani inapenda sana kero za Muungano kumalizwa lakini si kwa gharama za kuvunja Katiba ya nchi yetu, tusijeweke *presidency* inayoweza kutuingiza katika matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye ushuru wa bidhaa sura namba 147 katika kifungu cha 124 na jedwali la nne kwa bidhaa mbalimbali kuongeza ushuru wa kiwango cha asilimia saba kila mwaka ili kuendana na kiwango cha mfuko wa bei na hivyo kulinda thamani ya mapato ya Serikali katika vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la kodi katika bidhaa za mafuta yaani *diesel* nzito *(IDO)* ya kuendesha mitambo viwandani, mafuta mazito ya mitambo na *petrol*

siyo tu imeleta athari katika usafirisha wa abiria kama ambavyo imethibitika sasa katika jamii.

Bali pia madhara yake yameingia mpaka katika bidhaa zinazozalishwa mashambani na kuuzwa katika masoko yetu katika mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondoa ongezeko la ushuru katika mafuta ya taa na kuliweka katika dizeli na petroli imethibitika kweli kuwa ni kiini macho kutaka kuaminisha wananchi kuwa Serikali haijaongeza bei ya mafuta ya taa. Kwa sasa matokeo haya si nadharia tena kwani yamekwishaonekana maana bei za mafuta zimepanda sana na kuleta lawama kubwa kwa wananchi wa kawaida. Kilio cha kupanda bei za mafuta kilikuwa kikubwa kama ilivyojionyesha juzi katika mabango ya wafanyakazi walioandamana Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania kuwa shida hizi zitaisha lini? Je, marekebisho ya Sheria ya *EWURA* na ile ya petroli ambayo ni sehemu ya Muswada huu yatashusha bei zilizopanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu kufanya utafiti mdogo ili kujua gharama za kupanda kwa maisha ya wananchi na tumegundua upandaji uliokithiri wa bei za bidhaa, utafiti wetu umeonyesha bei za bidhaa mbalimbali katika maduka nchini kabla ya bajeti kusomwa hapo mwezi wa sita na hali ya sasa ya bei za bidhaa matokeo ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam sementi mfuko mmoja ulikuwa shilingi 10,500/= na bei ya sasa ni shilingi 14500/=. Bukoba Mjini sementi mfuko mmoja ulikuwa shilingi 14,000/=, bei ya sasa ni shilingi 18000/=, Ruvuma mche wa sabuni ulikuwa ni shilingi 500/= na bei ya sasa ni shilingi 1000/=, chumvi paketi moja katika Mkoa wa Ruvuma ilikuwa ni shilingi 100/= na sasa ni shilingi 500/=. Sukari kilo moja katika Mkoa wa Ruvuma ilikuwa ni shilling 1,200/= na sasa ni shilingi 1,500/=, ngano kilo moja ilikuwa ni shilingi 500/= na sasa ni shilingi 700/=.

Muleba sukari kilo moja ilikuwa ni shilingi 1,500/= na sasa ni shilingi 1,700/=, mche wa sabuni ulikuwa ni shilingi 800/= na sasa ni shilingi 900/=. Karagwe mche wa sabuni ulikuwa ni shilingi 900/= na sasa ni shilingi 1000/=, sukari kilo moja ilikuwa shilingi 1,500/= na sasa ni shilingi 1,700/=. Mikoa mingine kadhaa mafuta ya taa yamepanda kutoka shilingi 1,200/= mpaka shilingi 1,700/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utafiti wetu yanathibitishwa na ripoti ya Benki ya Tanzania ya mwezi Julai, taarifa ya Benki Kuu inaonyesha kuwa mfumuko wa bei umepanda kutoka 5.0% wakati bajeti inasomwa mpaka 5.9% mwisho wa mwezi Julai, 2007. Kiuchumi na hasa thamani ya pato la mwananchi upandaji huu wa 0.9% ndani ya mwezi mmoja ni mkubwa mnao. Hii ina maana kuwa shilingi mia ya mwezi Juni , 2007 ilishuka na kuwa shilingi 99.1 mwezi Julai, 2007. Hali hii ni mbaya zaidi kwa mfumuko wa bei katika vyakula kwani wakati mwezi Juni mfumuko ulikuwa 2.8%. Mwezi Julai mfumuko wa bei za vyakula ulipanda na kufikia asilimia 4.6% ambayo ni takriban maradufu. Hii ina maana kuwa chakula walichokuwa akikinunua mwananchi mwezi mmoja tu baada ya bajeti ananunua kwa shilingi 122.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yanayopendekezwa na Serikali katika Sheria ya Fedha yataumiza zaidi wananchi. Kambi ya Upinzani inashauri yasifanyike kwa kuwa mabadiliko haya yataifanya Serikali kukusanya shilingi bilioni 34 tu ni vema iachane nayo, kwani tayari Waziri wa Maliasili na Utalii. Amekwishafanya marekebisho makubwa katika tozo za magogo na uwindaji na hivyo Serikali kukusanya shilingi bilioni 40 zaidi kuziba pengo la marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri Kivuli wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Kambi ya Upinzani ilipongeza juhudi za Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako Tukufu katika kuleta muafaka wa ubinafsishaji wa Shirika la Bima ya Taifa. Kambi ya Upinzania ilidhani kufuatia muafaka huu Waziri wa Fedha angeunganisha katika Muswada huu wa marekebisho ya Sheria ya Bima ya mwaka 1996 ili kulifanya Shirika la Bima la Taifa kuweka bima za lazima za mashirika makubwa ya Serikali kama Benki Kuu na kadhalika. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Fedha ili kulinda shirika la Bima au kutoa maelezo ya kina ni lini atachukua hatua hiyo muhimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia inamwomba Waziri wa Fedha kufanya marekebisho katika Muswada huu na kuweka kipengele cha Sheria kinacholazimisha matumizi ya magunia ya katani kwa bidhaa muhimu ili kulinda viwanda vya magunia ya katani nchini na pia zao la katani kwa ujumla wake. Vilevile Waziri wa Fedha kwa wakati muafaka alete marekebisho ya kupandisha *suspended duty* kwa magunia ya *duty* kwa madhumuni hayo hayo ya kulinda zao la mkonge na viwanda vya magunia yanayotumia katani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha ameleta mapendekezo ili kurekebisha Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Sura ya 332. Marekebisho haya yatapunguza kiwango cha chini cha kukotoa kodi ya mapato kwa ajira kutoka 18.5% inayotozwa sasa hadi 15%. Marekebisho haya yangekuwa na maana iwapo tu kodi katika bidhaa nyingine zisingeongezwa, punguzo linalopendekezwa hapa halina maana yoyote kwa hali ya maisha ya mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani haina maoni kwa sasa kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia utoaji wa huduma za maji, Nishati na bidhaa za petroli Sura Namba 414 na pia Sheria ya hifadhi ya petroli Sura Namba 392. Mabadiliko ya Sheria yoyote hayana maana iwapo utekelezaji wake ni mdogo au haupo. Tutafurahi kuona hatua zitakazochukuliwa zitaleta ahueni kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho ya Sheria ya Kodi ya mauzo ya nje ya nchi, Sura Namba 196 kwenye Jedwali kwa kubadili mfumo wa kutoza ushuru wa kuuza ngozi ghafi kutoka kiwango cha sasa cha 20% na kuwa 40% au shilingi 400/= kwa kilo kutegemea kipi ni kikubwa.

Kambi ya Upinzani inaona ushuru huu umewekwa bila kuangalia hali halisi tuliyonayo hapa kwetu, jambo la kujiuliza ni viwanda vingapi vya ngozi vinavyofanya

kazi kwa sasa? Na je, ni nani anafaidi kwa kuweka ongezeko hilo mfugaji au yule mfanyabiashara wa kiwanda cha ngozi kilichofungwa cha Morogoro, Kilimanjaro, Shinyanga au Mwanza ambaye anataka kununua ngozi kwa bei ya chini kutoka kwa wafugaji na yeye kuuza kwa bei ya juu?

Tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni kiasi gani kitakusanywa kutokana na ongezeko hili au hii ni kwa matakwa ya wafanyabiashara wakubwa wa ngozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Grace S. Kiwelu. Sasa wachangiaji wetu nilionao hapa mezani ni wanne na ninaomba wajiandae, wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya , atatanguliwa na Mheshimiwa Said Amour Arfi, atatanguliwa na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya. Kwa hiyo, moja kwa moja sasa nimwite Mheshimiwa Ruth B. Msafiri kuanza kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe salamu za pole kwa familia ya Marehemu Mzee wetu tuliyekuwa naye hapa Bungeni Mzee Chifu Abdallah Said Fundikira ambaye ameaga dunia na pia niipe pole familia ya Mheshimiwa Spika ambaye yeye amepotelewa na Mjomba wake. Nilipozungumza na Mheshimiwa Spika wakati nilipokwenda kumpa pole alisema kwamba alimsaidia sana kusoma, kwa hiyo, kwake ameona amepoteza mlezi aliyemwezesha kufika ngazi aliyopo. Mwenyezi Mungu awafajiri na ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa alivyoiwasilisha hoja hii vizuri. Mimi nimesimama kwa lengo la kuunga mkono hoja hii lakini ninayo machache ambayo napenda nizungumze pengine katika kusaidia kurekebisha katika utendaji ama katika ufuatiliaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiunga mkono Wizara kwa mapendekezo yake ambayo imeyaleta lakini ninachopenda niseme, kwanza, ni kuipongeza kwa kurekebisha kodi kwa ajili ya wafanyakazi. Ilikuwa kubwa mno kuishusha kutoka 18% kufika 15%, ni faraja sana kwa wafanyakazi kwa sababu walikuwa na malalamiko yao ya muda mrefu na walikuwa hawajajua namna ambavyo wanaweza wakasaidiwa.

Kwa hiyo, Serikali kulifikiria hili na kulirekebisha katika bajeti ya mwaka huu ni hatua kubwa na mimi naipongeza na vilevile naungana na Serikali kuendelea kuwasihi wafanyakazi kwamba ni vizuri wakaendelea kuangalia jinsi uchumi wetu unavyokua ili kuisaidia Serikali katika kuendelea kushughulikia haki zao badala ya kukimbilia kufanya

pengine migomo kwa sababu ukiligomea taifa lako ina maana umejigomea wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niiombe Serikali isichelewe kurekebisha hii Sheria ya EWURA kusudi iweze kuipa nguvu kushughulikia ongezeko lolote la bei za mafuta pamoja na vifaa vyake basi viweze kwenda sambamba na Sheria kwa sababu hili ongezeko dogo sana la juzi la kati ya shilingi 100 na 128 limesababisha ongezeko kubwa sana la bei ya mafuta na pia limezua ongezeko kubwa sana la nauli ambazo kimsingi hazikustahili kufanyika hivyo. Utakuta bei ya mafuta kwa mfano petroli Dar es Salaam inauzwa kati ya shilingi 1,480/= kwa lita mpaka 1,500/=, ukifika Morogoro inaongezeka kidogo inakuwa shilingi 1,490/= au 1,500/=, ukifika Dodoma inaongezeka na inakuwa shilingi 1,540/=, ukifika Kagera inafika mpaka shilingi 1,700/=.

Pamoja na ongezeko hili ambalo napenda kwanza niwapongeze wafanyabiashara wa mafuta wa Mkoa wa Kagera, kwa sababu kabla ya ongezeko lililotangazwa na Serikali kuhusu dizeli na petroli zilikuwa zote ni shilingi 1,600/=. Kwa hiyo, wameongeza shilingi 100/= tu katika dizeli na petroli. Kwa hili mimi nawapongeza, ila kwa Serikali nina maombi kwamba pamoja na kuwa kwa wafanyabishara wa Kagera hawakuongeza bei kubwa kwa kuwaumiza wanunuzi wa Mafuta, lakini naomba Serikali iangalie hiyo tofauti ya mafuta kutoka Dar es Salaam kufika mpaka Bukoba. Ongezeko hili linakwenda kujitokeza katika ongezeko la nauli na bidhaa nyingine. Kwa mfano, sasa hivi nauli zote katika Mkoa wa Kagera sisi kwetu hakuna nauli ya shilingi 100/= wala 200/= na wala 300/=, nauli zote zilikuwa ni *flatted* yaani shilingi 500/= ziliongezeka kidogo zikawa shilingi 700/= kabla ya ongezeko la Serikali. Sasa hivi kila *route* imeongezewa shilingi 500/= hali ambayo imefanya waliokuwa wanalipa shilingi 500 sasa wanalipa shilingi 1,000/=, waliokuwa wanalipa shilingi 1,000/= wanalipa shilingi 1,500/= na hata sehemu nyingine hata kiwango hicho.

Kwa hali hiyo, kama ingelikuwa *SUMATRA* inapewa nguvu na yenyewe ingeliweza ikasimamia bei hizi kwa nguvu zaidi za nauli lakini kwa sababu haina uwezo huo bado na yenyewe imeshindwa kudhibiti nauli hizi. Wananchi wanalalamika lakini wafanyabishara wamenyamaza na hakuna Sheria ya nguvu ya kuweza kuwadhibiti. Suala hili naomba lisicheleweshwe, lifanyike haraka ili kuweza kuona kwamba ongezeko la kodi ya namna yoyote ile lisije likapelekea katika kuumiza wale ambao ni watumiaji na ni wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba sikubaliani moja kwa moja na maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu lile ongezeko la bei walizozitaja Bukoba na Muleba. Bei ya sementi katika Mkoa wa Kagera haikupandishwa na ongezeko la shilingi 100/= za juzi. Bei ya sementi katika Mkoa wa Kagera kabla ya tarehe 01/07 mfuko wa sementi inayotoka Kampala maana yake Uganda tulikuwa tunainunua shilingi 15,000/= na Twiga *Cement* pamoja Tanga *Cement* tulikuwa tunainunua kwa shilingi 18,000/=. Kwa hali hiyo, sasa hivi imeongezeka kwa shilingi 500/= tu yaani ni shilingi 18,500/= na 15,500/=. Sasa bei hii iliyosomwa hapa ya shilingi 19,500/= kwamba imeongezeka kutoka shilingi 14,000/= kwenda 18,000/= kwa sababu ya ongezeko hili si kweli. Mimi nilipokwenda Bukoba nikafanya mkutano wa hadhara tarehe 8/07, niliwafahamisha

wananchi kwamba ongezeko hili halijaenda kwenye bidhaa, wanaoongeza ni kwa mapenzi yao wenyewe na kama ingekuwa imeongezeka basi ni kidogo sana kama hivi ambavyo imekuja imetoka shilingi 18,000/= na imekuwa shilingi 18,500.00, kwenye sementi hakikuongezeka kiasi kilichotajwa hapo.

Vilevile bei ya sukari Muleba tulikuwa tunainunua shilingi 1,200.00 na sasa hivi tunainunua shilingi 1,300/=. Kama Mwenyekiti angekuwa amenipa taarifa mapema wakati msomaji ameanza kusoma nikahisi nitakuwa wa kwanza, ningeweza nikakupa *exactly* bei ya leo asubuhi ni shilingi ngapi. Lakini kwa sababu sikupewa muda basi naisema bei ninayoifahamu ambayo nimetoka Bukoba baada ya ongezeko la bei ya mafuta ilikuwa imeongezeka shilingi 100/= tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mche wa sabuni haujafikia shilingi 900/= ambayo msomaji ameutaja. Ni vizuri kabisa kuwa na hakika ya bei hizi na hasa ukizingatia kwamba Bungeni tupo Wawakilishi wa watu. Hawa na sisi tunafuatilia sana kwa sababu bei zinapoongezeka sana haya hayaonwi na wapinzani tu hata Chama Cha Mapinduzi kinaona. Watanzania hawa si Watanzania ambao hali halisi hawaioni, ukisema kitu kwa ku–*exaggerate* na kuongeza chumvi zaidi na wao wanasikia na wanafahamu kwa sababu bidhaa hizi ni za matumizi ya kila siku.

Wananchi wanajenga kila siku, ambaye hajengi nyumba yake basi amechangia ujenzi wa shule ya sekondari, anafahamu bei ya mfuko wa sementi, mtoto wake anasoma anafahamu vilevile bei ya sabuni na sukari kwa ajili ya huduma za familia yake. Kwa hiyo, napenda hili niliweke vizuri ili kwenye reckodi isionekane na wala Wizara isisumbuke kutafuta bei. Bei hizi ndivyo zilivyo. Mimi nimezaliwa Muleba na ninaishi Muleba, kwa hiyo ,nafahamu hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, mimi sikuwa nalo la ziada, napenda kusema kwamba ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI – MHE. JOB Y. NDUGAI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, sasa kama nilivyosema mwanzo, anafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya na Mheshimiwa Said Amour Arfi ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mawazo yangu hasa kuhusiana na haya marekebisho ambayo yameletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuonyesha kasi mpya kwa vitendo kwa sababu wananchi wamekuwa wakilalamikia juu ya upandaji ovyo wa bei za mafuta na maneno ambayo yamekuwa yakiendelea lakini baada ya kugundua kwamba EWURA hawana meno ya kuweza kushughulikia suala hilo mara moja sheria imeletwa na tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nichukue nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Spika kwa kuondokewa na mjomba wake mpendwa Mzee wetu, Chifu Abdallah Said Fundikira, Mwenyezi Mungu amuweke Mahali pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu aliyepita ameshazungumza. Kwa kweli mimi pia nashikwa sana na kigugumizi na inanisononesha. Sisi tunapoamua kutokuwa wakweli na kutokufanya utafiti wa kina ambao unalenga katika kuboresha maisha ya Watanzania, mimi nimeshtushwa sana na data zilizotolewa na Mheshimiwa Mbunge mwenzetu hasa kuhusu Mkoa wa Ruvuma. Nikafikiria kwamba je, hiyo *research* ilifanyika Mkoa mzima halafu ikatafutwa *average* au ali – *pick* duka moja kwa mtu anayemfahamu au ilikuwaje? Kwa kweli ni data ambazo zinapotosha. Mimi nadhani utaratibu si mzuri kufanya *research* ambayo haijathibitika halafu ukaja tu ukaiweka mahali kama hapa. (*Makofi*)

Nadhani lengo la vyama vyote vya Siasa na sisi wote Wawakilishi ni kuhakikisha kwamba tunafanya utetezi wa kina wenye lengo la kuwaendeleza Watanzania, kwa hiyo, tusiwatishe. Lakini pia kuwanyima imani na Serikali yao, nadhani siyo utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite zaidi katika Sheria hii kuhusiana na *EWURA*. Naomba niutahadharishe umma wa Tanzania kwamba tunapozungumzia maendeleo kwa vyovyote vile ni lazima tuweke *inputs* yaani tuweke vitu ambavyo vitaweza kutoa maendeleo. Kwa hiyo, kama ilivyoelezwa kwenye bajeti mwanzo na leo inarudiwa tena, *EWURA* peke yake kama ilivyo sidhani kama ni jibu la kudumu au jibu la moja kwa moja la kusema kwamba sasa ikishakuwepo *EWURA* basi yenyewe itaanza kushusha bei za mafuta, itakuwa inasema badala ya kuwa shilingi 1,500/= basi itakuwa 1,300/=, nadhani bado itatuletea tatizo. Isipokuwa *EWURA* tunaitegemea itafanya *monitoring* ya kina kuweza kujua bei halisi ambayo mafuta yamenunuliwa kwa mfano kutoka nje ni kiasi gani na Gharama za kusafirisha ni kiasi gani, itapata *range* ambayo inakaribiana na ukweli badala ya kuona kwamba kunakuwa na upandishwaji wa hizo bei kiholela.

Nasema hivyo kwa sababu gani? Kwa sababu katika mafuta tuna wawekezaji binafsi ambao wanakwenda kununua hizo bidhaa na zinapofika hapa kuna gharama nyingine ambazo wanazipata kupitia maeneo mbalimbali, ndiyo maana naona kuwa *EWURA* siyo jibu peke yake. Kwa mfano, ukichukulia meli yenyewe inayobeba baada ya kufika pale Bandarini unaweza ukakuta walioweka mafuta kwenye ile meli labda pengine ni makampuni mawili au matatu. Wakati wa kutoa unakuta mmoja yuko tayari ameshakuwa na pesa za kulipia na mwingine hajawa tayari. Kwa hiyo, meli inakaa bandarini, ikishachajiwa pale zile *demurage charges* ina maana zote zile atazibeba mlaji. Sasa hapo inategemea je, zile gharama au hasara zimetokana na wao wenyewe wajasiriamali wale ambao wameshasafirisha mzigo au imetokana na Mamlaka zetu sisi kama Watanzania?

Kwa mfano, tuna Mamlaka ya Bandari na wale ambao wanasimamia mizigo kwa ujumla unaweza kukuta labda mita siku hiyo hazifanyi kazi au baadhi yake ni mbovu, mzigo ukakaa bandarini muda mrefu, *demurage charges* zikapanda, je, gharama hizo

zitakuwa wapi? Ndiyo maana naona kwamba suala hili inabidi liangaliwe kwa kina ama sivyo linaweza likatuyumbisha kutokana na kelele zinazotoka maeneo mbalimbali bila kuangalia kwa kina. Kwa sababu hata huyu mfanyabishara ambaye tumemuweka kwa ajili ya kusaidia badala ya Serikali peke yake kuingiza mafuta tukaona kwamba basi hawa wenzetu watusaidie kuleta mafuta. Tukiwabana na tukawapangia bei labda shilingi 1,200/= wakati hiyo bei haifanani na gharama zake za kuingiza mafuta bado itakuwa ni tatizo tutakuta kwamba sisi kisiasa tumewini na tumewawezesha wananchi kujisikia kwamba mafuta kwa bei nafuu lakini kwa upande mwingine tutakuwa tumewafanya wale *investors* wakawa wanaona sasa ni hasara wakaamua ku – *withdraw activities* zao. Kwa hiyo, mimi naona hili ni suala la msingi sana, tuangalie katika maeneo yote ni jinsi gani tunafanya hivyo.

Lakini vilevile kuhusiana na maeneo mengine, nimejaribu kupitia papers kwenye internet kuweza kuona labda nchi nyingine wenzetu wanafanyaje. Kwa mfano India, wao wamejaribu kuona labda kuweka ruzuku katika maeneo mbalimbali lakini unakuta bado zile ruzuku kwa upande mmoja hazionyeshi moja kwa moja kwamba zimesaidia.

Lakini vilevile unakuta kwamba hata kwenye zile ruzuku, kwa mfano, tuchukulie sisi sasa hivi tumesema kwamba mafuta ya taa tuyapunguzie bei kabisa, lakini wakati huohuo je, yale mafuta ya taa tuliyoyapunguzia hizo bei ni kweli yanafuata watu ambao hawana uwezo kabisa? Ni kweli watu wote wanaotumia mafuta ya taa ni wale ambao hawana uwezo? Ni makundi yapi yanafaidika? Kwa hiyo, mimi nafikiria hata tunapoamua kufanya *subsides* zetu tuangalie ni makundi gani tunayagusa.

Mfano huo wa India pia nimeona kwamba wao katika zile *states* zao kuna bei tofauti tofauti. Kwa mfano, kama sisi tulivyotajwa hapo Ruvuma ni kweli Ruvuma kwenye mafuta mwezi wa tano mwaka jana mimi kwenye kile kijiji changu nilinunua lita shilingi 1,800/= lakini labla ya kupandisha hizi bei. Sasa hali hiyo inatokana na zile *distance* kutoka huku Dar es Salaam tunakopatia mafuta mpaka kule kwenye maeneo yetu. Sasa kwa hali hiyo labda Serikali inaweza ikaangalia katika zile *remote areas* je, wanaweka *subside* ya aina gani? Japo hapo hapo kuna hatari pia ya watu kunufaika kutokana na hayo maeneo. Kwa hiyo, tunafikira kwamba *EWURA* sasa kazi yake itakuwa hasa katika kutathmini maeneo kama hayo na si kwamba yenyewe kazi yake itakuwa ni ku – *dictate terms,* leo bei ni hii na kesho bei ni hii ama sivyo kwa kweli mimi nadhani tutakuwa tumebadilisha dhana halisi ya *EWURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naona kwamba baada ya kuzungumzia hayo, nizidi tu kusisitiza kwamba vyombo vyote *EWURA* yenyewe pamoja na hii Sheria itakayokuwa imepitishwa, *TRA, THA, TPA* na Mamlaka zinazohusika pamoja na hawa wajasiriamali binafsi na wananchi wenyewe wote kwa pamoja tuwe macho katika hili. Maana yake mpaka sasa hivi tunalalamika lakini mimi sijaona hata mmoja ambaye ameshafungwa, hata ile tu kuchukuliwa hatua angalau akahojiwa aweze kueleza binafsi ametumia kigezo gani kupandisha bei bado hatujawashika watu kama hao. Kwa hiyo, mimi nadhani kila mtu ana jukumu la utekelezaji wa hizi sheria zetu.

Kwa hiyo, katika misingi hiyo naona sihitaji kuchangia sana lakini msisitizo wangu ni kwamba isichukuliwe *EWURA* peke yake kama ndicho chombo pekee kinachoweza kuleta jibu la bei hii ya mafuta bali pamoja na vyombo vyote vinavyohusiana na uagizaji pamoja na usambazaji pamoja utumiaji na pamoja na kuona kwamba ni makundi yapi yanaguswa kihalali.

Jambo lingine la msingi ambalo labda lingenipita ni kwamba tunaposisitiza tu kushusha bei ya mafuta kwa sababu ni kubwa, tunasahau kwamba tunaweka hali ya kuwafanya wananchi wetu au watumiaji wa mafuta kwa ujumla kushindwa kufikiria umuhimu wa kutumia rasilimali mbadala au *energy* mbadala. Wanasema kwamba mafuta mafuta tu na *consumption* ya mafuta inazidi kuwa kubwa *unnecessarily* kumbe pengine angeweza kutumia rasilimali nyingine katika kupunguza hali iliyopo. Kwa hiyo, tusiwe na jibu moja kila wakati tuwe na majibu ya kutosha na tuwe na fikra za kina kwa sababu kwa kina suala hili ni mtambuka na linagusa maisha yetu na vilevile si Tanzania tu ambayo imeweza kuweka kodi kwenye mafuta katika kuongeza pato la taifa, hapana! Nimeshafuatilia na nimesoma pia nimeona kwamba ni nchi nyingi ambazo pale inapohitaji ku – *bust revenue* ya nchi pia katika kuongeza bei ya mafuta imekuwa ni sehemu mojawapo ya haraka. Wenzangu kama watafikiria kwamba labda hayo nimeyatoa kichwani mwangu tunaweza tukakutana na nitawapa hizo *papers* ili tuzipitie wote na tuweze kusaidiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya na sasa nitamwita Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Manju Salum Omar Msambya ajiandae.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie huu Muswada wa Fedha.

Awali ya yote napenda kuungana na wenzangu ambao wametoa pole kwa Mheshimiwa Spika kwa msiba aliokuwa ameupata. Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi Mzee wetu Chifu Abdallah Said Fundikira. Hiyo ndiyo njia yetu, yeye ametangulia na sisi tupo nyuma, *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikupenda sana kujiingiza sana katika hili lakini nimeona kwamba sasa ndiyo umekuwa utamaduni wetu kwamba tunatoka katika hoja na tunaanza kujibu hoja za Wabunge wenzetu. Haipendezi sana na hata kama kuna ulazima wa kufanya hivyo basi tusionekane kwamba tumekosea sana. *(Makofi)*

Taarifa ambayo msemaji wa Kambi ya Upinzani ameiwasilisha mbele ya Bunge hili tumeipitia na tumeifanyia utafiti. Ukiisoma taarifa yetu tumeelezea kwamba sehemu nyingi katika nchi yetu sasa hivi mafuta ya taa yanauzwa kati ya shilingi 1,700/= . Lakini sasa hivi msemaji wa mwisho anasema katika kijiji chao kabla hata bei hii haijatangazwa ilikuwa ni shilingi 1,800/= lakini hatuwezi kuwadanganya Watanzania. Watanzania wanafahamu na wanajua kama bei zimepanda wao wanafahamu na kama hazikupanda

wao pia wanafahamu na wanafahamu pia ni kwa sababu gani bei zimepanda, hili halihitaji mjadala, wananchi wenyewe watafanya maamuzi na watajua juu ya hilo na ni kwa sababu gani bei zimepanda wananchi wanafahamu.Tulisema toka awali kuhusu bei ya mafuta pamoja na marekebisho mazuri ambayo Waziri aliyafanya kwa kuondoa ile kodi kwenye mafuta ya taa na kuipeleka kwenye dizeli na petroli lakini hatujamsaidia mtumiaji wa mafuta ya taa, yaani hatujampunguzia bei. Ili mafuta ya taa yaweze kufika Mpanda ni lazima yasafirishwe kwa magari yanayotumia dizeli, kwa hiyo gharama za usafiri zinaongezeka na bei ya mafuta bila shaka lazima itapanda na imepanda na wananchi wanajua hilo.

Lakini kama zingekuwepo njia nyingine za kuweza kupata mapato ya Serikali na bila kuingiza katika mafuta kelele hizi leo zisingekuwepo. Kuongezeka kwa bei za mafuta kumesababisha vitu vingi viweze kupanda bei, lakini tumejikita sana katika usafiri kwa maana ya nauli na bei za mafuta tu na ndiyo maana katika Muswada huu pia kuna mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Sheria inayotoa Mamlaka kwa *EWURA* kuwa na Mamlaka zaidi juu ya udhibiti wa bei.Maamuzi haya tumeyachukua kwa sababu tu kumekuwa na kelele ya ongezeko la bei za nauli na bei ya mafuta. Lakini haikuishia katika nauli tu na mafuta lakini gharama nyingi zimeongezeka. Kwa mfano, bei ya mchele imepanda, bei ya sukari imepanda, bei ya nyama imeongezeka kwa maana hiyo bei ya mlaji imepanda sokoni. Sasa mlaji huyu tunamsaidia namna gani? Kuna mamlaka gani kisheria inasimamia na kudhibiti bei za walaji, lakini tumejikita tu katika kutazama bei za mafuta na nauli za mabasi lakini athari ya ongezeko la bei ya mafuta limeathiri mpaka kwa mlaji wa kawaida wa bidhaa za sokoni. *(Makofi)*

Sasa sijui Waziri anasemaje kuhusu hizi bei za walaji. Tunatengeneza mamlaka nyingine ya kusimamia bei kwa sababu tulikuwa na *Price Commission* kwa sababu nisizozijua *Price Commission* ikaondolewa ama kwa shinikizo au kwa kuonekana kwamba haina umuhimu, lakini leo bei zimekuwa ni holela. Lakini kwa ridhaa yetu wenyewe tumefanya kwamba liwe soko huru, sasa nadhani tuliache tu soko lijiendeshe. Ili Serikali iweze kudhibiti bei au kurudisha *Price Commission* iweze kusimamia bei au ipunguze kodi ili itoe nafuu kwa mlaji, ni njia mbili tu ambazo nafikiri zinaweza zikatusaidia. Lakini umuhimu wa kudhibiti bei bado tunakubaliana kwamba ni lazima uwepo, bei zisiende tu zikapanda zikaleta athari kubwa kwa wananchi na kuleta malalamiko ni lazima tulisimamie hilo. Serikali ni lazima ijiangalie kwamba sasa tunarudi kule tulikokuwa kwamba umuhimu wa *Price Commission* upo; je, tutarudisha Tume ya Kusimamia Bei au tutasimamia bei tu katika *SUMATRA*, *EWURA* na huko kingine tunaacha. Nadhani hilo nilikuwa naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kuongezeka kwa bei ya mafuta na makusanyo yatakayotokana na ongezeko hilo ambalo Mheshimiwa Waziri amependekeza tunadhani kabisa kwamba pengo hilo linaweza likafidiwa na ongezeko ambalo limefanywa sasa na Waziri wa Maliasili na Utalii kwenye magogo. Kwa hiyo, ingekuwa busara zaidi kwamba ongezeko hilo lingeondolewa. Kwa sababu yapo maeneo ambayo Serikali ikijikita inaweza kukusanya pesa zinazotokana na ongezeko la mafuta ili kuweza kuondoa mtafaruku huu ambao umejitokeza hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya *Finance Bill*, awali ya yote naiunga mkono. Pamoja na kuunga mkono kabla sijaendelea na mimi nitoe salamu za rambirambi kwa kifo kilichotokea cha mzee wetu, Chifu Abdallah Said Fundikira, naomba salamu za kwanza ziwafikie wafiwa pamoja na mpwa wake, Mheshimiwa Samwel Sitta, naomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo naipongeza Serikali kwa kuleta marekebisho ya Sheria yatakayoipa *EWURA* meno ya kusimamia bei za bidhaa za mafuta. Lakini ningependa nishauri Serikali kwamba meno haya yangeletwa mapema, kwa sababu Serikali ilikuwa inafahamu kwamba itafanyika bei ya mafuta kwa kiasi ambacho ilipandisha, lakini Serikali vilevile kwa uzoefu wa huko nyuma ilikuwa inatakiwa itambue riba za wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta. Ukiongeza senti kumi wenyewe wanakwenda shilingi 10/=. Sasa wangefahamu hili ingekuwa ni vizuri kwao kuweka tahadhari kabla ili *EWURA* wawe wamepewa nguvu kwa sababu kwa kipindi hiki ambacho leo tunazungumzia marekebisho ya sheria na pale bei ilipotangazwa wafanyabiashara wamekwishawaumiza watumiaji wa bidhaa hizi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linaloendana na marekebisho ya sheria inayotoa nguvu ya biashara hii ya bidhaa za mafuta, ni kwamba imetolewa adhabu kwa watu wanaoleta udanganyifu katika biashara hii Moja ya adhabu ni kwa wale watakaochanganya bidhaa hizi, kwa mfano wale wanaochanganya petroli na mafuta ya taa au dizeli na mafuta ya taa au petroli na dizeli. Na hapa naomba nitangaze maslahi binafsi kwenye hili. Tarehe 3 Julai nilikuwa nasafiri kwenda Dar es Salaam kwa kutumia gari yangu. Nilijaza mafuta kwenye vituo viwili tofauti hapa Dodoma lakini nilipofika Gairo gari likafa na kwa kuirudisha barabarani imenigharimu shilingi 4,800,000/=. Lakini wenye kufanya biashara hii kwa udanganyifu tunaambiwa anatozwa faini ya shilingi 1,000,000, huyu mtu anayepata faida ya zaidi ya shilingi 100,000,000 na anatoa hasara ya zaidi kwenye mitambo ya watu wengi tu. Hoja inayotolewa na Serikali ni kwamba tukitoa adhabu kubwa tutawafukuza wawekezaji. Hivi tunahitaji wawekezaji wa aina hii? Mimi sidhani kama tunahitaji wawekezaji wa aina hii. Ni bora tutoe adhabu kali wale wawekezaji wenye udanganyifu waondoke tubaki na wawekezaji wachache wenye kuweza kuwahudumia Watanzania katika hali nzuri. Nafikiri Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla watazame namna ya kuweza kuwaadhibu watu ambao hawana nia njema na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda haraka na sina mengi ya kueleza. La mwisho, ninalotaka kuzungumzia ni kwamba nilipochangia kwenye Wizara ya Miundombinu kwa maandishi na nikaeleza kilio cha watu wanaofanya shughuli za vyombo vya usafirishaji kwenye maziwa yetu na hususan Ziwa Tanganyika, Kigoma kule ambako mimi natoka. *SUMATRA* walisimamisha vyombo vya usafiri Ziwa Tanganyika na usafiri tunaotumia sana sisi ni maboti. Walisimamisha watu kwa sababu vyombo vile vilikuwa havina vifaa vya uokoaji, lakini Serikali huko nyuma ilifanya marekebisho ya sheria na katika kurekebisha wakaathiri kodi kwenye vifaa vya uokoaji. Kwa maana hiyo

walipofanya marekebisho walikaa kimya katika kodi ya vifaa vya uokoaji hivyo *TRA* basi kwa sababu waliona Serikali imekaa kimya wakatoza kodi kwenye vifaa vya uokoaji jambo ambalo kwa dunia nzima vifaa vya uokoaji na hasa uokoaji wa majini huwa havina kodi. Sasa kwa kukaa kimya vifaa ambavyo vingetakiwa vigharimu shilingi 15,000.00 vinagharimu shilingi 85,000.00, na mimi nimeongeza na watu wa Chuo cha Usafirishaji (*Maritime Institute)* Dar es Salaam wanasema hata wao huingiza bidhaa hizi kutokana na kodi inayotozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali iangalie kodi kwenye vifaa hivi ni lazima kwenye vyombo hivi vya usafiri viwe na vifaa hivi lakini kuwepo na vifaa ambavyo watumiaji wenye vyombo wanaweza wakamudu kununua. Kwenye soko sasa hivi kuna mfanyabiashara mmoja wa Mwanza ameingiza vifaa hafifu, maboya ya uokoaji hayatakiwi yakanyonya maji. Sasa ameingiza vifaa hafifu ambavyo nimeonyeshwa kwenye Chuo cha *Maritime* vikinyonya maji hata huyo aliyevaa lile boya aondoke nalo atazama nalo. Sasa ingekuwa ni vizuri tuangalie kwa undani kodi kwenye vifaa hivyo vya uokoaji ili tusiweze kuwaumiza waokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kumekuwa kuna malalamiko katika ukumbi wetu huu kwamba Mheshimiwa Mbunge akisimama akihoji na kurekebisha kauli inayotolewa na upande wa pili anaambiwa amechukua nafasi ya Serikali, si kweli!

Kama Mheshimiwa Mbunge anazo *facts* za kurekebisha kauli iliyotangulia ambayo siyo sahihi hata kama ni ya Mbunge wa Kambi yake mwenyewe hivi ukumbi huu kazi yetu ni sisi mtu asimame hapa atoe kauli ya kupotosha. Mimi nadhani kauli walizotoa Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya ni kauli ambazo zenye ukweli katika maeneo wanayotoka. Sasa zisitolewa kauli za kule wanakotoka wao za kupotosha na wenyewe wakae kimya na huku wakiwa wanafahamu ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo narudia kusema kwamba naunga hoja mkono. Ahsante sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea vitu vichache sana. Kwanza na mimi nianze kwa kutoa pole kwa Spika na kwa familia ya Chifu Abdallah Saidi Fundikira. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani itapata heshima kama inaweza ikajitegemea. Mataifa haya makubwa ambayo yameendelea, yameendelea kwa sababu wanaweza wakafanya shughuli zao za maendeleo kwa pesa zao wenyewe. Nchi yetu ina matatizo mengi sana, tunazo changamoto kubwa mbele yetu. Mimi ni imani yangu hatuna mjomba, hatuna baba wa kutegemea ila ni sisi wenyewe.

Mwalimu alituambia "Kupanga ni Kuchagua." Kwa hiyo, lazima tukubaliane njia mojawapo ya kupata fedha za kuendesha nchi, ili kuleta maendeleo ni kwa wananchi

wenyewe kujifunga mikanda na moja ya njia ni kutoa kodi. Mimi sijui ni nchi gani imeendelea bila watu wake kulipa kodi, mimi siifahamu. Ndugu zangu najua yako maneno mengi sana yatasemwa. Tunasoma kwenye magazeti lakini nadhani kuna vitu vingine lazima tukubaliane watu wanaongea upande mmoja wa gharama, kupanda hakuna anayeongea faida tunazopata kwa kuweza kujenga miradi yetu wenyewe.

Niambieni hivi leo tungeamua tusipandishe bei ya mafuta tusitoze kodi tusingejea barabara, tusingejenga shule, hospitali na tusingefanya chochote cha maendeleo, tungekuwa wapi. Tunavyosema hivi hatuchukui nafasi ya Serikali tunaangalia ukweli, nadhani maana ya Ubunge ni kusema ukweli na kama liko jambo zuri linafanyika tuliseme. Asubuhi ya leo tumeambiwa barabara vijijini, bajeti ya mwaka jana ilikuwa shilingi bilioni 25, mwaka huu wamekwenda mpaka shilingi bilioni 65. Hizi pesa zingepatikana wapi, hiki kilimo kitapandaje, biashara itakuwaje ya ndani? Ndugu zangu lazima tukubaliane hapo ni kweli mambo mengine yana machungu lakini tuangalie faida zake zaidi. Mwaka jana Serikali Kuu upande wa *TANROADS* bajeti ya barabara ilikuwa ni shilingi bilioni 56, mwaka huu imepanda kuwa shilingi bilioni 135, tunataka nini sasa Wabunge! Maana yake sasa tuchague.

Lakini naamini kupanda kwa bei huku ni kwa muda, tukishafanya haya mambo ya maendeleo kutakuja *competition, competition* inarudisha *price* chini. Hakuna dunia inayoweka *price stabilition any more* kwenye *economy,* hakuna ni *competition* tu. Kweli leo Kigoma kuna vitu, ni bei ghali lakini tukimaliza kujenga barabara hizi tukatoka hapa Tabora tukafika Kigoma kwa barabara ya lami, tukatoka Kigoma tukaenda Mpanda mpaka Mbeya kwa barabara ya lami, tukaenda mpaka Bukoba kwa barabara ya lami, maana yake watu wengi wata-*access* hiyo *market* ya Kigoma. Kwa hiyo, *the more* wakija wengi ndio watashindana, *price* zitashuka, hizi ndizo *principles* za *economy. (Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa wenzangu tuongelee pia na faida zitokanazo na haya mambo. Tumefanya mageuzi makubwa sana kwenye elimu lakini hizo hela tungezitoa wapi. Lazima tukubaliane na wananchi wetu. Mwalimu alitwambia “Kupanga ni Kuchagua”. Kama tunataka maendeleo, na mimi ni mmoja wa watu ambao naamini kabisa kabisa kama kuna kitu kinaleta heshima ni kujitegemea kwenye bajeti yetu wenyewe. Lakini ukiniambia usitoze kodi lakini *at the same time* kila siku wewe unapiga hodi kwa *donors,* inavunja heshima ya nchi. *Argument* kwa hili namwomba Waziri wa Fedha atusaidie, ni kufikiri zaidi kuongeza wigo wa kodi. Hii ndiyo *principle,* basi kwamba tusiendelee na *traditional way* ya kutoza kodi kwenye vitu vile vile sasa tuanze kujitanua tupanue wigo wetu na kwa kufanya hivyo tutapata fedha nyingi zaidi na nchi yetu itafanya maendeleo makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kati ya watu ambao naamini kwamba mambo haya yanayotokana na upandishaji huu wa kodi hizi za mafuta, ni wa muda lakini nchi yetu inahitaji sana maendeleo. Tunahitaji umeme vijijini, kila siku tunaomba, tunahitaji miradi ya maji. Yote haya hatuna mjomba eti! Kwa hiyo, nataka kuipongeza Serikali kwa kweli kwa kuamua, ni maamuzi mazito lakini yalihitaji kuchukuliwa. Ukipanda gari ukatembea kilomita 100 ya barabara ambayo haina lami na barabara yenye lami, mafuta

mtakayotumia ni tofauti, *vehicles operation costs* zitakuwa ni tofauti. Kwa hiyo, unaweza ukasema nisitoze kodi lakini mtu huyu akawa anatembea kwenye barabara mbaya mwisho wa siku akalipa kwenye vitu vingine, hiyo hiyo hela ambayo angelipa kwenye kodi ukatengeneza barabara, ni suala la kuchagua tu.

Sehemu ambayo ungekwenda kwa saa tatu, utakwenda kwa saa moja na *two hours* ambayo umei-*save it is also money.* Hakuna anayeongelea hili, anaye-*cost* huu muda. Kwa hiyo, ndugu zangu lazima tukubaliane na nchi zilizoendelea, ni kwa sababu hiyo watu wanalipa kodi. Wazungu wanatusaidia ni kwa sababu wanalipa kodi. *Infact* tuendeleze kampeni kubwa ili watu wasikwepe kodi. Agenda namba moja, Waziri wa Fedha atusaidie, aweke mkakati wa kuwafanya watu wengi zaidi ile *compliance* ya kulipa kodi iwe kubwa ndiyo nchi yetu itatoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nasema lazima tuliangalie katika mambo ya kodi ni kwamba kuna kitu kinaitwa *revenue ratio* v/s *GDP*. Ili nchi iweze kujitegemea lazima *revenue ratio* iwe 18% to the *GDP* mpaka 30 na kuendelea. Nashukuru Mungu wakati Waziri wa Fedha anatoa ile bajeti kubwa alisema anaamini mwaka huu tunakokwenda tunaelekea kwenye kufika hiyo asilimia 18. *South Africa* leo *revenue ratio v/s GDP* ni 30% ya *GDP.* Maana yake nini kwenye *economy*? Maana yake ni kwamba wanaweza waka-*finance* bajeti yao wenyewe. Kwa hiyo, na sisi lazima tuwe na mkakati kwamba katika miaka miwili mitatu inayokuja tufike sehemu tutoke kwenye asilimia 42 ya kutegemea *donors* twende ikiwezakana mpaka asilimia 10, hatuwezi kufika kama *revenue ratio v/s GDP* haijapanda, hatuwezi. Kenya wenzetu wamekwenda, wako mbali, sasa hivi *revenue ratio v/s GDP* yao ni *more than 18%.* Kwa hiyo, sasa wanaweza waka-*finance* vitu vyao vyenyewe. Haya ndiyo maendeleo hayapatikani kwa lelemama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia lingine ambalo nililisema na wenzangu wengi wamekuwa wakilisema ni hili suala la matumizi ya *long term bonds* kwa ajili ya maendeleo yetu. Nimwombe Waziri wa Fedha hili jambo alipe umakini zaidi. Ukienda *Wester Europe* yote wameendelea kwa sababu wamekuwa wana-*issue bonds* kwa ajili ya *specific project*. Ziko *bonds* za namna nyingi, mimi nasema tunaweza tukaamua leo kwamba sasa tunaanza ku-*issue long term bonds* za miaka 5, 10 mpaka zaidi. Na *area* ipo, tuna *pension funds* zetu kama *insurance*. Watu wa *Pension Funds* na hizi *insurance* wao wana *long term liability* kwa sababu wana *long term liability,* ni vizuri wa-*invest* kwenye *long term investment* ambazo ziko *targeted* kwenye maendeleo. Tukianza kutumia *bonds* kwa ajili ya ku-*finance projects* zetu baada ya miaka mitano tutai-*turn round* nchi hii na tutaanza kwenda kwenye kasi ya ajabu sana na haya ni mapinduzi. Naomba Waziri wa Fedha alisimamie, hatuna *choice,* lazima tuanze kutumia *bonds* kwa ajili ya maendeleo yetu. Kwa mtazamo wangu *bonds* ndio mkombozi wa peke yake, una hakika leo unakwenda una-*issue bonds* unapata shilingi bilioni mia moja pale, bilioni mia moja hizi sipeleki popote nakwenda kujenga barabara ya kilomita 100. *You get the road* na unaanza kulipa na ikifika wakati wa *maturity* wa kulipa una-*issue bond* nyingine, unamlipa huyu na nusu unafanya hiki mnakwenda mbele. Haya inawezekana watendaji wetu wakae, yako kwenye vitabu vya *economics* duniani kote wanafanya kwa nini sisi tusifanye?

Lingine Waziri wa Fedha wakati anatoa hotuba yake alisema Serikali haitokopa tena, mimi nasema nampongeza sana. Kwa sababu Serikali kwa kutokopa maana yake kwa ku-*reduce treasury bills* maana yake ni kwamba mabenki sasa yatakwenda kwa watu kuwakopesha, hayatonunua tena *Treasury bills.* Lakini hili tulifanye kwa umakini sana, bado naamini katika *economy role* ya *treasury bills* ipo. Kwa maana *treasury bills* ndiyo ina-*set the interest rate.* Lakini *at the same time* ndiyo inafanya *liquidity* ya *management,* ikitokea kuna hela nyingi kwenye *economic* wana *mop up*, una *mop up through treasury bill.* Kwa hiyo, kinachoweza kufanyika hapa ni kupunguza *frequency* ya ku-*issue treasury bills* na *amounts*. Tukiya-*manage* haya vizuri tuta-*stabilise our economy, economy* yetu itakua na nchi yetu itaendelea, itakwenda mbele. Mimi naomba wakati Waziri wa Fedha anajibu aniambie sasa tuna mpango gani kuanza kutumia hizi *long term bonds* kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja.

## MCHANGO WA MAANDISHI

**MHE. MANJU S. MSAMBYA**. Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kutamka kuwa naunga mkono hoja. Hata hivyo napenda nitoe maoni yafuatayo, kwanza, naipongeza Serikali kwa kuleta marekebisho ya sheria ambayo itawapa *EWURA* nguvu za kusimamia bidhaa za petroli, hata hivyo napenda niweke bayana kuwa lingekuwa jambo la busara kabla Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2007/2008 haijapandisha bei ya mafuta ingekuwa imetambua ghiriba za wenye vyombo vya usafiri wa wafanyabiashara za mafuta. Kwa hali hiyo Serikali kwa uzoefu wa huko nyuma ingetakiwa itambue kuwa ongezeko la bei ya mafuta kwa kiwango chochote kile linasababisha bughudha kwa walaji.

Pia napenda niitahadharishe Serikali kuwa adhabu iliyowekwa kwa wale wanaofanya udanganyifu katika biashara haitoshi, napenda ieleweke kuwa pale mfanyabiashara anapofanya udanganyifu wa kuchanganya aina tofauti za mafuta kama vile mafuta ya taa na dizeli anafanya uhujumu wa kiuchumi. Athari za kuchanganya mafuta ni uharibifu katika mitambo. Adhabu ya shilingi 1,000,000/= kwa mtu anayetengeneza faida ya shilingi 200,000,000/= au zaidi haitoshi. Pia hoja inayotolewa kuwa kuwaadhibu kwa adhabu kubwa itakuwa kufukuza wawekezaji, hivi kweli tunahitaji wawekezaji wa aina hii? Mwekezaji wa aina hii anatakiwa asiwepo na tubaki na wachache waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sikuona marekebisho ya kodi katika bidhaa za uokoaji, ikumbukwe kuwa huko nyuma yalipofanyika marekebisho ya *Finance Bill,* sheria ilikaa kimya katika bidhaa za uokoaji. Hivyo *TRA* wakatoza kodi kwenye vifaa hivyo. Bidhaa ambayo zingeweza kuuzwa kwa shilingi 15,000/= zimeweza kuuzwa kwa shilingi 85,000/=. hali hii imeweza kufanya wafanyabiashara wasio waaminifu kuingiza bidhaa hafifu katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Waziri atoe kauli ya namna gani atasimamia vifaa vya uokoaji.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kujibu baadhi ya hoja walizochangia kwa ajili ya Muswada huu wa Fedha wa mwaka 2007.

Kama kawaida ningependa kuwataja wale watu waliochangia kwa kuzungumza na pia wale waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Omari Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, ambaye alisimama kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Manju Msambya na Mheshimiwa Peter Serukamba. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Napenda kuchukua nafasi hii kwa kweli kuwashukuru wote kwa michango yao ambayo imejenga zaidi *bill* yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na swali lile la kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha ulitakiwa upitishwe kabla ya ule wa matumizi. Ningependa kusema kwamba suala hili kwa kweli lilikuwa limepangwa kwa Ofisi ya Bunge kwa ratiba na naona Ofisi ya Bunge waliona kwamba hili jambo ni sahihi, kwa hiyo, utaratibu ndivyo ambavyo uliotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zinazotumiwa Zanzibar kwamba uingizwe kwanza kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kipindi hiki kwamba umewekwa kwenye sheria kwamba fedha ambazo nimetoa mfano bia au sigara ambayo inazalishwa Tanzania Bara lakini inatumika upande wa Zanzibar , sasa suala ni kwamba labda pengine tutakuwa tumevunja Katiba. Jibu ni kwamba kwa mujibu wa Katiba yenyewe ushuru wa bidhaa ambao ni mapato ya Muungano ni ule tu unaokusanywa na Idara ya Forodha. Mabadiliko haya hayahusishi mapato yanayokusanywa na Idara ya Forodha. Fedha inayohusika kwa hiyo haitaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hivyo haimo katika *Appropriation Act,* 2007 iliyopitishwa juma lililopita. Kwa hiyo, jibu ni hilo kwamba tuko sawa sawa ndani ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya mafuta na bidhaa nyingine kupanda, niseme kwamba pamoja na sheria hii ya *EWURA* ambayo wengi pia wameisemea na napenda kuwashukuru kwamba itatoa meno zaidi hasa meno kwa *EWURA* lakini pia itakuwa inaangalia *formular* za bei na jinsi wafanyabiashara walivyonunua walipoingiza wanauza kiasi gani.

Pia kuhusu hili suala kwamba bei za mafuta kuweza kupanda nafikiri kwamba ni tatizo ka muda kwa sababu mtakumbuka hata mwaka jana wakati wa bajeti pale ambapo tulipoondoa *VAT* tukaingiza *excise duty,* hapa tulizungumza kwamba bei itapanda sana, ilipanda halafu baada ya hapo ika-*stabilise.*

Hata hivyo, jana nilikuja kutoka Dar es Salaam nilikuwa naona njiani kwamba kuna mabadiliko ya bei. Kwa mfano, hata hapo Morogoro bei ya dizeli mpaka shilingi 1,340/=. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo kwa kweli bei iko chini na hata wale ambao watasafiri wataona kuna shemu nyingine iko juu, lakini nafikiri hii itaweza kuwa-*stabilise* na hasa kwa kuwapa meno pia *EWURA*.

Lakini niseme pia naungana na wasemaji wengine kwamba fedha hizi tulizosema za kupandisha bei ya mafuta kwa shilingi 100/= zinakwenda moja kwa moja kutengeneza barabara zetu. Kwa hiyo, hata matatizo naamini ya mafuta kuwa katika bei ya juu katika mikoa ya mipakani pale ambapo barabara zitatengenezwa na kuimarishwa naamini kabisa kwamba mafuta haya pia yatakuwa chini kwa sababu barabara zitakuwa nzuri , hawatoharibu matairi na kadhalika.

Lakini pia niseme jana nilikuwa naangalia intaneti Marekani. Marekani kwenye *Congress* yao hivi sasa wanazungumzia kuongeza kodi ya mafuta kutokana na kuanguka daraja la Misisipi. Nafikiri mmesoma wengi kwamba daraja limeanguka na watu kadhaa wakaumia. Kwa hiyo, Marekani na wale ambao wanataka kwenda kwenye intaneti itaonyesha kwamba Marekani wanalizungumza sasa hivi *Congress* kwamba kuongeza kodi.

Sasa mimi nikajiuliza, nikasema kwamba Marekani ambao tunasema *big power* inaongeza kodi ya mafuta kwa ajili ya *infrastructure*, kwa hiyo Tanzania *actually* tuko *ahead.* Mara nyingi sana unajua watu wanasema kinachofanyika Marekani basi kinaigwa tu. Sasa labda pengine kipindi hiki ni tofuati kwamba Tanzania nao iko *ahead* katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya Bima kwamba marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Bima kwa kipindi hiki kwa kweli yasingeweza kuletwa katika vikao hivi, yatahitaji kufanyiwa kazi na tunapenda kusema kwamba tunaahidi kwamba suala hili tutalifanyia kazi na kuona jinsi gani tutakavyoweza kuliweka.

Kuhusu suala la ushuru wa ngozi na kwamba hautafaidia wafugaji. Niseme kwamba lengo hasa hasa la Serikali na naamini la Bunge hili ni kuwezesha Taifa kusindika ngozi. Hatua hii ina faida zifuatazo: Kwanza kabisa itafufua viwanda vya ngozi, uzalishaji. Hapa siku zote tunazungumzia uzalishaji. Tunapozungumzia hata suala la *inflation,* tunazungumzia fedha zetu zinaporomoka, tunazungumzia uzalishaji kwa sababu tumeona kwamba zaidi tunaagiza kutoka nje. Tukiagiza kutoka nje utahitaji Dola za Marekani na kwa maana hiyo hutohitaji shilingi ya Tanzania. Lakini kama tutazalisha nchini tutahitaji zaidi fedha shilingi ya Tanzania ambayo kwa kweli itanunua malighafi mbalimbali, itaajiri wafanyakazi na kadhalika na ndiyo maana hivi leo kwa mfano, unaweza kusema kwamba Japani imekuwa *strong* sana kwa sababu *yen* yao pia *strong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari yote haya aina ya Toyota na kadhalika yanayotoka Japani, kwa hivyo *yen* inatumika pale Japan katika uzalishaji wa magari haya. Kwa hiyo, naamini kwamba pale ambapo tutaweza kufufua viwanda hivyo nia mojawapo ni kufufua viwanda lakini pia kuongeza nafasi za ajira na kuwapatia wafugaji soko la hakika la ngozi ghafi. Itabidi kwa kweli viwanda hivi viweze kununua ngozi ghafi kutoka kwa wananchi hapa hapa. Fedha ambazo tutategemea kuzipata ni shilingi bilioni 2.6 kutokana na marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala hili la chakula na kwamba chakula kimepanda na kadhalika. Niseme kwamba nashukuru pia kuna wengine ambao wamesema hapana utafiti uliofanyika. Kwa sababu nakumbuka kuna wakati ndizi zilikuwa nyingi sana, nyanya hivi sasa nyingi sana, vitunguu vingi sana; kwa hiyo, ni kwamba inakwenda juu inashuka chini. Ndiyo maana nasema suala zima la uzalishaji na *inflation* kubwa ya Tanzania ni kutokana na vyakula. Utaona kwamba pale ambapo kulikuwa na ukame au chakula bado hakijatoka mashambani *inflation* ilikuwa juu. Ilifika mpaka mpaka 7.2 % baadaye ikashuka 6.2%, sasa hivi 5.9%. Kwa hiyo, utakuta kwamba uzalishaji nafikiri kwa hapa, *basket* ya *inflation* kubwa, nafikiri kama kwa asilimia 51 au 52 ni kutokana na uzalishaji wa chakula. Kwa hiyo, pale ambapo kwa kweli tutaweza kuzalisha zaidi naamini kabisa kwamba hali yetu pia ya *inflation* itakwenda chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa 5.9% sio mbaya kwa maana kwamba bei za mafuta hapa zimepanda na pia nje zilikuwa zimepanda. Kwa hiyo, suala la *inflation* mimi nafikiri linakuwa linakwenda juu na chini kama uchumi unaweza kwenda. Kwa hiyo, niseme kwamba katika suala hili si suala la kurudisha *price control*. Habari zaidi kama tulivyosema ni kuongeza uzalishaji na pia kuboresha miundombinu na bei siku zote tunasema kwamba ni matokeo ya *demand and supply*. Pale ambapo *supply* itaongezeka na kama miundombinu mizuri ndiyo sababu kodi ya mafuta imeongezwa ili fedha hizi ziweze kutengeneza barabara zetu.

Kitu muhimu nafikiri kwamba sasa katika kipindi hiki cha mwaka mmoja kuhakikisha kwamba fedha hizi nyingi zilizopelekwa kwenye barabara basi toune matokeo yake katika kipindi hiki kinachokuja. Hili nafikiri litakuwa ndiyo jambo muhimu sana. Kwa sababu *otherwise* kwa kweli tutakuwa tumefanya kazi bure ya kuongeza shilingi 100/- lakini barabara zisijengwe au zisitengenezwe. Sasa hili nafikiri ndiyo suala la kubanana kwamba tuhakikishe hili linafanyika na kama tulivyosema kwamba kuna *expenditure tracking system* ambayo inatarajia ifuate kule kule. Je, barabara hii ilikuwa itengenezwe kwa kiasi fulani, imetengenezwa? Haikutengenezwa. Hili nafikiri ni kazi kubwa tutakayokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la adhabu kwamba labda adhabu sio kubwa sana. Napenda kusema kwamba pale tulipotoka ni kwamba na wale ambao wako kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi watajua, kwamba adhabu ilikuwa shilingi 4,000/- kutoka 4,000/- ikaenda 5,000/-, 20,000/-. Sasa tumetoka hapo tumesema angalau basi iwe 1,000,000/= hadi 5,000,000/= . Kwa hiyo, mtaona kwamba tumetoka mbali, ambapo adhabu ilikuwa ya chini kabisa na labda tuseme kwamba basi tuanze na faini hizi ambazo

tunazipendekeza kwenye Muswada na kisha tuangalie. Tunaweza kufanya marekebisho kama kutakuwa na ulazima hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vifaa vya uokoaji ambalo limezungumzwa na niseme tutaliangalia hili lakini nakumbuka kama vile liliondolewa kodi miaka iliyopita. Lakini niseme kwamba tutaliangalia hili suala, kama ni hivyo basi tutaliangalia ni jinsi gani ambavyo tutaweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo napenda tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Naamini kwamba baada ya Sheria hii basi tutahakikisha kwamba wale wafanyabiashara wanaoongeza maji sijui kwenye mafuta ya taa pengine Sheria hii itafanya hili jambo lisifanyike. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Bungeni Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2007 *(The Finance Bill, 2007)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa jinsi ambavyo ameweza kujibu hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezileta na pia hoja za Kambi ya Upinzani. Nina swali moja. Kuna hoja moja ambayo Msemaji wa Kambi ya Upinzani ameizungumza na Mheshimiwa Waziri na nadhani labda kwa sababu ya muda hakuweza kupata muda wa kuijibu ambayo ningependa aweze kujibu.

Tulipendekeza na hili ni pendekezo ambalo tumekuwa tukilirudia mara kwa mara kwamba katika hii Sheria tuweze kuweka Sheria maalumu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunalinda magunia ya katani ya ndani ili kuzuia ushindani kutokana na magunia ya *jute.* Ninaomba Mheshimiwa Waziri aweze kuelezea jambo hili tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa niliiruka hii kwamba suala hili la magunia ya katani ni kwamba tumesema tunalichukua ili tuweze kulifanyia kazi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nipate maelezo kidogo tu kwenye hilo jedwali. Katika Hotuba ya Waziri wa Fedha kulikuwa na Leseni za Magari zimepandishwa viwango kufuatana na *CC* zake. Sasa nimejaribu kuangalia katika jedwali hili na katika Muswada huu sioni mahali ambapo suala hili linazungumzwa.

Naomba nipate maelezo ni wapi linazungumzwa. Unakumbuka kwamba magari leseni zake zimepandishiwa kufuatana na *CC*, kiwango cha chini kabisa ilikuwa ni shilingi 50,000 ikaenda mpaka shilingi 330,000. Sasa sijaona kwenye Muswada huu wapi inaelezwa hiyo. Ahsante.

**MWENYEKITI**: Tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri aendelee kuliangalia hilo, tutalirudia.

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17
Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Sasa tunarudi kwenye Ibara ya ya Sita, Mheshimiwa Waziri!

Ibara ya 6.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pamoja na ile ya tozo ya maliasili na utalii ni kwamba imewekwa kwenye *Government Notice* tayari ya tarehe 29 Juni. Kwa hiyo, hii tayari imekwishaanza kufanya kazi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2007 *(The Finance Bill,2007)***

***(Kusomwa Mara ya Tatu)***

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2007 *(The Finance Bill, 2007)* Kifungu kwa Kifingu pamoja Marekebisho yake. Naomba kutoa hoja kwamba Taarifa hiyo hivi sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa taratibu zetu hapo ndipo tumefikia mwisho wa suala hili la *The Finance Bill* kwa kulitaarifu Bunge rasmi sasa kwamba Mswada wa Sheria ya Fedha mwaka 2007, umepitishwa rasmi na Bunge hili.

**Muswada ya Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Mwaka 2007 *(The Higher Education Students' Loans Board (Amendment) Bill 2007)***

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Namba 9 ya mwaka 2004, sasa usomwe mara ya pili.

Kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa ambaye kwa Uenyekiti wake mzuri umewezesha Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kushirikiana na Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Omar Kwaangw,' Mbunge wa Babati Mjini, kwa maandalizi ya uwasilishwaji wa Muswada huu.

Maoni mazuri ya Kamati zote mbili yamesaidia sana kuboresha maudhui ya Muswada. Serikali imepokea na imezingatia maoni ya Kamati zote mbili kama yanavyoonekana katika Jedwali la marekebisho ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa. Aidha, ushauri wa Kamati zote mbili katika baadhi ya maeneo utazingatiwa wakati wa kuunda kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Bodi ya Mikopo na katika masuala ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tangu tupate uhuru Serikali imekuwa ikigharamia sehemu kubwa ya gharama za Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na kujenga vyuo, kulipa mishahara ya wafanyakazi, uendeshaji pamoja na gharama za moja kwa moja kwa wanafunzi.

Gharama hizo ni kama vile ada, posho ya Elimu ya Juu na nauli ya kwenda na kurudi chuoni. Licha ya kufanya hivyo mahitaji ya Elimu ya Juu yamekuwa yakiongezeka wakati uwezo wa Serikali kugharamia Elimu ya Juu umekuwa ukipungua kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wanaohitaji kupata Elimu ya Juu. Kutokana na ongezeko la mahitaji ya Elimu ya Juu na kupungua kwa uwezo wa Serikali kugharamia elimu hiyo utaratibu wa uchangiaji gharama yaani *cost sharing* uliandaliwa. Utaratibu huo ulianisha awamu tatu za utekelezaji utakaowezesha wazazi na wanafunzi kuchangia Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 1992/1993 ambapo wanafunzi walitakiwa kujilipia gharama za usafiri kwenda chuoni na kurudi nyumbani, gharama za udahili na usajili pamoja na michango ya Serikali za wanafunzi. Gharama hizi zilikuwa ni ndogo na kila mwanafunzi aliweza kuzimudu. Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Sera hii ulimhitaji mwanafunzi pamoja na gharama za awamu ya kwanza alipie chakula na malazi. Gharama hizi ambazo kwa wakati huo zilifikia shilingi 350,000/- kwa mwaka, zilionekana kuwa kubwa kwa wanafunzi walio wengi.

Ili kuhakikisha kuwa kuna fursa sawa katika utoaji wa elimu ya juu Serikali ilianzisha utaratibu wa mikopo ya kutoka Serikali moja kwa moja ili wanafunzi ambao hawana uwezo wa kujigharamia waweze kukopeshwa. Utaratibu huu ulianza kutumika mwaka wa masomo 1994/1995 na uliendelea kutumika hadi mwaka 2004/2005.

Awamu ya Tatu, ilianza kutekelezwa mwaka wa masomo wa 2005/2006 baada ya kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Awamu ya Tatu ilimtaka mwanafunzi agharamie pamoja na gharama zilizotajwa kwenye awamu ya Kwanza na ya Pili gharama zote nyingine za masomo, yaani ada ya masomo, elimu kwa vitendo, mahitaji maalumu ya vitivo, vitabu na viandikio na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ni utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 inayotamka bayana dhana ya uchangiaji wa Elimu ya Juu. Aidha, kuanzishwa kwa Bodi hii kulenga kutoa fursa kwa wanafunzi wenye sifa za kitaaluma na ambao wana uweza mdogo kiuchumi kuweza kugharamia Elimu ya Juu na kwamba utaratibu wa mikopo inayotolewa na Bodi unakuwa endelevu.

Azma ya Serikali ni kuongeza udahili wa wanafunzi kwenye vyuo vya Elimu ya Juu ili kuongeza idadi ya wataalamu wenye fani mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa letu. Ili kuweka utaratibu huo kisheria Sheria ya Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitungwa mwaka 2004. Sheria hiyo iliunda Bodi ambayo ilianza kazi rasmi mwezi Julai, 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Bodi ilikumbana na changamoto kadhaa. Changamoto hizo ndiyo kiini cha mapendekezo ya marekebisho yanayowasilishwa leo. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatazo:

(i) Mtazamo wa kwamba fedha inayotolewa ni ruzuku na si mkopo.

(ii) Ukinzani baina ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004 na Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 kwenye maeneo kadhaa yakiwemo maeneo ya mikopo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, umri wa mwombaji, mikopo kwa wanafunzi wa shahada za Uzamili na Uzamivu, wanafunzi wanaorudia mwaka na wale wanaorudia mitihani.

(iii) Kutokuwepo na masharti mahususi ya kisheria kuhusu urejeshwaji wa mikopo.

(iv) Kutobainisha wajibu wa mwajiri na mwajiriwa katika urejeshwaji wa mikopo.

(v) Bodi kutokuwa na njia au vyanzo vingine vya kujipatia fedha badala yake kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

(vi)Kutokuwepo masharti mahususi ya kuwadhibiti wanaodanganya na kujipatia mikopo; na

(vii) Wajibu wa wazazi au walezi kuchangia Elimu ya Juu kutokuwa bayana ndani ya Sheria.

Changamoto hizi zimeathiri ufanisi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, na hivyo upo umuhimu wa kufanyiwa marekebisho sheria hii ninayohusika. Aidha, Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 iko katika hatua za mwisho za uhuishwaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni na sababu ya mapendekezo ya marekebisho ni kama ifuatavyo:

(i) Kuondoa ukinzani uliopo baina ya Sera ya Elimu ya Juu ya Mwaka 1999 na Sheria ya Elimu ya Juu ya mwaka 2004.

(ii) Kuweka bayana masharti mahususi ya urejeshwaji mikopo kwa maana ya wajibu wa wadhamini, mwajiri, mwajiriwa na wale wanaojiajiri wenyewe.

(iii) Kuandaa mazingira ya Bodi ya Mikopo kubuni njia mbalimbali za kujipatia fedha baada ya kutegemea chanzo kimoja tu.

(iv) Kuweka bayana taratibu na adhabu kwa wale wanaofanya udanganyifu wakati wa kuomba na kupatiwa mikopo.

(v) Kuweka bayana vipengele ambavyo havikuwa wazi kwenye Sheria mama kama vile Uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi, Uwekezaji wa muda wa fedha za Bodi na kadhalika.

(vi) Kuanisha wajibu wa wazazi na walezi katika kuchangia gharama za Elimu ya Juu; na

(vii) Kuwezesha makundi mbalimbali ambayo awali hayakuwa yamezingatiwa kwenye sheria hasa wenye ulemavu na wasiojiweza kujipatia mikopo kama vile viziwi wasioona na wenye ulemavu wa viungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa marekebisho haya Wizara imewashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kote nchini.

Aidha, Wizara ikishirikiana na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliunda Kamati iliyozunguka nchi nzima kukusanya na kuratibu maoni ya wadau kuhusiana na marekebisho yanayopaswa kufanyika. Wizara ilibuni utaratibu uliowezesha kuwashirikisha wadau wengi zaidi katika marekebisho haya kwa kuigawa nchi nzima katika Kanda Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau walikusanywa kwa njia mbili: kwanza, wadau mbalimbali waliombwa kutoa maoni yao kwa njia ya maandishi na walifanya hivyo.

Wadau wengine hususan wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu kote nchini walifanya mikutano na Kamati iliyoundwa na kutoa maoni yao. Taasisi na Vyuo vya elimu ya juu ambavyo vilitembelewa na kutoa maoni yao mbele ya Kamati ni kama vifuatavyo:-

(i) Kanda ya Ziwa ambayo inajumuisha vyuo vya *St. Augustine University,* Bugando *University of Health Sciences,* Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mwanza.

(ii) Kanda ya Kaskazini inajumuisha vyuo vya Tumaini *University, KCMC* na Makumila *University Colleges,* Moshi *University College of Cooperative and Business Studies*, Mwenge *University College, Institute of Accounts* Arusha, Arusha *University,* Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

(iii) Kanda ya Nyanda za Juu inajumuisha vyuo vya Mkwawa *University College of Education,* Iringa *University College,* Ruaha *University College*, Mbeya *Institute of*

*Science and Technology,* Theophil Kisanji *University*, Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

(iv) Kanda ya Kati inajumuisha vyuo vya Sokoine *University of Agriculture*, Mzumbe *University,* Muslim *University of* Morogoro, *Institute of Rural Development Planning*, *Christian Council of* Tanzania, Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma.

(v) Kanda ya Mashariki na Zanzibar inajumuisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam *University College of Education,* Muhimbili *University College of Health Sciences*, *University College of Land, Architectural Studies, Institute of Finance Management, College of Business Education.*Tanzania *Institute of Accountancy,* Dar es Salaam *Institute of Technology,* Dar es Salaam *Marine Institute.*

Nyingine ni: *Herbert Kairuki Memorial University, Zanzibar University, College of Education Zanzibar, State University of* Zanzibar, Sekretarieti ya Mkoa wa Unguja, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Zanzibar Mjini pamoja na Shirikisho la Vyama vya Walemavu Tanzania, *Tanzania Episcope Conference* na Baraza Kuu la Waislamu.

(vi) Kanda ya Magharibi inajumuisha Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora, na Halmashauri ya Wilaya ya Tabora.

Aidha Wizara na Serikali kwa ujumla wake inaishukuru sana Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ambayo ilitoa maoni kama Kanda maalumu ya saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara mbalimbali, Wahisani Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Dini, Chama cha Waajiri Tanzania, na Menejimenti ya Vyuo vya Elimu ya Juu, walitoa maoni yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao na Serikali imezingatia maoni hayo katika kuboresha marekebisho yanayowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yanayotarajiwa endapo Bunge litaridhia marekebisho haya ni kama ifuatavyo:-

(i) Dhana ya kwamba Fedha inayotolewa ni ruzuku itaondoka.

(ii) Bodi itakuwa na uwezo wa kutoa na kukusanya marejesho ya mikopo kwa ufanisi zaidi.

(iii) Bodi itakuwa na uwezo wa kupata fedha zaidi kulingana na vyanzo vilivyoainishwa katika Sheria ya Bodi ya Mikopo na hivyo kuweza kuwakopesha wanafunzi wengi zaidi.

(iv) Ukinzani uliopo kati ya sheria ya Bodi na Sera ya Elimu ya Juu utakuwa umeondoka.

(v) Bodi itakuwa na uwezo zaidi wa kuwabaini na hata kuwachukulia hatua za kisheria wale wanaofanya udanganyifu katika kujipatia mikopo.

(vi) Makundi zaidi ambayo awali hayakuzingatiwa yataweza kupata fursa ya kuweza kupata mikopo.

(vii) Utekelezaji wa Sheria utakuwa wenye ufanisi zaidi baada ya vipengele ambavyo havikuwa wazi hapo awali kuwekwa bayana; na

(viii) Misingi ya kisheria kuhusu wajibu wa wazazi na walezi kuchangia elimu ya juu utakuwa umewekwa bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukamilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho yanayowasilishwa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilizingatia na kuhakikisha kwamba, maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Baraza la Mawaziri, Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kushirikiana na Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, yametekelezwa. Hivyo basi, ni matarajio yangu kwamba, Bunge litajadili na kisha kuridhia na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuwasilisha na kutoa maelezo kuhusu Muswada huu na kupitia kwako, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu, kwa kuniwezesha kusimama hapa ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu wa mwaka 2004. Nakushukuru wewe pia kwa kunipatia nafasi ya kufanya mawasilisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni ya Kamati, kwa niaba ya Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwawa, nachukua fursa hii, kwa niaba ya Kamati, kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa wafuatao: Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum,

Marehemu Stephen Kazi, aliyewahi kuwa Mbunge wa Mwanza Mjini, Marehemu Omari Chubi, aliyewahi kuwa Mbunge wa Kilwa Kaskazini. Aidha, Kamati inatoa pole kwako Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu, jamaa na Wananchi wa Mkoa wa Tabora, kutokana na kifo cha Mzee wetu, Chifu Abdallah Saidi Fundikira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi yetu tunamkumbuka Mzee Fundikira, kwa mengi. Kwanza, katika miaka ya 50, jinsi alivyojitolea kuuweka pembeni Uchifu, kuungana na Marehemu Baba wa Taifa na wanasiasa wengine katika kupigania uhuru wa nchi yetu. Kama walivyofanya machifu mashuhuri akiwemo Chifu Adam Sapi Mkwawa wa Wahehe na Chifu David Kidaha Makwaiya wa Wasukuma. Anakumbukwa pia kwa kuwa Waziri wa Kwanza wa Serikali ya Tanganyika, Rais wa Umoja wa Waislamu wa Afrika ya Mashariki *(East African Muslim Association)* na Mwenyekiti wa Kwanza wa Shirika la Ndege la Afrika Mashariki. Mwisho na muhimu zaidi kwa Kamati hii, alipokuwa Mbunge wa Kuteuliwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kati ya mwaka 2000 – 2005, Mzee Fundikira alikuwa Mjumbe wa Kamati hii. Yeye na Mzee mwenzake, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, ambaye kwa sasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii, walikuwa washauri wakuu wa Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, natoa salamu za rambirambi kwa ndugu na jamaa wote, waliopoteza ndugu zao, kutokana na ajali mbalimbali zilizotokea hivi karibuni. Mungu azilaze roho za Marehemu hao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu wa Mwaka 2007 *(Higher Education Students' Loans Board (Amendements) Bill, 2007).* Kutokana na uzito wa Muswada huu, baada ya Mheshimiwa Spika kuipelekea Kamati hii kazi ya kuujadili, Kamati ilitenga jumla ya siku mbili, kuushughulikia kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii.

Kamati ilifanya hivyo kwa kuzingatia kuwa Muswada huu unahusu utekelezaji wa mojawapo ya mikakati ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kuwekeza katika Elimu kwa kuwawezesha wasomi wengi zaidi, kupata elimu ya juu kwa kuzingatia vipato halisi vya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa yaliyowasilishwa na Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mbunge wa Kilolo, akisaidiwa na Naibu wake, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mbunge wa Viti Maalum. Kama alivyoeleza mtoa hoja, pamekuwa na changamoto nyingi dhidi ya suala hili, kwa hiyo basi, kwa muhtasari; Muswada huu unalenga kufanya marekebisho katika Sheria ya Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sheria Na. 9 ya Mwaka 2004 *(The Higher Education Students' Loans Board Act, 2004)*, kama ifuatavyo: -

(i) Kuondoa ukinzani kati ya sheria na sera ya elimu ya taifa;

(ii) Kuondoa malalamiko na migomo ya wanafunzi wa vyuo vikuu inayotokana na utoaji wa mikopo yaliyojitokeza hivi karibuni kwa wanafunzi ambao wameomba kukopa fedha kwa ajili ya kugharamia mafunzo yao;

(iii) Kumpa Rais mamlaka ya kumteua Mwenyekiti wa Bodi badala ya Mwenyekiti huyo kuteuliwa na Waziri;

(iv) Kuipa Bodi uwezo wa kusimamia utaratibu wa kutafuta fedha, kutoa mikopo na urejeshaji, utaratibu ambao utawarahisishia wanafunzi husika kurejesha mikopo hiyo. Aidha, marekebisho hayo yanakusudia kuweka masharti yatakayohakikisha kuwa mikopo kwa wanafunzi inarejeshwa;

(v) Kuipa Bodi uwezo wa kuwachukulia hatua za kisheria watakaoshindwa kurudisha mikopo;

(vi) Kuipa Bodi mamlaka ya kuwekeza fedha za ziada kwa lengo la kutunisha mfuko wa Bodi; na

(vii) Kuongeza vyanzo vya mapato kwa kumpa Waziri mwenye dhamana ya fedha kupeleka kwa Bodi sehemu ya kiasi cha tozo za mwaka zinazotokana na makusanyo halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, sasa naomba nijielekeze kwenye maoni ya Kamati kuanzia na Muundo wa Bodi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imebaini kuwa Muundo wa Bodi wa sasa kama ulivyoelezwa katika kifungu cha 5 cha Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 hauridhishi, kwani hauzingatii uwakilishi wa wadau wa elimu ya juu.

Muundo huo una Wajumbe wasiozidi kumi na nne, kumi wanatoka kwenye Wizara za Serikali, mmoja mmoja kutoka taasisi zifuatazo: Vyuo Vikuu vinavyomilikiwa na Serikali, Vyuo Vikuu vinavyomilikiwa na Taasisi Binafsi, Chama cha Waajiri Tanzania na mwisho Mwenyekiti wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa Muswada huu unagusa maslahi ya Taifa letu na maslahi ya wananchi walio wengi kutoka maeneo mbalimbali. Kwa sababu hiyo, kuwepo kwa wadau mbalimbali katika Bodi hiyo ni jambo lisiloepukika. Kwa hiyo, Kamati yangu inashauri kuwa Muundo wa Bodi urekebishwe kwa kuzingatia uwakilishi wa wadau mbalimbali wa elimu ya juu, ambao Kamati inaamini kuwa watawasilisha michango mbalimbali ya mawazo kulingana na maslahi ya wale wanaowakilishwa. Aidha, inashauriwa kuwa Wakurugenzi na Maafisa kutoka kwenye Wizara na Ofisi mbalimbali za Serikali wanaopendekezwa kuwa Wajumbe chini ya kifungu cha 5(1) cha Sheria Na.9 ya mwaka 2004, wasiwe Wajumbe wa Bodi kwa sababu Bodi inaweza kuwashirikisha kutoa ushauri wakati wowote itakapowahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali, Muswada huu pia unapendekeza kuipa Bodi uwezo wa kuwekeza fedha za ziada. Kamati inaafiki kuwa hili ni wazo zuri. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa pale itakapotokea kwamba Bodi inatakiwa kuwekeza fedha za Mfuko, ichukue tahadhari kuhakikisha kuwa manufaa yanayokusudiwa katika uwekezaji wa fedha hizo, yanapatikana na kwamba hakutatokea upotevu wa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya waombaji wa mikopo ya mafunzo ni kubwa kuliko fedha zinazotolewa na Serikali kila mwaka hivyo, kuilazimisha Bodi kufanya mchujo usiozingatia mahitaji ya wanafunzi wenye sifa za kujiunga na Vyuo Vikuu au Vyuo vya Elimu ya Juu. Kamati inashauri kuwa, Serikali itenge fedha za kutosha ili waombaji wengi zaidi wapate mikopo. Aidha, asilimia 0.5 inayopendekezwa kutokana na ushuru wa kuendeleza taaluma *(Skills Development Funds)* ni ndogo sana. Kamati inashauri kuwa ushuru huo uongezwe angalau ufikie asilimia 2.5. Ili kuwezesha ongezeko hilo, Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie vyanzo vingine vya fedha vitakavyosaidia kuutunisha Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, Kamati imegundua kuwa wananchi walio wengi, wana uelewa mdogo sana kuhusu masharti na taratibu za kuomba mikopo ya mafunzo. Inaonekana kuwa wananchi wengi wanaelewa kuwa mikopo hiyo ni misaada ambayo haina umuhimu wa kurejeshwa. Isitoshe mbali ya mikopo wanayopewa wanafunzi, wananchi hawaelewi mchango wa Serikali katika mikopo hiyo ni kiasi gani.

Kamati inashauri kuwa, Wizara iandae utaratibu wa kuwaelimisha wananchi juu ya mikopo hiyo na umuhimu wa kurejesha mikopo ili watu wengi wapate fursa ya kukopa na kujiendeleza kielimu. Aidha, Serikali iweke utaratibu utakaohakikisha kuwa waajiri hawatakiuka utaratibu wa kuwasilisha makato ya mikopo ya wafanyakazi wao waliofaidika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwepo kwa mahitaji maalumu ya wanafunzi wenye ulemavu wanaojiunga na elimu ya juu. Kwa kuzingatia mahitaji yao halisi, Kamati inapendekeza kuwa wanafunzi walemavu wapatiwe mikopo itakayokidhi mahitaji yao ya pekee. Aidha, Kamati inashauri kuwa mikopo kwa wanafunzi hao na muda wa kurejesha mikopo hiyo uzingatie hali yao halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nihitimishe kwa kukushukuru kwa mara nyingine, kwa kunipatia nafasi hii ya pekee kuwasilisha Maoni ya Kamati. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla, akisaidiwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika na wataalamu wao wote, kwa kuuwasilisha vyema Muswada huu mbele ya Kamati, kutoa ufafanuzi wa kina na kuzingatia ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, chini ya Uongozi wa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa kushirikiana vyema na Kamati yangu, kuujadili Muswada huu na kutoa michango ya kina iliyouboresha Muswada.

Naomba nitumie fursa hii pia kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, walioshiriki katika kuchangia Muswada huu kama ifuatavyo: Mheshimiwa Geroge M. Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athuman S. Janguo, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian Foka, kwa kuiwezesha Kamati hii ifanye kazi vizuri. Vilevile nawashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Charles Mloka, Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Emmanuel Mpanda, kwa kuihudumia Kamati, ikiwemo utayarishaji wa maoni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitoe shukrani zangu binafsi pia za Kambi ya Upinzani kwako Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na kwa kazi kubwa iliyofanyika ya kuongoza Bunge hili kwa kipindi chote cha bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 43(5)(c), Toleo la 2004, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu marekebisho ya Sheria ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ya mwaka 2007 *(The Higher Education Students' Loan Board (Amendment) Act, 2007)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Spika, kwa kufiliwa na mjomba wake, Mzee wetu, Marehemu Chifu Abdallah Fundikira. Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi, *amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho yanayofanywa katika sehemu ya nne ya Sheria na katika Muswada huu, inaonekana katika sehemu ya pili ya marekebisho ya jumla, *eligible student, means a Tanzania student who fulfils conditions stipulated under section 17 and any other condition as may be stipulated by the Board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya Ibara ya 17, tafsiri ya neno *eligible student* sehemu ya mwisho ya *any other condition as may be stipulated by the board,* yaondolewe kwa kuwa yanaipa mamlaka bodi ya kuweka vigezo vya ziada vya nani anastahili kukopeshwa zaidi ya vigezo vilivyomo kisheria, ambavyo tayari vinajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki kikiachwa kinaweza kutumiwa vibaya baadaye na bodi kuweka vigezo vyenye kuchochea ubaguzi ama kuwanyima fursa kundi fulani la wanafunzi. Nyongeza hii ya tafsiri ndiyo inayotaka kutumika kuhalalisha uamuzi wa bodi wa kukopesha kwa madaraja (daraja la kwanza na la pili - *division one and two*), badala ya kukopesha kwa misingi ya kigezo cha udahili *(admission),* kama sifa ya msingi iliyomo kwenye sheria mama. Hapa ndipo tutakapoendelea kuwa na matabaka ya hali ya juu katika elimu nchini, kwani wanafunzi wanaopata daraja la tatu *(division three)* na kadhalika, ndio hao hao wanaosomea katika mazingira magumu katika shule za watu wa kawaida, wakati shule ambazo wanapelekwa wenye uwezo na kufaulu vizuri, ndio hao hao baadae sheria inawatambua kuwa wanastahili mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kwa kuangalia kifungu 17(1)(c) cha Sheria, si wote wanaohitaji msaada huo, aidha wazazi ama walezi na hata *guarantors*. Mfano mzuri ni wale wote walio yatima na watoto wasiokuwa na makazi maalum, ambao elimu zao za awali zilihudumiwa na wachache wenye kujitolea au wasamaria wema. Kutokana na sheria ngumu na zinazomfunga *guarantor*, watu wengi hawatakuwa tayari kuwasaidia watu wasio na watoto wao. Tungependa kujua upatikanaji wa elimu ya juu kwa kundi hili, utalindwaje hasa pale matokeo ya masomo yao yatakapowaruhusu kuomba kuendelea na elimu ya juu na wakakosa *guarantors*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 17(1)(d) cha Sheria, Kambi ya Upinzani ianaona kuwa itakuwa vigumu sana kutambua mwanafunzi mwenye *financial assistance* na asiyekuwa nayo. Baadhi ya vigezo tulivyowahi kusikia kama vile kumtambua kwa kuangalia shule za sekondari alizosoma kama ni za *academy* au za kiserikali, havitoshelezi kutoa picha halisi, kwani wapo waliosaidiwa na wasamaria na misaada hiyo haipo tena. Hivyo, naomba Wizara ieleze ni vigezo gani hasa vitatumika ili kumtambua asiye na msaada wa kifedha na aliye nao bila ya kubagua na kumnyima haki yake ya msingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kifungu cha 17(1)(e) katika sheria, marekebisho yake katika Muswada huu bado hakioneshi kwa wale wanaorudia mwaka kwa kufanya vibaya mitihani yake au kupata matatizo yatakayoeleweka, apatiwe mkopo ili aendelee na masomo yake. Matatizo ni sehemu ya maisha na kama mwanadamu, hayaepukiki. Kundi la watu kama hawa, lisikilizwe na lipatiwe haki yake ya msingi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iliangalie suala hili kwa umakini vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha sita cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha sita cha sheria, katika kifungu kidogo kipya cha "c", kinachoeleza mchakato mzima wa utoaji wa mikopo na ukusanyaji/urejeshwaji wa mikopo, limetumika neno *granting*.

Serikali ili kuwafanya wanafunzi wengi kuwa katika ari ya ushindani na katika ngazi za chini, pamoja na kuwa na wanafunzi wengi wanaochukua masomo ya sayansi ili kukidhi kilio cha Wabunge wengi na Serikali kwa ujumla, kuhusu wanafunzi wanaosomea masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, ingekuwa bora kukawa na motisha kwa wanafunzi wanaofaulu vizuri toka ngazi za chini katika masomo ya sayansi kwa kuwapa *grants* asilimia fulani na *loan* kuwa asilimia fulani. Tulikuwa tunashauri kati ya asilimia 100 za mkopo, asilimia 70 wapewe wale wanaofaulu vizuri masomo ya sayansi kama *grant* na zilizobaki asilimia 30 ziwe ni *loan*. Hii itawafanya waendelee kufanya vizuri masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 5(a) cha Muswada kinachofanyia marekebisho ya kifungu cha 7(1)(c) cha Sheria, nanukuu: *"To borrow money for any purpose deemed fit by the board and, subject to any law in relation to investment of funds by a trustee, to invest in land or government securities or other interest bearing assets such funds as may be vested in it and which may not be immediately required for current expenditure."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inauliza kama Mifuko ya Hifadhi za Jamii kama *PPF, PSPF* na *NSSF,* ina fedha ambazo ni fedha za watumishi? Iweje bodi iazime pesa kutoka katika mifuko hiyo, wakati wanaokopeshwa na bodi hiyo uhakika wao wa kurudisha pesa hizo ni wa mashaka *(risk factors)?* Hii ni kwa sababu Serikali haina mkakati wa kueleweka, utakaohakikisha wakopaji wake wanarudisha fedha hizo na kwa wakati mwafaka. Je, watumishi wakistaafu pesa za kulipa mafao yao zitatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16(3), *The Board shall determine percentage of the amount of the sum that shall be contributed by a student, a parent, a guardian or other person concerned as the case may be.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona huu ni uonevu na utarudisha nyuma juhudi za Serikali za kuongeza Watanzania wenye elimu ya juu. Watanzania walio wengi ni maskini na hivyo suala la kuchangia ni gumu sana. Watoto wa wakulima na walio maskini, ndio wanaosoma kwenye vyuo hapa nchini. Serikali iwahudumie watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19(4)(a) nanukuu: "*Arrange with the employer, monthly deductions from his salary for remittance to the Board and of such amount and for such period as shall be determined by the Board."* Yaani ni kwamba inasema kuwa: "Kwa kushirikiana na mwajiri, Bodi itapanga kiasi cha fedha na muda wa kumtoza mwajiriwa (aliyekopeshwa na Bodi) kwa kila mwezi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa ajira ni tatizo tosha linaloongeza mashaka ya wakopeshwaji kushindwa kumudu ulipaji wa deni. Kwa hiyo basi, Serikali iongeze juhudi za kutosha katika kudhibiti tatizo hili la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ibara ya 19(4)(b) inasema kuwa, makato yote ya mwajiriwa aliyekopeshwa na Bodi, hayatazidi moja ya tatu ya mapato yote baada ya makato ya kisheria kufanywa *(total net income per month).* Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, mkopeshwaji hana budi kushirikishwa kikamilifu katika kupanga kiasi na muda wa kurudisha malipo hayo kwenye Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo, mwajiri na mwajiriwa, washirikiane kikamilifu katika kupanga kiasi na muda wa kurejesha malipo hayo bila kuathiri au kuleta usumbufu kwa pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha moja ya tatu ya mapato pia isiwe sawia kwa kila mwajiriwa, mkopeshwaji, bali yawe na madaraja kulingana na kipato cha mtu. Pia ni vyema makato hayo yazingatie na makato mengine ya mfanyakazi kama vile *NSSF, PSPF, PPF,* kodi ya mapato na vyama vya wafanyakazi, isije ikaongeza hali ngumu ya maisha ya mfanyakazi kwa mshahara wote wa mfanyakazi kuishia kwenye makato mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Amendment of Section 21(2),* ambayo naomba kunukuu: *"Where any person employs a loan beneficiary and fails to disclose or conceals such information to the Board or fails to arrange for repayment plan with such beneficiary, such person commits an offence and shall be liable upon conviction to a fine of seven million shillings or imprisonment for a term not less than twelve months or to both."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ni mzigo usio na sababu kwa mwajiri. Hii inaweza kupelekea uwepo wa ugumu wa kuajiriwa kwa watu waliosoma kwa mikopo. Kwa kifupi, Sheria inaweza kuwa moja ya kigezo cha kukosa kazi, kwani hakuna atakayetaka kusumbuka kwa ajili ya matatizo ya mwingine. Mwajiri asihusishwe na mambo ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21(2) ya Muswada huo, inaonesha kuwa, mwajiri atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa zinazohusu wafanyakazi wake walionufaika na mikopo ili kuepuka kushtakiwa. Pia mwajiri yeyote atakayeshindwa kutoa taarifa kwa Bodi ya Mikopo, juu ya mfanyakazi wake, atakuwa amefanya kosa la jinai na ataweza kutozwa faini ya shilingi milioni saba au kwenda jela miezi kumi na mbili na adhabu hizo hazitazingatia wala kuzuiliwa na Sheria za Makampuni zinazowalinda maofisa wake, kutoshtakiwa kwa makosa ya makampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sheria hizo, Kambi ya Upinzani inaona athari katika soko la ajira, hasa kwa wanafunzi waliosomeshwa, wanaosomeshwa na watakaosomeshwa na Bodi ya Mikopo, hasa katika mwelekeo wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Duniani kote, kwani itasababisha ubaguzi wa ajira kwa Watanzania waliosomeshwa na Bodi ya Mikopo kutokana na waajiri kuja kukwepa usumbufu uliopo

katika Muswada huo. Hivyo, waliosoma nje ya Bodi (matajiri), watakuwa na soko kubwa kutokana na kutokuwa wasumbufu kwa waajiri. Hivyo, kuendeleza matabaka katika jamii ya Watanzania kati ya waliosomeshwa na Bodi na wasiosomeshwa na Bodi katika kupata fursa za ajira chache zilizopo hapa nchini. Kambi ya Upinzani tunashauri kuwa kiwango cha adhabu ya faini ya shilingi milioni saba ni kikubwa sana na ingefaa izingatie uwezo, ukubwa na mtaji anaomiliki mwajiri, kampuni au shirika lililomwajiri mwajiriwa (mkopeshwaji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21(4)(2) inasema kuwa, iwapo waajiri wote watakaoajiri mtu aliyesomeshwa na Bodi ya Mikopo na akashindwa kutoa taarifa kulingana na Sheria, Bodi ya Mikopo itakuwa na Mamlaka ya kulidai Shirika hilo kulipa kiasi chote anachodaiwa mkopeshwaji kwa malipo ya mara moja (mwajiriwa wake). Pia Ibara ya 21(5) inasema kuwa, mtu yeyote atayekuwa kizuizi cha kumzuia Afisa wa Bodi au Wakala wa Bodi kufanya kazi yake, atakuwa ametenda kosa la jinai na atapelekwa Mahakamani na akipatikana na hatia, atalipa faini ya shilingi milioni saba. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, kiwango cha shilingi milioni saba ni kikubwa hivyo, kiwango cha adhabu kizingatie uwezo na mtaji wa kampuni, Shirika au Taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 inayofanyiwa marekebisho katika *section 22(d),* ambayo naomba kunukuu: *"Where the debt is due and payable to the Board and the loan beneficiary fails to pay the loan, he pays the loan as if he were the loan beneficiary and all recovery mechanism shall apply against the guarantor."*

Suala la kuwa na *guarantor* kama nilivyokwisha kusema awali, litasumbua sana. Kwa hiyo basi, Serikali iongeze jitihada za dhati na iwe *guarantor* wa wale wote watakaokopa. Serikali inaweza kuwa ya Kijiji ama Serikali Kuu, kutegemeana na mazingira. Pia sheria hii ni ngumu kiasi kwamba, mtu akizijua hatakubali kuwa mdhamini na hii itafanya watu wengi kukosa wadhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kambi inashauri Serikali ibuni njia mbadala, itakayomwezesha mkopaji kurejesha mkopo pasipo kumwingiza hatiani mwajiri. Ni wazi kuwa katika Muswada huo, mwajiri anaingizwa hatiani kwa mkataba uliofanywa kati ya mwanafunzi na Bodi ya Mikopo, tena mkataba asiyohusishwa. Muswada huu kwa kuwaingiza waajiri katika hatia ni sawa na Serikali kuwaambia waajiri, wasiajiri wanafunzi waliosomeshwa na Bodi ya Mikopo ili waepuke usumbufu wa kuja kufungwa au kulipa faini ya shilingi milioni saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya 2004 na sera nzima ya gharama ya uchangiaji *(Cost Sharing),* kama inavyoitwa, hailengi kukuza elimu na moyo wa kizalendo miongoni mwa wanafunzi na raia wa Kitanzania, kwani mwanafunzi pindi amalizapo masomo yake, anajiona kuwa hana deni au mzigo wa kuisadia nchi hii, kutokana na kujigharamia masomo yake kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inazidi kuisisitizia Serikali ya Tanzania kutoa elimu kwa wanafunzi wote watakaopata udahili wa chuo *(admission),* badala ya kuwabebesha Watanzania mzigo mzito wa gharama ya uchangiaji, ambao kiuhalisia ni gharama bebeshi *(Cost Bearing).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfumo ulioko hivi sasa, mwananchi anabeba mwenyewe mzigo wa gharama ya elimu ya juu kwa asilimia 100. Kupitia mfumo huu, hivi sasa mwanafunzi anakopeshwa kati ya 0% hadi 100%, ambazo anawajibika kuzirejesha amalizapo masomo yake. Hivyo, mfumo huu ni ubebaji wa gharama *(Cost Bearing)* na si uchangiaji wa gharama *(Cost Sharing).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waziri kusema wadau walishirikishwa kikamilifu, naomba atuhakikishie ni vipi wadau walishirikishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa, hakukuwa na ushirikishwaji wa kutosha wa wadau na wananchi katika mchakato wa maandalizi ya Muswada huu. Kwa sababu kuna ngazi mbili za kuwashirikisha wananachi. Ngazi ya kwanza ni katika kukusanya maoni ya awali kabisa, kuhusu hoja ambazo zinatarajiwa kufanyika. Hapa ni kweli Wizara ilishirikisha baadhi ya wawakilishi wa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ngazi ya pili ni baada ya Muswada kuandaliwa, hapa Muswada ulipaswa kuwekwa wazi kwa umma. Serikali iliweka wazi Muswada huu kwa kuuchapa kwenye Gazeti la Serikali *(Government Gazette)*, tarehe 22 Juni, 2007. Gazeti la serikali ni nini? Kwa kuwa ni gazeti linalosomwa na wachache, tofauti na *mainstream papers* kama gazeti la Serikali la Habari Leo au *The Daily News,* tunadhani ni vyema Muswada ungewekwa kwenye tovuti *(website)* ya Taifa na ya Bunge. Pamoja na kuwa Bodi ina uwakilishi wa baadhi ya wadau, wawakilishi hawaondoi umuhimu wa wadau wenyewe kushirikishwa. Tunaamini kwamba, kama Muswada huu ungewekwa kwenye tovuti, basi wananchi wengi au wadau wengi, wangeweza kuuona na kuutolea ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba, mabadiliko haya ya sheria yalipaswa kujadiliwa kwanza na wadau wafuatao: Wanafunzi na Vyama Vyao katika vyuo mbalimbali vya umma na vya binafsi; Vyama vya Wafanyakazi, hii ni kwa sababu walipaji wa mikopo ni waajiriwa; suala la makato yao ni sehemu ya mijadala ya haki za wafanyakazi kama ilivyo katika michango mingine ya kisheria kama ile ya mifuko ya jamii; Chama cha Waajiri, sio *ATE* pekee, hata waajiri wa sekta mbalimbali kwa ujumla wao; Wananchi kwa ujumla hususan wazazi, walezi na wadhamini. Ushirikishwaji finyu wa wadau ni msingi wa migogoro wakati wa utekelezaji wa sheria. Hoja hii ni muhimu kwa kuwa wanafunzi walioko vyuoni hivi sasa na vijana waliomaliza hivi karibuni, ambao wanapaswa kulipa mikopo, wanashangaa kuhusu uwepo wa mabadiliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho haya ya Sheria, Serikali imeendeleza upungufu wa kuona Bodi ya Mikopo kama Taasisi ya kutoa msaada wa mkopo na si kutoa mahitaji ya mkopo kwa wanafunzi. Ikumbukwe kwamba, hii ni mikopo ambayo inahitaji kurejeshwa hivyo, uhusiano kati ya mkopaji na Bodi unapaswa uwe hivyo na si uhusiano wa hisani. Kwa ujumla mtazamo wa Sheria nzima ni finyu badala yake ilipaswa kuwa na tafsiri inayozingatia misingi mitatu muhimu: *Eligibility* (anayestahili mkopo lazima apewe); *Need* (mkopaji anapaswa kupewa kwa kadiri ya mahitaji na si vinginevyo) ; na *ability to pay* (mkopeshwaji anapewa fedha kwa kadiri ya

uwezo wake wa kulipa). Sasa kwa kuwa tayari kwenye fomu kuna kipengele cha *guarantee* ama *guarantor,* tayari *underlying basis* ni kuwa kila mkopeshwaji anaweza kulipa. Hivyo, mkopo kamili ni haki ya wanafunzi wote wanaotimiza misingi hii mitatu na si hisani ya Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Ibara 5, kuongezwe Mwakilishi wa *Workers Union* (Vyama vya Wafanyakazi katika orodha ya Wajumbe wa Bodi ya Mikopo). Hii ni kwa sababu masuala ya urejeshaji wa mikopo *(loan repayment)*, yanahusisha wafanyakazi hivyo, lazima kuhakikisha haki zao zinalindwa katika hatua zote. Kama kuna mwakalishi wa Chama cha Waajiri katika Bodi ya Mikopo, kwa nini pasiwe na Mwakilishi wa Shirikisho la Wafanyakazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16(1)(f) cha Muswada kinachosema, nanukuu: "*Special needs for students with disabilities as the Board shall determine.*" Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa ni lazima kwa wale wote ambao ni walemavu na hawana uwezo *(students with disabilities),* kupatiwa mahitaji yao maalumu na kwa kiwango kinachoridhisha kulingana na hali zao na hali ya maisha. Sanjari na hilo ni lazima kuwa na *minimum requirements* na sio Bodi iachiwe kutoa uamuzi kwa vigezo hivyo, pia mkopo utakaotolewa uendane na hali halisi ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kutoa pongezi zetu kwa Muswada huu kuwajali walemavu kwa kutoa kipaumbele katika kuwapatia mikopo kwa mahitaji maalumu kama Ibara ya 16(2)(f) inavyotamka. Hata hivyo, kifungu (c) na kifungu (d) ni vyema vikapingwa kwa nguvu zote. Vifungu hivi vinalenga kuhalalisha maamuzi ambayo yameshafanyika tayari ya kutotoa mikopo katika mahitaji yote na hata katika yale mahitaji ambayo wanatoa kwa misingi ya asilimia tu. Huu ndio msingi wa 40% na hata katika mazingira ya sasa ya kukopesha kwa kuangalia mtu usoni kwamba, huyu akopeshwe 80% huyu 10% na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi anaweza kuomba mkopo kwa kadiri ya hali yake ya kiuchumi, lakini Bodi kwa sababu mbalimbali, inaweza ikampa kiwango kidogo na kuleta utata**.** Lakini kwa upande mwingine, uamuzi wa Serikali kuweka vifungu hivi ni ushahidi wa wazi kuwa Serikali ilikiuka sheria ilipoweka 40% na kwamba sasa inataka kuhalalisha uamuzi wake pengine baada ya tamko la Wapinzani kuwa watakwenda mahakamani kupinga uamuzi wa Serikali. Lakini hapa napo panaleta tatizo lingine la ziada; kuanzia wanafunzi wa mwaka gani vifungu hivi vipya vya sheria vitatumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba,, vikitumika kwa wanafunzi wanaoendelea *(continuing students)*, sheria itakuwa kama ni *restrospective* (yenye uwezo wa kurudi nyuma), kwani hawa ni wanavyuo ambao waliomba vyuo wakijua kwamba watapewa mkopo kamili na Serikali. Ni wazi leo wakiambiwa kuchangia kwa kiasi kitakachoamuliwa na Bodi, wengi watashindwa kulipa na ushahidi uko wazi mpaka sasa *Tumaini University* na *St. Augustine,* Mwanza wanafunzi zaidi ya 400 wameshindwa kufanya mitiahani yao; katika vyuo vingine asilimia 60 ya wanafunzi hawajaweza mpaka sasa kulipa 40%, ingawa waliruhusiwa kufanya mitihani na hata hao waliolipa wengi

wamelipa kwa kuuza vitu ama kukopa, hali ambayo inaonesha kwamba, watashindwa kulipa katika miaka inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Ibara 19(b)(2), idadi ya siku 21 za kulipa fedha ama sivyo agizo la kushikiliwa kwa vitu na kuuzwa linatolewa ni dogo sana. Wengi watapoteza mali zao; kwa nini isiwe siku 90? Kifungu (b)(5), kwa nini agizo la kushikilia na agizo la kuuza litatolewa kwa pamoja? Kwa nini yasitenganishwe ili kutoa bado fursa ya mtu kufanya malipo katikati? Kwamba, kama hatalipa siku 21 toka mali yake ikamatwe, ndipo hapo litoke agizo la kuuza. Hii itawezesha kuwa na *check and balance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Ibara ya 20(1)(b), inapendekezwa kuweka siku 28 za kutoa taarifa. Siku hizi zinaelekea kuwa ndogo; je, Sheria ya Makato ya Mifumo ya Jamii *(Statutory Payments),* inasema siku ngapi? Idadi ya siku inayotajwa kwenye sheria hiyo ndiyo iwe *standard*. Hii itasaidia kuwalinda waajiri dhidi ya kuhukumiwa kwa haraka kuwa wamekwepa kupeleka taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Ibara ya 21, kifungu kipya cha pili, kinachopendekezwa hususan faini ya shilingi milioni saba, kinaonekana kuwa ni kikubwa. Je Sheria ya Michango ya Wafanyakazi kwa ajili ya Mifuko ya Jamii/Pesheni inasema faini ya shilingi ngapi kwa waajiri wakiacha kupeleka michango ya wafanyakazi wao? Kiasi kilichomo humo ndio kiwe msingi wa kiwango cha hapa pia. Kama kiwango cha sheria hii kikiwa kikubwa kuliko cha michango mingine ya kisheria, kitapelekea waajiri kuogopa kuajiri wahitimu wa vyuo, ambao bado wana madeni ya mikopo, hususan waajiri walio katika sekta ya kati *(SME)*, ambao mitaji yao ni midogo. Kifungu cha sita, neno '*any record'* ya mwajiri ni vyema kikarekebishwa. Hii itawatisha waajiri kwamba, rekodi zao zozote zinaweza kutazwama kwa kisingizio cha kutafuta taarifa za mwajiriwa. Je, Sheria za Michango ya Kisheria *(statutory payments)*, zinasemaje kuhusu mipaka ya mamlaka ya kuchunguza taarifa? Mipaka hiyo itumike vilevile katika sheria hii. Je, mipaka ya haki ya faragha *(right to privacy)*, iko kwa kiasi gani katika suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekiri kwamba, sheria hii inatoa haki zaidi ya sera ya elimu, lakini cha kushangaza katika kikao kilichomalizika cha Bunge, imeahidi kuirekebisha sheria hii, kwa misingi ya mapendekezo ya awali yaliyotolewa na Wizara husika. Mabadiliko hayo yanalenga kuhalalisha maamuzi yaliyokwisha kuchukuliwa, hali ambayo itarudisha nyuma kasi ya kuongeza elimu ya juu nchini. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 44 imeahidi kuwezesha 12.5% ya wahitimu wa Kidato cha Sita kufika Elimu ya Juu, pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni huko Mchinga, Lindi tarehe 23 Agosti, 2005 na maeneo mengine kwamba, mtawezesha vijana wa Kitanzania wapya 30,000 kuingia Chuo Kikuu kwa mwaka.

Katika mwaka 2005/2006, ahadi hii haijatekelezwa kwa ukamilifu wake, mfumo uliopo wa uchangiaji utakwamisha zaidi utekelezaji wa ahadi hii. Huu ni mkataba na wapiga kura na ni muhimu ahadi hii ikatekelezwa kwa kuwa tafiti zimeonesha uwekezaji wa kina na makini katika elimu ya juu kwa mwaka mmoja huongeza Pato la Taifa kwa

asilimia 0.63 (Rejea Hotuba ya Bajeti ya Wizara husika 2006/2007) na kwamba ni msingi muhimu katika kutekeleza MKUKUTA na kutimiza Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(MDGs)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu ni hitaji la Wananchi na Serikali yetu inao uwezo wa kuweka mazingira ya wanavyuo kuweza kusoma elimu ya juu**.** Sababu inayotolewa ya kutokuwapatia udhamini kamili wanafunzi ni kwamba, nchi yetu haina uwezo na kwamba kama uchumi wetu ukikua basi Serikali itabadili maamuzi yake. Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliwahi kutuasa wakati wa mjadala wa uchangiaji wa elimu kwamba, kama Taifa hatuwezi kujua gharama ya elimu mpaka tutakapojaribu ujinga, tunapaswa kujiuliza; kipi kinaaza elimu ama uchumi au vyote kwa pamoja? Kama nchi ambazo zina uchumi wa chini kuliko ya kwetu, zinawekeza katika elimu ikiwemo ya juu zaidi yetu; ni kwa vipi tutaendelea kwenda mbele zaidi yao?

Mathalani rejea viwango vya idadi ya wanafunzi katika nchi za *SADC;* Afrika Kusini 9.11%, Kenya 1.47, Uganda 1.23, Lesotho 0.98, Malawi 0.42, Msumbiji 0.33 na Tanzania 0.27. Nchi za Asia Mashariki *(The Tigers),* walikuwa na nguvu ya kiuchumi kama sisi katika miaka ya 1960, lakini pamoja na mambo mengine, kuwekeza katika elimu ya juu wameweza kufikia hatua waliyoko sasa, kwa nini sisi tuendelee kutumia umaskini wetu kama sababu ya kutowekeza kwenye elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG),* inaonesha kwamba, kwa mwaka 2005/2006 shilingi bilioni 700 hazieleweki matumizi yake na tayari tumeshazidisha bajeti kwa shilingi bilioni 900; kama Serikali kwa kipindi hiki imeweza kusamehe kodi na kwa kiasi kikubwa kwa wafanyabiashara wakubwa kwa takribani shilingi bilioni 400; kama tumeweza kuilipa Kampuni ya Dowans (kampuni iliyotokana na Richmond), shilingi zaidi ya bilioni 100, pamoja na kwamba mpaka sasa hawajaweza kutupatia umeme wa *megawatts* 100 kama ilivyokuwa katika mkataba ; kama tumeweza kuongeza idadi ya magari ya thamani (mashangingi) na semina elekezi; ni dhahiri kwamba uwezo tunao.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006, wakati ambapo hakukuwa na uchangiaji wa 40% wala madaraja katika utoaji wa mikopo, Serikali ilikopesha jumla ya wanafunzi 42,729, ambayo ni sawa ya jumla ya shilingi bilioni 62.9, (rejea Hotuba ya Waziri wa Elimu ya Juu akiwasilisha makadirio ya Bajeti ya Serikali 2006/2007).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo elimu ya juu ni gharama ambayo kama Taifa, tunaweza kuimudu. Kwa mantiki hiyo basi, baada ya Serikali kulipa 60%, tunaamini kwamba, kiwango cha 40% kilichobaki, Serikali inaweza kukimudu ndani ya bajeti inayoendelea hivi sasa, kwa kubadilisha mafungu ya bajeti ama kuahirisha ulipaji, isipokuwa suala la kuwalipa wanafunzi kikamilifu kwa ajili ya kwenda mafunzo kwa vitendo, ambalo lipaswa kufanyika sasa mpaka mwaka wa fedha 2007/2008. Izingatiwe kuwa, fedha hizi ni mkopo kwa hiyo, sio gharama zinazozama ni uamuzi wa kutunisha Mfuko wa Bodi ya Mikopo, ambao kwa msingi wake wa kisheria, fedha zake ni za mzunguko *(revolving).* Ikumbukwe kwamba, elimu (ikiwemo elimu ya juu) ni hitaji la

kipaumbele kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Ni dhahiri kwa muktadha wa Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu Tanzania *(Poverty and Human Development Report)*, Watanzania walio wengi, hususan wa vijijini, hawana uwezo wa kuchangia 40% ya elimu ya juu, ambayo ni kati ya shilingi 500,000 na 1,500,000, ukijumlisha ada ya masomo, matibabu, gharama za mafunzo kwa vitendo na michango mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa, Serikali itatingatia hoja hii ili tuweze kusomesha vijana wengi zaidi, hasa ikizingatiwa kuwa tunaingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki, Tanzania ikiwa nyuma kwa idadi ya wanafunzi walio Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana kwa kusoma maoni ya Kambi ya Upinzani. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, kuwa mchangiaji wa kwanza wa hoja hii, nilipata mawasiliano toka kwa Mheshimiwa Godfrey W. Zambi akisema kwamba, anadhani kikao hiki hakikupaswa kuendelea kwa sababu anaamini tupo chini ya nusu ya Wabunge wote na hapa tunafanya maamuzi muhimu na anatoa maoni hayo kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1) hadi (3) na Kanuni ya 68, Toleo la 2004. Ameomba Mwongozo wa Mwenyekiti na mimi ninamwongoza ifuatavyo:-

Ukisoma Kanuni zile 63(1) inasema kiwango cha mikutano na vikao vyote vya Bunge wakati wa kufanya maamuzi kitakuwa ni nusu ya Wabunge wote. Sasa hivi ni wakati wa majadiliano. Kwa hiyo, akidi inayozungumzwa katika Kanuni ya 63(1) ni pale Bunge linapofanya maamuzi na siyo majadiliano. Kama ulivyosema Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, ungeweza kutoa hoja chini ya Kanuni ya 63(2) ili kengele ipigwe wakati ule wa kufanya maamuzi ili kuita Wabunge wote walioko katika Kamati na walioko nje, waje hapa ndani halafu tungehesabiana na kama Mwenyekiti angeridhika kwamba Wabunge wote waliomo ndani, ukiondoa yeye mwenyewe, hawafikii nusu, basi tungefanya maamuzi mengine. Lakini ni wakati wa kufanya maamuzi, kwa kuwa wakati huu ni wa majadiliano, tunaendelea na majadiliano.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu niendelee kuchangia katika majadiliano ya sasa hivi. Nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Naibu wake na Watendaji wote na hasa katika Bodi ya Mikopo. Mimi niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri ni jasiri, katika hili imemchukua muda sana kujadili suala hili la mikopo. Nadhani hata shughuli nyingine hafanyi kwa sababu anashughulikia suala la mikopo. Ni gumu na zito halafu ni zuri kwa nchi yetu na wahenga wanasema, bahari shwari haitoi boharia mashuhuri. Nadhani wale wanaofanya suala la mikopo ni majasiri na sasa hivi wana uzoefu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, ingawa wenzetu wanasema Mheshimiwa Waziri, pamoja na Bodi ya Mikopo hawajawashirikisha Wajumbe, mimi nimeshiriki tangu tulipoanza Bodi ya Mkopo mpaka juzi, tumekutana na wadau tumebishana. Kwa hiyo, nadhani sina sababu ya kuweza kupinga mawazo tuliyoyatoa.

Tatizo kubwa linalojitokeza katika hili ni kwamba, elimu ya juu sasa hivi inatakiwa na watu wengi, tatizo fedha hazitoshi. Mheshimiwa Waziri, pamoja na wenzake wanajaribu kupanua uwigo katika kuweka *regulations,* tatizo linakuja tu ni kwamba, zile fedha zinazotolewa ni kidogo. Mimi niiombe Serikali, kwa kweli kwa nchi yetu elimu ya juu ya sasa hivi ni kitu ambacho ni cha lazima, kama alivyosema mwenzangu kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki. Mapambano ya kule au ushirika kule si wa watu wasioelewa ni wa watu wanaoelewa, ruhusu vijana wetu waende vyuo vikuu wasome ndani na nje ya nchi, ndipo wataweza kushiriki na kuweza kujiendeleza vizuri. Naomba sana Serikali ijitahidi kutafuta fedha na ninaomba ieleweke mkopo ukishakuwa mkopo, lazima mdhamini awepo kwa sababu unarudi, sasa ukisema kwamba asiwepo mdhamini, atatishiwa ataogopa. Sasa ina maana tunatoa basi bure fedha hizo. Zinatolewa hizi fedha ni mkopo na ieleweke kwamba zinarudi na karibu nchi zote zinafanya hivyo.

Kwa hiyo, tutenge kiasi kikubwa cha kuweza kutosha. Katika Kamati tulifikiria labda *skill levy* inaweza ikasadia lakini nimepiga hesabu nikaona *skill levy* haiwezi kusaidia wanafunzi wetu. Tufanye jitihada za makusudi za kuwasomesha vijana na vijana wengi katika vyuo vyetu vikuu, wanabaki wengi wenye sifa, ambao wengine wanaanza kuhangaika wanatufa vyuo nchi jirani, wanaenda Kenya, Uganda, wengine wako Zambia, mimi nafikiri wote hawa wafikiriwe.

Kwa sababu anayesoma Chuo binafsi Uganda au Kenya, unakuta wakati mwingine ada ya kule iko chini, hana tofauti na anayesoma *St. Augustine* na wao wafikiriwe wapewe mkopo. Kulikuwa na wazo kwamba, labda tuwaachie mabenki ndiyo yaweze kuwakopesha, lakini benki mikopo yao ina *interest,* mkopo wa Serikali huu hauna *interest*, kwa hiyo ni kwamba unakopa leo milioni tano utaenda kuzilipa baada ya miaka saba, kwa hiyo, utakuta ule mkopo hata wale matajiri wanaona huu mkopo ni tulivu, ambao ukifika baada ya miaka saba, hauna gharama yoyote ni sawa sawa unaweza ukaulipa kwenye mshahara mmoja.

Kwa hiyo, ndiyo maana watu wanagombania huu na ninaomba watu waelewe kwamba, kila mmoja anayejua hesabu, hata ningekuwa mimi Mbunge, nikipiga hesabu mtoto wangu akisomeshwa kwa mkopo huo ni safi sana kuliko kutoa fedha yangu ya leo, kwa sababu baada ya muda fulani atalipa. Labda nilikuwa naomba mkakati wa kulipwa watu walipe na niwapongeze juzi walionesha mfano, baadhi ya Wabunge ambao wameanza kulipa, mmefanya vizuri sana wale ambao mmelipa mmekuwa mfano mzuri na wengine waelewe kwamba zinalipwa. Kwa sababu kama wataweka *interest*, maana yake gharama itakuwa inaongezeka kila wakati, lakini kama watu watakuwa wanalipa kwa hiari, basi twende hivyo.

Mimi nilikuwa nampongeza Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi, lakini ombi langu kwa Serikali, wale wote wanaochaguliwa, kama wanahitaji mkopo basi tuwawezeshe wakope. Tutafute kila namna, wakope waweze kusoma. Hii itasaidia hata vijana wetu ambao sasa hivi tuna shule ambazo huko vijijini kuna shule kama Bukondo, Kamena ni vijijini kabisa kule ndani, shule nyingine sasa atapatikana wapi wa *division one* na *division two*, hakuna kompyuta, hakuna umeme, kwa hiyo, watasoma wapi; wale

wanaokaa na Dar es Salaam, Mwanza, Moshi ndiyo watakaosoma. Lakini wale wanaosoma shule ambazo wanasema *St. Gasper,* hawa ndiyo wanaweza kupata nafasi, lakini kama tutawakopesha wote ambao wamechaguliwa kwenye vyuo vikuu, mimi nadhani tutakuwa na mafanikio makubwa sana.

Mimi naunga sana mkono hoja hii iliyoletwa mbele yetu, kwa kweli Mheshimiwa Waziri, nakupa pole kwa kazi unayofanya ni kubwa, naomba Wabunge wenzangu wote, tumuunge mkono. Wadau tumekaa nao wameshindwa kupata majibu ni kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, dakika zilizobaki hazifiki kumi na tano kamili ili tumtendee haki mchangiaji mwingine yeyote, isipokuwa nimepata mawasiliano na wachangiaji wengine ambao walitaka kuchangia.

Naomba nitoe tangazo moja kwamba, katika michezo ya timu ya *Bunge Sports Club*, siku ya Jumamosi ambapo *Bunge Sports Club* ilienda Mpwapwa, naomba kutangaza matokeo yetu ya *Bunge Netball,* ambayo iliishinda Timu ya *Mpwapwa Combine* kwa jumla ya magoli 20 kwa magoli manane. Tangazo hili lilipaswa kusomwa mapema, tunaomba mtuwie radhi kwa usumbufu ulitokea. *(Makofi)*

Tutakaporudi jioni ya leo, tutakuwa na wachangiaji watatu ambao ataanza Mheshimiwa Magreth A. Mkanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles N. Keenja na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto. Baadaye tutaendelea na utaratibu kama Meza itakavyoelekeza.

Kwa kufikia hapo, shughuli zilizopangwa asubuhi ya leo zimekamilika, naomba nisitishe Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

*(Saa 06.48 mchanga Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza asubuhi, tunaendelea na uchangiaji na utaratibu mwingine. Lakini ningependa kusema hapa mapema, kuna Wabunge wawili, watatu, ambao wasingependa Muswada huu upite bila kuwa wameongea kitu, mnaruhusiwa kuniandikia kwa sababu muda naona upo upande wangu, ninaweza kuona nini naweza kufanya. Vinginevyo, moja kwa moja naomba nimwite Mheshimiwa Magreth A. Mkanga.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika marekebisho ya Muswada huu. Kwanza, natoa pongezi kwa Timu ya Bunge ya *Football* na *Netball,* kwa kuonesha

ushindi tangu Jumamosi ile na mpaka Jumamosi iliyopita ila jana pakatokea dharura kidogo, lakini najua wanaweza sana hawa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, natoa rambirambi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na familia yake, kwa ujumla kwa kumpoteza mjomba wao, babu yetu, mimi nilikuwa ninakaa naye mstari mmoja alipokuwa Mbunge. Ni babu ambaye alikuwa na hekima, alikuwa anatoa maongozo, alikuwa anatulea na alikuwa anatushauri. Kwa yote yaliyotokea ni mapenzi ya Mungu, naomba Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amen.*

Pia natoa rambirambi kwa wana-Mpwapwa, kwa Mheshimiwa George M. Lubeleje na Mbunge mwenzake, kwa tukio lililotokea la kupinduka gari na kwamba kwa taarifa ya asubuhi, kuna wawili wamepoteza maisha. Inasikitisha kwa sababu kufariki kwa ghafla nako kunatia uchungu zaidi. Lakini basi Mungu ndivyo alivyowaandikia kwamba, wasafiri kwa mkondo huo nao nawaombea kulala mahali pema peponi na majeruhi waweze kupona ili waweze kuendelea na shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Bodi ya Mikopo na Timu nzima ya Wizara hii, kuweza kutuandalia marekebisho ya sheria hii tena haraka katika nia nadhani ya kuweka sawa suala la mikopo kwa wanachuo, wazazi, walezi, *guarantors,* waajiri na niseme jamii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho haya, mimi nimefarika sana na kufurahi kwa sababu kuna kipengele kipya kilichoongezwa kwenye marekebisho haya tofauti na ilivyokuwa kwenye *principal,* Muswada ule au ile Sheria ya mwanzo. Marekebisho haya yamejitokeza kuwa na nyongeza, *section 16* sehemu ya 7(f) na katika Muswada wa sasa ukurasa wa sita ilipofafanuliwa vizuri kabisa kwamba, Bodi ya Mikopo itatoa mikopo kwa ajili ya mahitaji, maalum kwa wanachuo wenye ulemavu. Hili mimi nimelifurahia sana na ninaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kuwa na mwono wa kuangalia kundi hili liwezeshwe namna gani kwa hali na mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kufahamu vifaa hivyo maalum, vitakavyokuwa *accommodate* kwenye mkopo huu ni vipi? Kwa sababu ninajua kila aina ya ulemavu ina mahitaji yake maalum. Kwa hiyo kwanza, ningepata *clarification* ya vifaa hivyo. Je, ni pajaji mpaka *hearing aid?* Kwa hiyo, watanisaidia kunifafanulia sawa sawa hivyo vifaa ni vipi na ningeomba viwe vyovyote ambavyo vitawawezesha wanachuo hawa kuweza kumudu masomo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, lakini mimi ningeomba kabisa kwa dhati kushauri kutokana na vifaa ambavyo Bodi itaamua kuwakopesha wanaohusika, vifaa hivyo wanachuo hawa waondoke navyo. Isiwe ile lugha ya kusema ni vifaa vya mahitaji ya Idara Maalum, hapana waondoke navyo. Ataweza kupata Bajaji akaitumia pale Chuoni kuweza kumsaidia ku-*move* eti Bajaji hiyo ibaki kwa Idara. Sasa huyu anakokwenda huko, ulemavu ndiyo utaisha baada ya kumaliza tu chuo kwamba hatahitaji Bajaji? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kabisa hivi vifaa watakavyokopeshwa,

waondoke navyo ili kila anayekuja basi akopeshwe na ndiyo inakuwa uwezesho angalau wa kudumu, hata akimaliza chuo akabahatika labda kupata ajira, vitaweza kumsaidia vifaa hivyo kuendelea kujenga taifa katika ajira ya kuajiriwa au kujiajiri.

Mheshimiwe Mwenyekiti, kwa ujumla niseme kwamba, watu wenye ulemavu mpaka kubahatika kuwa na hatua ya kufika kusoma elimu ya juu, wanakuwa wamekwisha sumbuka sana. Wanakuwa wameshahangaika sana, wanakuwa wameshakuwa yaani basi tu ni wale wachache wanaobahatika. Mimi nasema ni wachache waliobahatika, wanakuwa wameshahangaika mno, mpaka hata kufika Chuo Kikuu matatizo yake mimi hapa nikiyasimulia, kutakucha kutakuchwa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwa sababu wanaofika vyuo vikuu ni wachache, hata habari ya mikopo kwa wanachuo wenye ulemavu isiwepo, wapewe *grant* wasomeshwe bure hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mfano, tumeweza kufikiria kwamba taaluma muhimu zinazohitajika haraka haraka wasome bure walimu na wahandisi, sasa hawa hawafikii hata idadi ya 100, ukijumlisha vyuo vyote watoto wenye ulemavu hawafiki wanaofika maeneo haya ya chuo kikuu. Kwa hiyo, mimi hawa nilikuwa naiomba Serikali kabisa wapewe *grant* siyo wala ya kurudisha, ni bure kabisa kwa sababu wameshateseka mno mpaka kufika hatua hiyo waliyofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *experience* yangu, watu wenye ulemavu wakifikia hatua ya kufika Chuo Kikuu huwa hawafeli, wanakuwa ni wale wenye akili kweli. Hawafeli, yaani tunajitahidi mno kwa udi na uvumba, kushindana kitaaluma mle ndani. Kwa hiyo, hawa siyo wale wa wasi wasi kwamba, hawatalipa sijui hawatafanya nini, wasaidiwe kwa sababu hata ile *brain* anayoitumia kwa nguvu zote, jamani *it is a gift* kwa Mungu. Kwa nini wasishukuriwe basi kwa kusomeshwa bure? Kwa hiyo, mimi ndilo ninalolisisitiza hapa wanachuo wenye ulemavu wawe ndani ya *private,* wawe ndani ya vyuo vya Serikali, kwa kweli wasomeshwe bure. Watatukumbuka maisha yao yote kwa sababu ni wachache na wengi wao wakishamaliza hata ajira zenyewe inakuwa tatizo kuzipata. Ninajibiwa hapa ninafahamu kwamba, kuna sheria zimebadilishwa, imewekwa tu *with disability no discrimination,* ile haijafanya kazi. Wanasota mno kupata kazi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita waliomaliza wanafahamu namba yangu ya simu, waliniomba Mheshimiwa ututafutie kazi. Mungu wangu, hivi mimi kazi naipata wapi? Inakuwa ni shida. Ninapoweza unaenda kama Halmashauri, jamani kuna mwanachuo huyu mlemavu amemaliza, chonde mtakapotoa *application* mfikirieni. Wengine nabahatika, wengine sibahatiki, wala hawapati kazi. Kwa hiyo, naomba kabisa hawa watu wasomeshwe, kama mama zao tulipata shida ya kukatwa mishahara tukajilipia, potelea pote, si lako wewe tatizo uliendeleze na mwingine apate tatizo hapana. Unamwandalia mapito mema, nadhani hili limeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hili, wala sikuwa na mengi, ninaamini Serikali imenisikia. Nataka kujua ni vifaa gani, *however expensive* kwa kweli wapewe bure na watoto hawa wasome bure, ili baadaye waweze kulijenga taifa hili bila

kuwa na wasi wasi, bila kuwa na *pressure* kwa sababu wanasoma kwa bidii na wote kabisa huwa wanafaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja nikitegemea hapa nitaambiwa kabisa Kanuni zitasema watasoma bure. Asanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu. Naomba nijiunge na Wabunge wenzangu wote, kumpa pole Mheshimiwa Spika, kwa msiba uliowapata na vilevile kumpa pole Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa George M. Lubeleje, kwa msiba wa watu waliokufa kwenye ajali ya gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, ningependa kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi anazozafanya za kuhakikisha kwamba, kunakuwepo na maendeleo ya elimu ya juu katika nchi yetu na kwa uongozi wake na Manaibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kueleza kwamba, mimi ni mdau katika suala hili kwa maana mbili; Kamati yangu ilipitia Muswada huu na pili natoka Ubungo na kama mnavyojua, kule Ubungo ndiyo kuna wanafunzi wengi sana wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hiyo, mimi ni mdau kweli kweli wa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nichukue nafasi hii, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma, kitakachochukua wanafunzi 40. Katika mwaka mmoja na nusu, chuo hicho tayari kimeshakamilika na naambiwa mwezi ujao kitaanza kazi. Hii ndiyo kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tumpongeze sana na kumshukuru kwa juhudi hizi anazofanya. Naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote walioanzisha vyuo vikuu, yakiwepo mashirika ya dini na watu binafsi, ambao naambiwa kwamba sasa hivi vyuo hivyo vimefika ukichukua pamoja na vya Serikali tumefikisha Vyuo Vikuu 32, katika muda usiofika miaka kumi, mtu ambaye amekuwa akiiangalia Tanzania atashangaa tulivyobadilika katika kipindi hicho kifupi. Tumebadilika katika elimu ya juu, tumebadilika katika elimu ya sekondari, tumebadilika katika elimu ya msingi, nafikiri tunakwenda vizuri na Mwenyezi Mungu akijalia, baada ya muda si mrefu hali yetu itakuwa nzuri sana. Kwa hiyo, wote hao nawapongeza kwa dhati kabisa, kwa kazi hizi nzuri wanazofanya ambazo zinahakikisha kwamba, sasa kuna nafasi nyingi za kutosha kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita kuweza kwenda Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali basi ikubali kama tulivyokubali katika shule za msingi kwenda sekondari kwamba, vijana watakaomaliza kidato cha sita, watakaopata sifa za kwenda Vyuo Vikuu na watakapotaka kwenda Vyuo Vikuu, basi nao wote waende chuo kikuu ili kujaza hizi nafasi ambazo tumekuwa tunaunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushe tu kwamba, vijana hawa wengi watakaokwenda Vyuo Vikuu ni watoto wa maskini. Ni watoto wa wazazi ambao hawana uwezo mkubwa sana. Ombi langu kubwa ni kwamba, katika kuamua ni kiasi gani cha mikopo wapewe, hili lizingatiwe. Kwa sababu kuna watoto ambao wanatoka katika familia ambazo hazina uwezo wa kulipa asilimia kubwa ya kiasi hicho kitakachohitajika kulipwa. Umaskini usiwe ni sababu ya mtoto kutokwenda Chuo Kikuu.

Kwa hiyo, nitategemea kwamba, katika kuweka viwango vya kulipwa wale wenye uwezo katika jamii yetu watalipa kikamilifu na wala siyo kulipa tu ile sehemu ya mkopo, lakini kulipia sehemu kubwa ya mafunzo ya watoto wao Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale ambao uwezo wao ni mdogo na mdogo kabisa basi na viwango vyao viteremke hivyo hivyo mpaka kumfikia huyo ambaye uwezo wake ni mdogo kabisa, ambaye anaweza akasomeshwa na Serikali bila hata kulazimishwa kuchangia. Nafikiri tukifanya hivyo, tutakuwa tumetenda haki. Hapa ndipo ninapopata tatizo, ninapoangalia marekebisho haya maana tulipoyapitia wakati ule tulikubaliana kwamba, suala hili lingetazamwa na katika marekebisho katika ainisho la *eligible student,* tukafuta *any other conditions* zinazoweza kuwekwa na Bodi, lakini tukaweka kifungu kingine kwenye fungu la saba, kifungu kidogo cha tatu cha huu Muswada tunaoupitia ambalo linasema kwamba, *the Board shall determine the percentage.* Sasa Bodi hii ina-*determine* nini tena na kwa misingi gani? Ni masharti gani tunayoiwekea ya ku-*determine* hii *percentage? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ama wanajiamkia tu wanasema leo 40%, mwaka kesho wanasema hapana, tumebadilika kidogo hatutaki tena 40% lipeni 50%. Sasa kama tunataka hili, lazima kiwepo chombo kitakachoweka kiasi kitakacholipwa, lakini chombo hicho lazima kiwekewe utaratibu utakaohakikisha kwamba, hakitafanya mambo yake bila kuzingatia hali halisi ya Taifa ilivyo. Kwa hiyo, ningetegemea kwamba, kifungu hiki kingekuwa na masharti na kwamba ambao hawataridhika na uamuzi, basi wanaweza wakakata rufaa kwa Waziri, ambaye ni mwanasiasa mwenzetu, tunaweza tukabanana hapa Bungeni ili atazame malalamiko hayo na kuyafanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki tungependa sana kitazamwe upya na kirekebishwe, kama hakiwezi kurekebishwa katika sheria, basi kirekebishwe katika Kanuni zitakazotungwa za kusimamia mikopo hii. Mimi nategemea baada ya kupitisha sheria hii, ile migogoro, migomo na malalamiko ya Vyuo Vikuu itapungua, kwa sababu itakuwa tumeweka misingi imara, itakayotumika katika kutoa mikopo na kila mwanafunzi atakayekwenda Chuo Kikuu atakuwa na nafasi ya kusoma Sheria hii, kujua haya ndiyo masharti yatakayomfunga na kwa hiyo kukubali. Lakini tukiacha mwanya ambapo Bodi inaweza ikabadilisha badilisha viwango vya *percentage* itakavyoona inafaa, bila misingi inayojulikana, hatutaondokana na malalamiko hayo na ningeomba kifungu hiki kitazamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu katika kifungu hicho hicho sehemu inayofuata pale mwisho inasema na atakayeamuliwa *percentage* hiyo atalipa *percentage* hiyo. Sasa

najiuliza, hivi kama kuna mtu ambaye hajiwezi kabisa, hawezi kulipa na amepewa *percentage* ambayo inazidi uwezo wake; inakuwaje? Maana kwa mujibu wa Sheria hii kila atakachoambiwa itabidi alipe na mimi ningefikiri hapa tungeweka utaratibu ambao mtu huyu anaruhusiwa kukiangalia kiwango kile alichowekewa na akiona kimemzidi uwezo, basi aweze vilevile kuwasiliana na Mamlaka itakayowekwa ya Rufaa ili kuomba afikiriwe upya, apunguziwe mpaka kibaki kima kile ambacho anaweza akalipa. Tukifanya hivyo, itakuwa na maana kwamba wenye uwezo watasoma wasiokuwa na uwezo watasoma na Taifa baada ya muda si mrefu, litakuwa ni Taifa la wasomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri, alitazame hili na baadaye atufafanulie ni nini anachofikiri kinapaswa kufanyika ili kuhakikisha kwamba, watoto wetu wote wanasoma. Lingine liko kwenye *paragraph* ya 18, kwa sababu jambo muhimu sana ni Bodi kuwa na fedha kama Bodi haina mapato, haitaweza kuwakopesha hawa watoto. Kwa hiyo, lazima tuweke utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kwamba, hii Bodi inapata fedha za kukidhi mahitaji yake. Chanzo kimoja ni bajeti ya Serikali. Kwa hiyo, Serikali itatoa pesa, itaweka katika Bodi hii, ili Bodi iweze kukopesha wanafunzi wa Taifa hili. Ni uwekezaji katika kuendeleza uma wa Tanzania. Kwa hiyo, ni pesa itakayokuwa imetumika vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kingine kitakuwa ni kiasi kile cha fedha kitakachokusanywa kutokana na watakaokopeshwa. Lakini chanzo kingine kimezungumzwa katika aya hii kwamba, ile *skills development levy* nayo itachangia, lakini kiasi itakayochangia ni kidogo sana ni *0.5 pecent*. Asilimia 0.5 maana hata hiyo asilimia ukiangalia inatisha kwa udogo wake. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ilipendekeza kwamba, kiwango hiki kitazamwe upya na katika mawasilisho yaliyofanyika asubuhi hii hapa, aliyofanya Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Kamati ilipendekeza kwamba, kiwango hiki kiongezwe kifike angalau asilimia 2.5. Sasa bila kuwa na takwimu, utafikiri pengine hili ni badiliko kubwa sana, lakini hii asilimia 2.5 inayosemwa hapa ni sawa sawa na shilingi zisizozidi 250 milioni. Lakini *skills developemtn levy* kwa mwaka inakusanya zaidi ya shilingi 53 bilioni. Kwa hiyo, shilingi 250 milioni katika 53 bilioni ni kiasi kidogo sana cha fedha, tusingeweza kuongeza tukawapa hata bilioni 2, 3 badala ya hizi shilingi 250 milioni ambazo haziwafikishi popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, alitazame suala hili na Serikali ilitazame suala hili. Katika hii *skills development levy,* tutenge angalau asilimia 5 au 6 iende katika mfuko huu kwa ajili ya kuwakopesha hawa wanafunzi waweze kusoma na kwa kupata fedha za kutosha, tutahakikisha kwamba watoto wote watakaofaulu kwenda vyuo vikuu wataweza kwenda Vyuo Vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naliomba kwa dhati kabisa tulitazame, kwa sababu kazi moja ya hivi Vyuo Vikuu ni ku-*develop skills* za watoto wetu katika nchi hii. Kabla sijakaa, ningependa nizungumzie suala moja zuri sana ninaloliona likifanyika katika nchi hii na ambalo limezingatiwa katika Muswada huu. Nalo ni kwamba, wanafunzi watakaofaidika na fedha hizi ni wanafunzi wa Vyuo Vikuu vyote, hili ni jambo la msingi sana kwamba, kuna mwanafunzi aliyepata sifa za kujiunga na Chuo cha Serikali pengine

akakosa nafasi akaenda akajiunga na ile *Morogoro Islamic University,* mwenye sifa sawa sawa na aliyejiunga na Chuo Kikuu aliyepata sifa za kwenda Chuo Kikuu, huyu naye kapata mkopo kwa maana hii.

Mimi naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu, ambao kwa kweli unazingatia haki. Kuna wakati tuliogopa kidogo kwamba, hii mikopo ikitolewa kiholela basi wanafunzi ambao hawakufaulu, ambao hawakupata sifa za kujiunga na Chuo Kikuu, wakapitia mlango wa vyuo vya kujitegemea ama vya watu binafsi, wakapata mikopo. Lakini msingi hapa ni kwamba, watakaopata sifa wakienda kwenye Vyuo vya Serikali watapata mikopo, wakienda kwenye vyuo vya madhehebu ya dini watapata mikopo na wakienda kwenye vyuo vya watu binafsi pia wakiomba watapata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili ni suala zuri sana. Sasa kazi iliyobakia ni kwa wanafunzi wetu kufanya bidii kuhakikisha kwamba, wanapopata nafasi hizi za kwenda Vyuo Vikuu wanazitumia na wanafanikiwa katika kile kinachowapeleka kule.

Nawaomba sana wanafunzi wanapopata sababu ya kutofautiana na uongozi wa chuo ama wa Serikali, wasigomee masomo. Wagomee mambo mengine yote, lakini darasani waende, maana kinachowapeleka Chuo Kikuu ni kusoma. Sasa wanapogomea lile jambo la msingi linalokupeleka Chuo Kikuu, sisi wazazi wenu hatuwaelewi.

Kwa hiyo, tungeomba sana wale vijana wanaopata nafasi za kwenda Vyuo Vikuu, watumie nafasi hizo kikamilifu kujiendeleza. Kwa sababu kujiendeleza kwao ndiyo manufaa ya Taifa hili, baada ya wao kumaliza masomo yao ya Chuo Kikuu. Wakitufanyia hilo, wametufanyia upendeleo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naomba niseme kwa dhati kabisa kwamba ,naunga mkono Muswada huu na naliomba Bunge hili nalo liunge mkono, wale watakaochangia kutoka pande zote mbili wakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Charles N. Keenja. Sasa kama nilivyosema mwanzo, namwita Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge ajiandae.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyingine, kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Elimu ya Juu *(The Higher Education Students' Loan Board Amendment Act, 2007),* ambayo inaifanyia marekebisho Sheria Na. 9 ya mwaka 2004, Sheria ambayo upitishwaji wake ulileta malalamiko makubwa sana kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapojenga misingi ya hoja yangu, naomba kurejea kauli ya aliyekuwa mgombea Urais wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoitoa huko Mchinga katika Jimbo la Mchinga, Mkoani Lindi, tarehe 23 Agosti, 2005 na alikuwa akinukuu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi,

ambayo iliahidi kwamba, mara baada ya Chama cha Mapinduzi kuwa kimechaguliwa, asilimia 12.5 ya wahitimu wote wa Kidato cha Sita wataweza kuingia Chuo Kikuu na kusomeshwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile najengea msingi hoja yangu, kwa kauli aliyotoa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati alipokuwa akizindua Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005 ambapo alisema kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, itafanya kazi ya kuimarisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili iweze kutoa mikopo kwa wahitaji wengi zaidi, tofauti na ilivyokuwa. Hii ndiyo misingi ya hoja yangu, wakati tunafanya Marekebisho ya Sheria Na. 9 ya mwaka 2004, Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya mabadiliko yoyote ya Sheria ni lazima kuwe kuna kasoro ambayo imetokea na ambayo tunataka kuirekebisha au sisi kama viongozi, tumeona kwamba kuna suala jema ambalo linapaswa kuchukuliwa na kuingizwa ndani ya Sheria ili liweze kushughulikiwa. Ni kweli kabisa kwamba, toka tumetunga Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu mwezi Aprili, 2004, kumekuwa na takriban migomo mikubwa miwili ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu. Migomo yote hiyo wanafunzi walikuwa wakilalamikia mikopo, utoaji wa mikopo na taratibu za mikopo. Kwa hiyo, kulikuwa na tatizo ama lilikuwa ni lazima liwe *addressed* ili kuweza kulitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kulikuwa na tatizo linalotokana na jinsi ambavyo wanafunzi wanaingia katika Shule za Msingi, Shule za Sekondari na hatimaye kuongeza idadi ya wanafunzi ambao wanamaliza elimu ya Kidato cha Sita. Kwa maana hiyo ni kwamba, lazima ilikuwa tuweke mazingira ya kuhakikisha kwamba, wanafunzi wengi zaidi wanapata mikopo ili waweze kupata elimu yao ya juu na nadhani huo ndiyo msingi halisi wa ahadi ambayo Chama kinachoongoza Serikali sasa hivi, kiliiweka kwa wananchi na ndiyo mkataba kati ya Chama na wananchi na watahojiwa mwaka 2010 kama wameweza kutekeleza kiasi gani na vilevile ndiyo msingi wa rejea wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo nimeieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 9 ya mwaka 2004, haikuweka madaraja ya jinsi gani ambavyo wanafunzi watapewa mikopo. Kwa mfano, sheria ilikuwa kimya kabisa kuhusiana na suala la asilimia 40 na asilimia 60 na sheria ilikuwa kimya kabisa kuhusiana na suala la madaraja, kwa maana *division one and two* na kadhalika. Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, alipokuwa anachangia alizungumzia tatizo alilokuwa analiona katika Ibara ya 7 ya Muswada na vilevile katika tafsiri ya *eligible students.* Lakini napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, mara baada ya Msemaji wa Upinzani ku-*raise* hoja hiyo, tulipitishiwa *ammendment* ambayo ilikuwa imefuta hiyo *concern* na kwa hiyo, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Kwa maana hiyo ni kwamba, sasa hivi Bodi itaweza kutoa mikopo kutokana na Sheria inavyotamka, badala ya kuweza kuweka viwango kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba kwa vyovyote vile bodi inaweka masharti, ili kutokana na uwezo wake wa kifedha, katika jambo la msingi sana ambalo

inabidi tulijadili ni kuangalia ni jinsi gani ambavyo sisi kama Taifa tunawezesha elimu ya juu yaani *Financing Higher Education*.

Nadhani hii ni *very critical issue* ili tusiweze kufanya maamuzi kutokana tu na jinsi gani ambavyo bodi ina pesa sasa hivi, ni lazima tuweze kuangalia Kamati ya Bunge imetoa mapendekezo kuhusiana *scheme development levy* lakini pia kuna mapendekezo kadha wa kadha ambayo yanatolewa kuhakikisha kwamba bodi iwe na fedha nyingi zaidi ili iweze kusomesha wanafunzi wote ambao wamedahiliwa kama jinsi ambavyo sheria inavyotamka.

Leo hii tunavyozungumza wanafunzi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii, Kijitonyama wamezuiliwa matokeo yao ya mwaka sababu tu ya kutokulipa *40 percent* na hii tunafahamu kabisa kwamba *40 percent* haikuwepo kwenye sheria, lakini kwa kuwa sheria imekuja tunaifanyia mabadiliko na *amendment* zimekuja, naamini kabisa kwamba sharti hili la wanafunzi wa Kijitonyama wataweza kupatiwa matokeo yao ili waweze kujua kama ni *supplementary or not* ili waweze kufanya mitihani yao na vile vile itakuwa ni kwa sababu sheria sasa imeweka *very clear* kwamba *board* haiwezi ikajiamulia ikajiwekea viwango gani ambavyo inatoa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuleta masikitiko tena kwa Mheshimiwa Waziri na ninaomba hili labda angeweza kulijibu kwa sababu watu wa bodi ya mikopo wapo, nimepata taarifa mchana huu kwamba sasa watu wenye *division two* wanaume wanaokwenda kuchukua fomu za mikopo, kwa sababu ya vile vigezo ambavyo bodi ilikuwa imeviwekwa katika *academic year* iliyopita.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sina uhakika kwa sababu nimetumiwa taarifa hii kwa *sms* na inawezekana ni mtu mmoja tu labda hakutimiza baadhi ya masharti, lakini kama suala hili lipo kwa kweli nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aweze kulielezea na awaeleze watu wa bodi kwamba asimnyime mtu fomu sababu tu amepata *division two* kwa sababu sheria haizui fomu zitolewe kwa namna gani. Naamini kabisa kwamba bodi lazima itoe fomu kwa watu ambao wamekuwa *admitted* katika vyuo vyetu ambao wamefanyiwa udahili na bodi itaamua kutokana na jinsi yenyewe ilivyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili jinsi gani ambavyo tunawezesha elimu ya juu iweze kuwa na mafanikio, tuweze kusomesha vijana wetu zaidi wanaomaliza kidato cha sita katika Vyuo Vikuu na taasisi mbalimbali ambazo ni za elimu ya juu. Lazima sasa tuanze kuliangalia uwezekano wa kutumia kodi zetu za matumizi, kwa sababu tuna kodi zinazotokana na forodha, tunakodi zinatokana na mapato ambayo wananchi wanapata. Lakini tuna kodi zinazotokana na jinsi ambavyo wanachi wanatumia vitu katika masoko yaani *consumption tax* na moja *consumption tax* tuliyonayo Tanzania ni *VAT* tuweze kuangalia uwezekano wa kuweka asilimia fulani ya *VAT* kwa ajili ya kusomesha elimu ya juu yaani kile kiwango cha *VAT* ambacho *TRA* wanakikusanya baada ya kwenda mfuko mkuu wa Hazina Waziri wa Fedha azitoe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, kuziingiza katika bodi ya mikopo ya elimu juu ili tusiwe na ukosefu wowote wa fedha kwa ajili ya kusomesha raia wetu. Mimi ningependekeza kwa mfano, kiwango cha kati ya asilimia moja na asilimia mbili ya *VAT* kinatosheleza kabisa kabisa kuweza kusomesha vijana wetu. Kwa sababu kwa mujibu wa Bajeti ya sasa ambayo ni takribani

shilingi bilioni 159 kwa ajili ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu ni asilimia takribani 1.5 tu ya *VAT* ambayo Waziri wa Fedha alitangaza kwamba tunarajia kuweza kuikusanya.

Kwa hiyo, tungejaribu kuangalia uwezekano huu ili tuwe chanzo cha uhakika cha kuweza kusomesha raia wetu. Huko Botswana wameamua kabisa kwamba mapato yote yanayotokana na almasi ambayo inauzwa nje yanaenda katika sekta ya elimu. Kwa hiyo, tunao uwezo na sisi wa kuweza kuamua kwa makusudi kabisa kwamba asilimia moja mpaka mbili ya *consumption tax* ambayo Watanzania wanaitoa iweze kwenda kusomesha kwenda kwenye bodi ya mikopo ili tuweze kutoa mikopo kwa wanafunzi wetu wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa napenda nipendekeze uwezekano wa kuangalia uwezekano wa kutoa *award* kwa wanafunzi wanaofanya vizuri kwa mfumo wa sasa wa elimu na jinsi ambavyo bodi inatoa mikopo yake, wanafunzi wanaoingia mwaka wa kwanza, mwanafunzi aliyepata *first class* katika mtihani wake wa mwisho na mwanafunzi aliyepata *pass* au aliyefanya *supplementary* mwisho wa mwaka yaani watakapoanza kulipa mikopo wanalipa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba nilipokuwa kiongozi wa Serikali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Wizara ya Elimu ya Juu, ilinipeleka *South Africa* kwenda kujifunza kuona ni jinsi ambavyo wao wana *Finance Higher Education*. Kule *South Africa* wanafunzi wanapoingia mwaka wa kwanza, wale ambao wamepata *first class,* asilimia 80 ya mikopo inageuzwa kuwa *grants* na wale ambao wamepata *lower second*, asilimia 25 ya mikopo yao inageuzwa kuwa *grants*, hii inasaidia kwa hiyo wanaolipa *100 percent* ni wale ambao wamefaulu kawaida na hii inasaidia sana kuwafanya wanafunzi wetu watumie muda wa kutosha kujisomea na hata matatizo ya migomo yanaweza yakaepukika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa kiongozi wa wanafunzi najua, ukiangalia *trained* ya migomo yote inakaribia tarehe za mitihani ndiyo *trend* ya migomo yote *especially* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho mimi nina uzoefu nacho. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia hili uwezekano wa kubadilisha mikopo kuwa *grants* kutokana na *performance* ya mwanafunzi darasani na hii itasaidia kuli-*award* wanafunzi ambao wana uwezo zaidi, wanasayansi wetu na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo Waziri aweze kuliangalia. Lakini suala lingine ambalo napenda tuliangalie katika suala zima la *higher education* sasa hivi kuna *trend* ya vijana wengi wanapomaliza Chuo Kikuu kukataa kwenda kufanya kazi mikoa ya mbali kama Lindi, Mtwara, Kigoma, Rukwa, Kigoma na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza kuweka mazingira ambayo ili iwe *incentive* kwa ajili ya vijana ambao wamemaliza chuo na kuajiriwa katika Serikali au Serikali za Mitaa au Idara mbalimbali za Kiserikali, *especially* wafanyakazi wa Serikali kwa sababu tunahitaji wataalamu zaidi katika watu wanaofanya kazi Serikali kuangalia uwezekano wale watu ambao watakubali kwenda kufanya kazi maeneo ambayo watu

wanakataa kwenda kwa kipindi fulani wawe wanapunguziwa kiasi cha mikopo ambayo inalipwa ili iwe *grants,* na hii itasaidia sana kuweka *incentive* kuhakikisha kwamba maeneo ambayo wataalamu wengi wanakataa kwenda yanaweza yakasaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni suala lazima la *means testing* watu wanahoji, bodi itatumia vigezo gani kuweza kusema kwamba huyu atapewa mkopo wa asilimia 10, huyu atapewa mkopo wa asilimia 80, huyu atapewa mkopo wa asilimia 10 au huyu hatapewa mkopo kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile njia pekee ya kuweza kujua ni jinsi gani mtu atapewa mikopo ni *means testing* na nilikuwa napenda Wizara ijaribu kuangalia kuweka mchakato maalumu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba *means testing* inakuwa na uwazi wa hali ya juu. Kwa vyovyote vile kuna wanafunzi ambao ni kweli kabisa kwamba hawahitaji mikopo, kuna watu ambao wamesoma shule za sekondari za *private* wamelipa mpaka milioni moja kwa mwaka wakati kitu ambacho kinatakiwa kulipwa chuoni ni takribani laki sita mpaka milioni moja hiyo hiyo. Kwa hiyo, kama mzazi ameweza kumlipia mtoto shilingi milioni moja anaposema sekondari, sioni sababu kwa nini asiweze kumlipia mtoto wake shilingi milioni moja anapoenda Chuo Kikuu.

Lakini tatizo litakalokuja hapo, ni jinsi gani ambavyo tutaweza kugundua kwamba mzazi huyu ana uwezo ama mzazi huyu hana uwezo. Kwa hiyo, ni vizuri sana kuweza kuangalia mchakato mzima wa *means testing,* wakati tuko chuo tulijaribu kufanya hivyo na akina Lubambula na kadhalika na Mkurugenzi Ndugu Mbeku lakini hakuweza kufikia popote na mikopo ikawa inatolewa kama jinsi ambavyo ilivyotolewa na matokeo yake unajikuta kuna watu ambao wamepewa mikopo mara mbili. Kwa hiyo, ni vizuri tuweze kuangalia jinsi gani ambavyo mchakato huu wa kuweza kufanya *determination* ya *means testing* uweze kuwa wa wazi ili kweli wale watu wanaohitaji mikopo waweze kupewa mikopo. Watoto wale wanaotoka Kalinzi, Mwandiga na kadhalika ambao wazazi wao ni maskini hawana uwezo kweli waweze kupata mikopo na wale watoto ambao wazazi wao wana uwezo watoto wengine wa Mawaziri, wa Wabunge, wa Wakurugenzi waweze tu kuepuka mikopo kutokana na uwezo wa wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba suala hili Serikali iweze kuliangalia kwa kina suala la *means testing* ili kuweza kuhakikisha kwamba wanaopata mikopo ni wale ambao kweli wanahitaji mikopo na suala la kugeuza mikopo kuwa *grants* kwa wanafunzi ambao wanafanya vizuri Waziri pia aweze kuliangalia na suala la kuangalia jinsi gani ambavyo tunaweza tuka *page certain percentage* ya *consumption tax* kwa ajili ya ku-*finance higher education*, ili kuhakikisha kwamba muda wote tuna uhakika wa kwamba mfuko una fedha na haitatokea sababu ya kusema kwamba hatuna fedha za kuwasomesha watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa muda ulionipa na naamini kabisa kwamba ushauri wetu kwa upande wa Kambi ya Upinzani utachukuliwa vizuri na Waziri na wataufanyia kazi kwa manufaa ya Taifa letu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabwe Zitto na kabla sijamuita msemaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, nitoe masahisho kidogo kwa watu wa *Hansard* ili waweze kuweka sawa wakati Mheshimiwa Charles Keenja anachangia alisema *Morogoro Islamic University*, inaitwa *Morogoro Muslim University*, baada ya hapo nimuite Mheshimiwa Mahenge. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mezani petu. Lakini kabla ya yote naomba nichukue nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kumpa pole Mheshimiwa Spika, kutokana na kifo ambacho kimetakikana na ambacho wote kwa kweli kimetugusa sana.

Lakini nitumie nafasi hii vile vile kuwapa pole wananchi wangu wa Makete, kwa kufiwa na ndugu yetu mpendwa ndugu Kisakiki Mahenge wa Kata ya Bulongwa aliyekuwa anasafirisha abiria wakati wote wa mwaka bila kuzingatia ubaya wa barabara kwa kutumia gari yake ya *Landcruser* kutoka Makete mpaka Njombe, kwa hakika Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu wetu, *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza sana Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kwa kuleta Muswada huu yeye pamoja na wafanyakazi wake wa Wizara, mimi nadhani hii inadhihirisha wazi jinsi Waziri huyu alivyoweza kuliona wazi kwamba hakuna kinachodumu isipokuwa mabadiliko kwamba kwa hakika tunatakiwa tufanye mabadiliko kuhusu matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza kwenye tatizo hili la *loan* za wanafunzi kwa hiyo, nampongeza sana kwa ku-*react* mapema na kuleta hapa mezani ili tuweze kuijadili na tupunguze kero ambazo zilikuwa kwa wanafunzi, lakini la msingi kwamba tunataka tupate wasomi walio wengi katika nyanja nyingi mbalimbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu nataka niipongeze Serikali ya awamu ya nne kwa ari, nguvu na kasi mpya kwa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma, unafahamu sasa hivi ukitaka habari za *Leeds Metro Politan University* mtu anakuambia nipe taarifa utakimbilia kwenda kwenye *internet,* lakini ukitaka habari za *Dodoma University* unakwenda pale Mlimani, mimi nimefika nimejionea maajabu ambayo yamefanywa na awamu hii ya nne na nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini la msingi nataka niwapongeze maprofesa waliokubali kuondoka Dar es Salaam kuja kuleta haya mabadiliko pale Dodoma. Nawapongeza sana Profesa Kikula, Profesa Mlacha na wengine wote kwamba hii ni chachu na ni changamoto kwa Maprofesa wote kukubali kwenda mikoani kuleta mabadiliko katika nchi yetu hii, nawapongezeni sana na kwa moyo huo nawaomba sana wafike mpaka kule Mbeya, Chuo cha Sayansi na Teknolojia nacho kiko karibuni kutoa *degree* za elimu juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kuhusu hii sehemu ya sita kwenye *section* ya tatu, ambayo inasema kwamba bodi ita-*determine percentage* ya kiwango cha mwanafunzi kuweza kuchangia kwamba atalipa kiasi gani? Mimi nilikuwa nadhani tungetumia *approach* tofauti kwa mfano ukiangalia sasa hivi tunayo matatizo kwamba

kwanza madaktari hawawezi kwenda vijijini, Wilayani huko, tatizo la pili tumekuwa na mkakati mzuri ambao ni wa MMES wa kuhakikisha kwamba tunapata sekondari kila kata, lakini tumekuwa na tatizo la walimu hawafiki huko, kwa sababu mazingira magumu kwenye hizo sehemu la vijijini.

Lakini tatizo la tatu ni sehemu nyingi za sekta za sayansi ambazo wataalamu hawako tayari kwenda huko kwenye vijijini. Kwa hiyo, pendekezo langu nilikuwa nadhani pamoja na kukizingatia kipengele hiki kiwepo, lakini nilikuwa nadhani kuna haja ya kuwa na kipengele ambacho kinatoa *guarantee* ya *loan* kwa vijana walioomba masomo ya sayansi na hasa kwenye taaluma hizi ambazo sisi tunashida nazo kama za udaktari, uhandisi, ualimu na kadhalika kwa masharti kwamba huyu anapewa *loan* bila masharti kwamba yeye ana uwezo kulipa au hana uwezo wa kulipa na ukizingatia ukiangalia katika takwimu mbalimbali mara nyingi watoto hawa wa wakulima ndiyo wanaopasi sana masomo ya sayansi kimsingi ndiyo wanakuwa na uwezo sana wa kwenda hizi *degree* za sayansi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukifanya vile ukatoa *loan* kwa watoto hawa ambao wameomba kwenda kusoma *engineering,* wameomba kwenda kusoma *medicine* sasa uwape mkataba kwamba utakapomaliza utakwenda kufanya kazi Mtwara kwa muda wa miaka mitano kwa hiyo, kwanza utakuwa umevutia apate fani yake ile, lakini vile vile utakuwa unatatua tatizo ambalo linaisibu Serikali yetu ya kupata wataalamu katika sehemu za vijijini. Lakini nikadhani kwamba baada ya huyu kijana kukubali huo wito sasa namna gani kama yeye atakuwa pengine hapendi kwenda hiyo sehemu ndipo hapo sasa unam-*subject* kwamba *loan* yako airudishe mapema iwezekanavyo. Hilo lilikuwa ni pendekezo langu naomba tuangalie matatizo ya nchi yetu, vipaumbele vyetu kama tulivyo na kipaumbele sasa hivi cha kuwa na sekondari kila kata na tunajenga Vyuo Vikuu ambavyo vitahitaji walimu wa kufundisha wale wanafunzi. Sasa kama tutakuwa tunasema bodi ndiyo i-*determine* nani aweze kwenda tunaweza tukakuta kwamba tunakosa wale vijana ambao wamefaulu wenye *willing* ya kwenda sayansi lakini wakawa wamekosa hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili nilikuwa napendekeza namna ya kukusanya hizi hela, kwa sababu utaratibu ulioanzishwa ni mzuri, mtu unaweza ukajitolea na ukaamua mshahara wako ukatwe. Lakini nilikuwa nadhani kama kweli tunataka kuijenga mifuko yetu hii ya *NSSF* na *PPF* kwamba ifike kila sehemu kwenye sekta binafsi, sekta za Serikali kwamba wafanyakazi wao waweze kujiandikisha iwe mfuko na wachangie mafao yao kwenye ile mifuko basi hii ilikuwa nidyo sehemu pekee ambayo tungeweza ku-*subject* kwamba wanafunzi baada ya kumaliza hela zile zinapatikana kwenye mifuko ya *NSSF* au *PPF* na mifuko mingine, kwa hiyo, kunakuwa hamna tatizo kwa bodi hii kupata hela zake kwa hiyo, inakuwa inajua kwamba mwaka huu wameajiriwa wangapi kwenye sekta binafsi, sekta ya Serikali wangapi, *then* inatengeneza *formula* hela zake zinaweza zikapatikana zote. Kwa hiyo, hii inaweza ikatusaidia sana katika zile sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zingine ambazo zinaweza kuwa za sayansi zingeweze kutumia utaratibu huu wa hiyo bodi ku-*determine* nani aweze kutoa kiwango

fulani na nani aweze kuongeza kiwango fulani. Kwa hiyo, nadhani tutakuwa tumekata *cross* kwa vijana wetu wote waweze kupata elimu hiyo ya juu. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia machache naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kunipa nafasi hii, lakini nitamuomba sana mtoa hoja akubaliane nami kwamba ipo haja ya kuweka kutoa *loan* kwa wanafunzi katika sekta muhimu za Serikali ambazo zitauletea mafanikio katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia napenda kuungana na Wabunge wenzangu kutoa pole sana kwa Spika, kwa msiba mkubwa uliompata kwa kufiwa na mjomba wake na pia nimpe pole Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati za Huduma za Jamii kwa msiba uliotokea huko Mpwapwa. *(Makofi?Kicheko)*

Pili niwashukuru sana wote waliopata nafasi kuchangia kwa kusema hapa Bungeni lakini vile vile kwa maandishi. Michango yao imekuwa ni ya kina na ni mizuri sana napenda kuwahakikishieni kwamba yote mliyosema tutayazingatia. Lakini michango hii mingi kwenye upande wa elimu ya juu inaonyesha kiu kubwa tuliyonayo ya kupanua elimu ya juu na kwamba kwa sasa hivi kuna mwamko mkubwa sana kwa watu kutaka kupata elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwatambua wale waliochangia kwanza kwa kuongea hapa Bungeni kama ifuatavyo, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliochangia kwa maandishi ni kama wafuatavyo, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. *(Makofi)*

Napenda sasa nitoe ufafanuzi katika hoja zilizotolewa toka asubuhi hii. Nianze na hoja zilizotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala zilizowasilishwa na Mheshimiwa Athumani Janguo, kwanza amezungumzia juu ya muundo wa bodi kwamba muundo wa bodi uliopo haushirikishi wadau wa kutosha, akasema kwamba Wakurugenzi wa Elimu ya Juu na Ufundi ni muhimu kuwepo katika bodi, si muhimu kuwepo katika bodi lakini wanaweza kukaribisha.

Napenda kutoa maelezo kwamba Wakurugenzi wa Elimu ya Juu na Ufundi ni muhimu kuwepo katika bodi kwa vile wao ndio wasimamizi wa elimu juu na ufundi kwa maana ya kuainisha vipaumbele vya Serikali na matatizo ya sekta husika. Hata hivyo Serikali imetenga nafasi mbili ambazo Waziri anaweza kuteua watu mahiri na ningependa kuisoma katika jarida mlilopewa ukurasa wa pili (m); *"Two eminent persons having knowledge and experience in management of higher learning institutions."*

Tunafikiri kwamba nafasi hiyo itakuwa ni muhimu sana. Lakini vile vile kuna mjumbe kutoka Hazina, huyu mjumbe ni muhimu kwa sababu fedha hizi zinatoka Serikalini ambazo wanafunzi wanapewa kama mikopo. Halafu kuna mjumbe mmoja kutoka kwenye *financial institutions* naye huyu ni muhimu kwa sababu kama mnavyofahamu tumekuwa tukikopa fedha hizi kutoka kwenye mifuko ya jamii. Halafu vile vile tunawakilishwa na Vyuo Vikuu vya Umma na Vyuo Binafsi tunafikiri kwamba muundo huo utasaidia sana katika kuboresha muundo wa bodi.

La pili, Mheshimiwa Athumani Janguo alizungumza kwamba Serikali itenge fedha za kutosha kwa vile asilimia 0.5 ya *skills development level* ni kidogo sana, hili limezungumzwa na watu wengine, limezungumzwa na Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba wote wakijenga hoja kwa upande huu kwamba mfuko huu lazima ujitosheleze. Tunakubaliana na maoni ya Wabunge na kwamba Serikali itakuwa ikiongeza fedha za elimu ya juu kwenye mfuko huu kadri uwezo wa kiuchumi unavyoongezeka. Hata hivyo Serikali imekuwa ikiongeza fedha kutoka shilingi bilioni 43.5 mwaka 2005/2006 hadi kufikia sasa shilingi bilioni 117 kwa mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara iandae utaratibu wa kuelimisha umma. Serikali imepokea ushauri huo na itaendelea kuelimisha umma kupitia njia mbalimbali ikiwemo redio na *TV* kwa sasa hivi tuna kipindi kimoja kila siku ya Alhamisi jioni nafikiri ni saa 12.30 jioni ambacho kinatangazwa. Lakini baada ya sheria hii kupita tutakuwa na vipindi maalumu kama vile Tuambie, Sema Usikike, ili kusudi watu wengi waweze kushiriki zaidi kutoa michango yao katika hili. Serikali iweke utaratibu wa kuhakikisha kuwa waajiri hawakiuki taratibu limetolewa na Mheshimiwa Athumani Janguo. Utaratibu huo unaopendekezwa umezingatiwa katika Muswada huu ambao tumewasilisha leo asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Serikali izingatie mahitaji maalumu ya wanafunzi wenye ulemavu. Hili limezungumzwa na watu wengi, Mheshimiwa Athumani Janguo pamoja na Mheshimiwa Susan Lyimo, limezungumzwa na Mheshimiwa Margaret Mkanga, kwa undani kabisa na tunasema kwamba suala hili limezingatiwa katika Muswada na jedwali la marekebisho. Pengine nitoe ufafanuzi zaidi kwa lile alilolizungumza Mheshimiwa Margaret Mkanga kwa ajili ya mahitaji maalumu akauliza ni vifaa vipi ambavyo vinazungumziwa katika hili. *(Makofi)*

Kwanza nafikiri ni lazima tutambue aina ya ulemavu. Kuna walemavu ambao ni viziwi, kuna walemavu wasioona, kuna wenye ulemavu wa viuongo na kadhalika. Kwa hiyo, vifaa ambavyo vinazungumzwa ni kusaidia hao wenye ulemavu wa aina hiyo na kwamba tunazungumzia vitu kama Bajaji, *hearing aids, blear machines*, *walking sticks* sijui kwa utalaamu zinaitwa nini na kwamba hivi vitu kwa kuwa ni mkopo unaondoka navyo havibakii pale chuoni kwa sababu umekopeshwa huendi ukatumie huko unakofanya vile vile. Amezungumza vile vile kwamba walemavu wasomeshwe bure. Lengo la Bodi ya Mikopo kuanzishwa ilikuwa ni kuwasaidia wanaofanya vizuri katika taaluma lakini hawana uwezo wa kulipia masomo hayo. Sasa kuwa mlemavu haina maana kwamba huna uwezo kuna walemavu ambao wana uwezo mkubwa, kuna walemavu wanaofanyakazi, kuna walemavu ambao wana mali za kwao. Kwa hiyo, huu

ulemavu kweli pamoja na kwamba ataangaliwa lakini wataangaliwa pamoja na mambo mengine. Kama una uwezo wa kiuchumi basi utapewa mkopo kutokana na uwezo wako wa kiuchumi. Lakini isije ikawa kama ni *blanket* tu ili mradi wewe mlemavu basi upewe mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo katika vigezo vya mkopo yanasomeka *as may be stipulated by the board*. Nashukuru kwamba Mheshimiwa Kabwe Zitto ameliona hili kwamba hili limeshatolewa toka tukiwa kwenye Kamati kwa hiyo, hilo halipo tena. *(Makofi)*

Halafu sharti la kuwa na mdhamini *(guarantee)* katika utoaji wa mikopo hili limeulizwa na Mheshimiwa Susan Lyimo. Suala la mdhamini katika utoaji wa mikopo ni la msingi ili kuwezesha mikopo inayotolewa kurejeshwa. Utaratibu huu ni wa kawaida katika mikopo ya aina yoyote. Kwa hiyo, huu hauwezi kuwa ni tofauti. Hapa tunazungumzia juu ya uchache wa fedha ambazo zinapatikana kwenye mkopo. Sasa huku usipoweka taratibu ambazo kwa kweli zinambana mtu ili arudishe mkopo basi huu mkopo itakuwa ni kutoa tu lakini ku-*guarantee* hata ungekwenda hata benki wanataka *guarantee* hata ukitaka kutolewa mahakamani una kesi wanahitaji mdhamini, kwa hiyo, hili siyo jambo ambalo likifanyika katika jamii yetu.

Lingine vigezo vitakavyotumika kuwatambua wanafunzi wahitaji tunasema msingi wa kuwatambua wanafunzi wasio na uwezo utakuwa ni hali ya kiuchumi ya mwombaji na wazazi ama walezi wake. Hili ndiyo litakalofanyika ili mradi zile fomu za maombi zinajazwa kikamilifu na vizuri na kwa usahihi na zinakwenda kuanzia kule kijijini unakotoka zinakwenda kwenye kata na hatimaye kufika kwenye bodi. Nina hakika katika kupita kwenye bodi tuna hakika katika kupita njia hizo watu wengi wanakufahamu zaidi na kwamba watasema lile ambalo lina ukweli. Baada ya kupitishwa sheria zitaandaliwa kanuni *(regulations)* ambazo zitabainisha mambo ya msingi ya kuzingatiwa wakati wa kutambua waombaji wahitaji.

Halafu kuhusu mikopo kwa wanafunzi wanaorudia mwaka wa masomo, Mheshimiwa Susan Lyimo, sheria hii haikatazi wanafunzi wanaorudia mwaka wa masomo kupewa mikopo hata wale wanaopewa *supplementary* Serikali tayari inatoa *(grants)* inatoa mikopo hiyo kwa wale wanaorudia mwaka wa masomo na vile vile kwa wale wanaorudia mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanafunzi wasianze kulipiwa na Serikali kwa asilimia 70 na kupewa mikopo kwa asilimia 30, nasema Serikali tayari inatoa *grants* na baadhi ya fani muhimu zenye upungufu wa wataalamu hili linatokea kwa sasa. Aidha, Serikali imekuwa ikitoa tuzo na zawadi mbalimbali kwa shule na wanafunzi wanafanya vizuri katika masomo ya sayansi, haya yanafanywa hata na vyuo vyenyewe na kila mwaka *a day before graduation* kunakuwa na sherehe za kuwatambua wale wanafunzi waliofanya vizuri na wanapewa zawadi, hizi zawadi zinatolewa na chuo chenyewe, Wizara zenyewe na hapa kuna Wizara nyingi sana zinatoa hizo zawadi ikiwa ni pamoja na watu binafsi ambao wametaka majina yao yatambuliwe katika taaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bodi kukopa fedha kutoka mifuko ya jamii wakati bodi haina uwezo wa kurudisha ni Mheshimiwa Susan Lyimo amelizungumza, bodi inakopa fedha kwa udhamini wa Serikali. Aidha, marekebisho haya yanaainisha njia za kuimarisha urejeshwaji wa mikopo, laana ya uchangiaji ni onevu kwa Watanzania walio wengi maskini. Uchangiaji wa gharama za elimu ya juu ni utekelelezaji wa sera ya elimu ya juu ya mwaka 1999 kama ambavyo nimeeleza wakati wa kuwasilisha hoja hii ili wanafunzi walio wengi zaidi waweze kunufaika. Mkopaji ashirikishwe kikamilifu katika kupanga kiwango cha makato na muda wa kurejesha, sheria inaruhusu ushirikishwaji wa wakopaji na utaratibu huo ndio unaotumika kwa sasa. Lingine lilikuwa mwajiri asihusishwe na mambo ya mikopo limetolewa na Mheshimiwa Susan Lyimo, mwajiri kuhusishwa na mikopo ni wajibu wa Kitaifa na huu ni utaratibu wa kawaida na si kwa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu peke yake bali hata katika makato mengine kama kodi za Serikali, *PPF* na mambo mengine waajiri hukata na kupeleke fedha hizo zinapotakiwa, kuahirishwa jambo jipya ni jambo ambalo limekuwa likitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ukubwa wa adhabu, Mheshimiwa Susan Lyimo, falsafa ya adhabu ni kuzuia kufanya kosa na kutoa onyo kwa atakayetaka kutenda kosa kama hilo hilo. Wanafunzi wanajigharamia kwa asilimia mia moja hili nafikiri lilielezwa wakati wa kuwasilisha Bajeti tarehe 20 Julai, 2007 kwamba sehemu ambayo mwanafunzi kwa kweli anachangia ni sehemu kidogo sana, nilitoa mfano wa mwanafunzi anayesomea udaktari wa mwanadamu kwamba gharama halisi ya mwanafunzi anayesomea shahada ya wanadamu kwa maana ya malipo *Tanzania shillings* ni karibu milioni sita kila mwaka, lakini kwa pale Muhimbili malipo wanayatarajiwa kulipwa ni milioni moja, milioni moja katika milioni sita ni asilimia 16.7. *(Makofi)*

Hata hivyo katika mpango uliokuwepo mwaka jana anachotakiwa kulipa katika hizo ni asilimia 40 yaani shilingi 400,000/= ambayo ni sawa na asilimia 6.7, mkopo huu hauna riba, mkopo huu unatakiwa kurudishwa kwa kipindi cha miaka 10 katika miaka 10 fedha hii inakuwa haina hata thamani. Kusema kweli Serikali ndiyo inayobeba mzigo mkubwa wa kumsomesha mwanafunzi Chuo Kikuu katika utaratibu tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wadau kutoshirikishwa kikamilifu wakati wa kuandaa Muswada, kama nilivyosema asubuhi nilizungumza juu ya kanda saba, wananchi walishirikishwa kikamilifu kama nilivyoeleza mara ya kwanza. Taasisi za elimu ya juu karibu zote nimetembelea kwenye Wilaya, nimetembelea kwenye Mikoa mpaka Zanzibar na watu wametoa maoni yao na kabrasha namna hii lipo ushahidi. Licha ya wanafunzi kushirikishwa kwa ujumla lakini hata vyama vya wanafunzi nao walishiriki kutoa maoni yao ikiwa ni pamoja na TAHIRISHO yenyewe ambayo nayo ilileta maoni yake kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16(c) na (d) mikopo kwa wanafunzi ambacho kinazungumza juu ya masharti ya 16 (2) (c) na (d0 hii pengine niisome kusudi iweze kueleweka, hii ya 16(c) na (d) ambayo vile vile mjumbe mwingine amelizungumzia (c) inasema kwamba *provided that the board shall offer to eligible seize loans in respect of items specified under subsection two, to the extend either it may determine*, hili neno naona kama linatisha watu lakini utaratibu wa kawaida na

tunazungumzia juu ya hiyo *means testing* hiyo ndio *determination* yake siyo kwamba mtu anakaa kama alivyozungumza Mheshimiwa Susan Lyimo, kama unatizama mtu usoni, kwanza utaonana na watu wangapi, wanafunzi waliopo sasa wanaoingia Vyuo Vikuu wanafikia karibu 75,000 wewe utaangalia nyuso ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ipo hiyo *means testing* ambayo ina vigezo vyake ndio kitakachokuwa kinalenga. Lingine masharti mapya ya mikopo yatatumika kwa wanafunzi wa makundi yapi? Masharti haya mapya ya mikopo yataanza kutumika mwaka huu wa masomo kwa maana ya mwaka 2007/2008. Kanuni za kusimamia mikopo zitungwe mapema hili limezungumzwa na Mheshimiwa Charles Keenja, Serikali inaahidi kuwa mara baada ya Muswada kupitishwa na kuwa sheria, kanuni zitaandaliwa na kutangazwa mapema iwezekanavyo, pengine niunganishe na swali lake lingine ambalo alilizungumzia Mheshimiwa Charles Keenja, amezungumzia juu ya lengo la kufika asilimia 12.5 ya washiriki katika Vyuo Vikuu ifikapo mwaka 2010 na ninakushukuru sana pale ulipotamka kwamba wale walio na uwezo kwa kweli wasihangaike kwenye mikopo ila walipie vijana wao na hili ndio lengo la huu Muswada kwamba wale walio na uwezo walipie vijana wao na wale ambao kweli ni wahitaji ndio waende kwenye bodi ya mikopo na lile ambalo alizungumzia hilo hilo la 16(c) nafikiri nimeshalieleza lakini akasema, je, kwa wale ambao hawataridhika na kiwango wanachokopeshwa waenda wapi? Jambo kama hili ni jambo la kawaida lakini kama litakuwa limefanywa kikamilifu na wamejaza taarifa zote ambazo ni muhimu sitarajii kwamba kutakuwa na matatizo kama hayo na kama kutakuwa na matatizo wataweza kuomba rufaa bodi ili kusudi wakaangalie haya mazingira vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile umezungumzia juu ya s*tress, a skills development level* kwamba ni kidogo asilimia 0.5 iende mpaka asilimia 2.5, wazo ni zuri nimeshajibu hapo mapema kwamba kadri ya uwezo unavyoongezeka kiwango hicho kitaongezeka, lakini vile vile kuna mengine ambayo yametolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto ambayo yanatakiwa nayo vile vile yafikirie kuangalia vyanzo vingine vya fedha.

Pia Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe alizungumzia mambo mengi na akazungumzia juu ya urejeshwaji wa mikopo, taratibu ziongezewe nguvu na akazungumza vile vile kwamba kuwepo utaratibu kwa wale ambao hawarudishi mikopo wasiruhusiwe kugombea hata Ubunge wasiandikishwe hata kwenye *professional associations,* mambo mengi ameyazungumza, tunasema kwamba ametoa ushauri mzuri wa kuboresha katika maeneo mengi kama nilivyosema wanaodaiwa mikopo wasipewe nafasi ya uongozi wala kuingia kwenye *professional bodies,* muda wa hatua za kimahakama kurejesha mikopo upunguzwe kutoka miaka 10 mpaka miaka mitano, nasema ushauri wa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, ni mzuri ambao unagusa mambo mengi ya kisera. Serikali inaahidi kufanyia kazi ili hatimaye yaweze kuboresha urejeshwaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Lazaro Nyalandu amesema kwamba Bodi ya Mikopo iwe na mamlaka kamili ya kukusanya, kufanya shughuli zake, napenda kumfahamisha kwamba taasisi hii ina mamlaka kamili kisheria ya kufanya shughuli zake, ina-*operate* kama *agents*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa Mheshimiwa Kabwe Zitto, amejenga misingi hata ile ya asilimia 12.5 kufikia mwaka 2010 kwamba wahitimu za kidato cha sita waweze kujiunga na Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi, lakini vile vile kwamba bodi iimarishwe ili itoe mikopo kwa walio wengi zaidi na kwamba amezungumzia madaraja na ile asilimia 40 tunasema hayo ndiyo yaliyotufikisha hapa kuleta huu Muswada Bungeni. Lakini katika *financing of high education* aliyoizungumzia kwamba tubuni sehemu nyingi zaidi za kuangalia ni namna gani tuna-*finance high education*, napenda kumuarifu Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba Serikali imeliona hilo mapema sana, iliunda Kamati ya watu ambayo iliandika *financial sustainability of higher learning institutions in Tanzania* na kuna ripoti yake. Katika ripoti nyingi zilizotolewa na baada ya hao wataalamu kutembelea nchi mbalimbali na mimi nilikuwa mjumbe mmojawapo, mimi nilitembelea Marekani na Canada njia ambayo ilionekana iko wazi zaidi ni mambo *cost sharing* tuanzie hapo ndio tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ilishafanywa na kuna mifano mingi hata haya mambo tunayozungumza leo ya *skills development level* yalikuwepo kwenye ripoti toka mara ya kwanza na mambo mengine mengi, lakini nashukuru kwamba umelikumbushia hilo. Neno ambalo umesikia kwamba wanafunzi wa kiume wenye *division two* watanyimwa mikopo hilo siyo kweli na ninapenda kuwaambia wanafunzi kama tulivyotangaza kwenye hotuba yangu ya Bajeti, wanafunzi wa daraja la pili wanaume ambao walikuwa wameachwa kwa mwaka jana wanaruhusiwa sasa kuchukua mikopo, huu wigo umepanuka zaidi vile vile wote wanaochukua sayansi kwa wale waliozungumzia mambo ya sayansi, Mheshimiwa Susan Lyimo na wengine, wote wanaochukua sayansi wanaruhusiwa kuchukua mikopo sasa. Umependekeza mapato mengine juu ya *consumption taxes* kwa mfano *VAT,* nasema hili ni jambo la kisera tunachukua hayo maoni yako na kwamba *rewards* kwa wanaofanya vizuri vyuoni nimeshaeleza kwamba vyuo vyenyewe hutoa zawadi na kuna mashirika mbalimbali kama vile *TANAPA* na watu binafsi ambao kwa kweli wamekuwa wakivutiwa sana kwa kutoa zawadi kwa vijana waofanya vizuri, unaweza tu wewe ukatoa fedha zako pale ukasema natoa hizi milioni pengine tano zinakuwa kwenye *fixed deposit* ikaitwa *Zitto Kabwe's price.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vijana unamsomesha yule ambaye anakuwa amefaya vizuri katika eneo ambalo wewe unalilenga, haya mambo yamekuwa yakifanyika na tunazo zawadi nyingi zinazotolewa na Serikali hapo nyuma ilikuwa inatoa *scholarships* kwa ajili ya wanafunzi ambao walikuwa na *outstanding performance*. Kuhusu wale wanaofanya kazi pembezoni, wanaofanya kazi pembezoni siyo wahitimu wa Vyuo Vikuu tu wako watu wengi sana kwa hiyo, kwa ujumla wake kama tunataka kuwamotisha hawa ni lazima pengine jambo hili liangaliwe kwa upana wake, najua limezungumzwa mahali pengine lakini haiwezi kuwa ni vijana wanaotoka Vyuo Vikuu peke yake. Umezungumzia juu ya *means testing* kuwa wazi zaidi ni kwamba hii *means testing* ni chombo ambacho kitasaidia kuwatambua wale ambao ni wahitaji zaidi na kwamba kuwatambua huko kutatokana na namna fomu ile ilivyojazwa, umezungumzia juu ya wanafunzi waliosoma katika shule za *private* kwamba tutawatambuaje hao, *it is very easy to go back on records* kwenye shule walizosoma, unaweza kujua maana yake

watu wakishasikia hivi mwingine anaweza kusema kwamba sasa mimi nibadilishe niseme nilisoma shule hii, lakini kuna namna ya kupata *information* yote na kujua huyu kutoka *nursery, primary, secondary* amepitia katika mikondo hii na anataka kuja kubadilika tu katika hizi dakika za mwisho, nafikiri kwamba hili si tatizo *records* zikifuatwa zinakuwa hazina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, anasema bodi itaamua kiasi gani **cha** mkopo nishalieleza hilo, linazingatia hiyo ya miezi sita sita lakini akashauri kwamba *guarantee* ya *loan* kwa wale wanaochukua sayansi ni vema wakainga mkataba wa kufanya kazi nchini baada ya kuhitimu masomo, utaratibu huu ulikuwepo kwa watu wengi tu ni hapa miaka ya katikati ndio kidogo imekuwa kama imelegea kwamba ukipewa kwa mfano *scholarship* au *bursary* ilikuwa lazima usaini mkataba na Serikali kwamba wewe utarudi na kufanya kazi angalau kwa miaka mitano hapa nchini, ushauri huo nafikiri ni mzuri kuweza kuurejea ili kusudi tusipoteze watu wengi. Kuhusu ukusanyaji wa fedha kupitia mifuko ya jamii kama nilivyosema hapo nyuma kidogo, hili ni swali ambalo ni kisera na tungependa kulipokea tu tulifanyie kazi tunacho-*suggest* ni kwamba tuwe na njia mbayo ni rahisi kuweza kukusanya fedha kutoka kwa wale waliokopeshwa na ninasema kwamba hili tutalizingatia wakati tunafanya marejeo katika haya yote ambayo tumeyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii tena niwashukuru sana tena sana wote walipata nafasi ya kuchangia katika Muswada huu na kwamba tunathamini sana mawazo yaliyotolewa na kwamba tutayafanyia kazi ili kusudi tuweze kuboresha hii sheria ya bodi ya mikopo. Ni njia pekee ambayo inasaidia vijana wengi sana kuweza kupata nafasi ya kujiunga na elimu ya vyuo vya juu kinyume na taratibu zilizokuwepo huko nyuma na nafikiri kwamba wote kwa pamoja tushirikiane katika hili ili kusudi mfuko huu uzidi kuwa na nguvu na vijana wetu wengi zaidi waweze kupata nafasi ya elimu ya juu.Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono lakini kwa ajili ya watu wa hansard nirekebishe sahisho dogo wakati Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia akitoa pole kwa Mheshimiwa George Lubeleje alimtaja kuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii sahihi ni kwamba ni Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ilisomwa Bungeni Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*
Ibara ya 3

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya mimi kuweza kuzungumza kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3 kuna hiyo *composition* ya wajumbe wa bodi ni kwamba idadi wasizidi 14 lakini ni 13, hoja yangu ni kwamba wengi wa wanafunzi ambao wameajiriwa watakuwa ni wafanyakazi kwa hiyo nilikuwa napendekeza kwamba katika *composition* hiyo basi kuwe na *at least one member* katika kuweka hizi *association* ili waweze kutetea maslahi ya wanafunzi wakati wameajiri.

Lakini la pili kwenye Ibara hiyo hiyo kipengele cha tatu inasema, provided *in appointing members of the board the minister shall insure that at least one third of the members of the board consist of woman.* Mimi ninaamini Wizara hii ina wasomi wengi lakini zaidi ya hayo wanawake wengi ni wasomi kwa hiyo nilikuwa nafikiri ifike wakati sasa walau ingesema *at least half* na siyo *one third* kwa sababu ninaamini wanawake wengi wapo na wanaweza kuwa katika hiyo bodi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo una-*move amendment* au unaomba maelezo?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hawa *worker association* kwa kweli wale ambao ni *relevant* hiki chombo ni chombo kinachoangalia taaluma siyo kwamba kiangalia watu baada ya kuhitimu wanakoenda kufanya kazi, tunaangalia namna bora ya kuweza kuwafikishia mikopo kwa hiyo *workers association* hapa kulinda maslahi ya wafanyakazi haiendani sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya *one third* ya wajumbe wa bodi wawe wakina mama hili tayari lipo katika sheria mbalimbali *it's a formative action*, hata hapa Bunge hatujafika 50 *percent* kwa hiyo hatuwezi kuruka tu huko tukaenda kwenye 50 *percent* na hii amendment hatu-*amend* hapa hii sheria kwa namna hii.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika. Mimi nadhani suala la wanawake kwamba Bungeni hatujafika 50, 50 kwenye *decision marking* hii siyo *decision* kwa hiyo nilikuwa nafikiri kwamba ifike mahali sasa kwa sababu *one third* imeanza toka zamani sasa hivi ninachozungumzia ni kwamba wanawake wasomi wengi kwa hiyo hakuna haja ya kuwa na *one third* kwa nini tusiseme *at least a half* au kwa nini tusiseme *at least one third* ya wanaume basi ndio wawepo kwa nini wanasema *at least one third* kwa wanawake.

**MWENYEKITI:** Ndio maana mara ya kwanza nilikuuliza unafanya *amendment* au unataka maelezo? Na kama ni maelezo yameshatolewa, kama ulitaka ku-*move amendment* ungeileta mapema. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7 (3) nilipochangia nilishauri kwamba Waziri angeangalia uwezekano wa kuweka utaratibu wa *appeal* kama bodi imeamua kwamba mwanafunzi huyo atalipa *percentage* fulani na mwanafunzi huyo na wazazi wake hawawezi kulipa lazima kuwa na mahali ambapo wanaweza kwenda wakajieleza na nilipendekeza kwamba hiyo *appeal* inaweza ikaenda hata kwa Waziri mwenyewe, Waziri ni mwanasiasa mwenzetu kwa hiyo anaweza akaangalia mazingira ya mtu yule halafu akafanya marekebisha, sasa naomba maelezo kwa nini Waziri ananikatalia hilo.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najibu hoja yake nimeeleza hilo. Lakini nafikiri tusiwe na shaka sana kabla sheria hii haijaanza kutumika kwa sababu tunafikiria mapema mno kusema kwamba lazima kutakuwa na matatizo kama haya, lakini nilitoa maelezo hapa kwamba tuiruhusu hii sheria itumike tuone kama kuna matatizo tutakuja kuingia. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17 inaongeza kipengele cha 28 a ambacho kinasema *the ball shall be exempted from payment of all taxes rates, duties and charges* sasa nilipoangalia upande wa *definition* sijakuta wakisema *board* wana maana gani kwa sababu kuna *definition* ambayo naweza *board including members to the board* sasa ukishaweka *a blankets statement like that* unaweza kujikuta kwamba wajumbe wa *board* wana-*apply for tax exemption* wakati ni *institution* inayotakiwa iwe na *exemption* kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri a-*clarify* anaposema *the board shall be exempted from payment of all taxes* ana-*include* wajumbe wa bodi?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa inalenga wajumbe wa bodi tungesema *members of the board*. Lakini hii inasema the *board*, *board* inaeleweka ni kitu gani. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki inapendekezwa kwamba asiliami 0.5 ya mapato ya *skills develoment level* itengwe kwa ajili ya mfuko huu, kwanza ningependa kujua msingi wa hii asilimia ilifikiwaje maana sisi hapa ndani tunaamini kwamba kiwango hiki ni kidogo sana na kamati imependekeza asilimia 2.5 ambayo na mimi nafikiri bado ndogo ingeenda labda asilimia tano, naomba maelezo tafadhali.

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa maelezo yangu nilikiri kwamba ni kweli kiasi hicho, inasema kwamba *the Ministers of finance shall in every financial year remit to the account of the board the sum of not less than 0.5 percent not less*, sasa tusiichukulie 0.5 na nilipokuwa natoa maelezo nilisema kwamba kadri ya uwezo unavyoongezeka basi kiwango hiki kitazidi kuongezeka kwa sababu ni *not less than* siyo kwamba hicho ndio kikomo chake cha mwisho. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Bunge lilirudia*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, taarifa ya kazi ya Kamati.

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha *Loan* ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu wa Mwaka ya 2007**
***(The Higher Education Student's Loans Board Amendment Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *the Higher Education Student's Loans Board Amendment Act* 2007, Ibara kwa Ibara na kuridhia pamoja na marekebisho yaliyomo katika jedwali na marekebisho bila mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa kabla sijawahoji nasimamisha shughuli zinazoendelea kwa dakika tatu na ninamwagiza Katibu apige kengele kwa vituo yaani siyo mfululizo, kwa nia ya kuwataka Wabunge wote walio ukumbi huu warudi humu ndani na mliomo ndani mbakie humu ili tuweze kufanya maamuzi yanayofuata.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge walio nje waingie ndani ya Ukumbi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaamini muda wa kuwaita Waheshimiwa Wabunge walioko nje sasa umetosha na kilichofanyika ni *standard practice* ya Mabunge ya *Commonwealth* Duniani inapofika wakati wa maamuzi muhimu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa wakati huo Muswada wetu umeshapitia hatua zote, kwa hiyo nalipa taarifa Bunge kwamba Muswada wa sheria ya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu wa Mwaka 2007 sasa umeshakubaliwa na Bunge. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mkiangalia *order paper* yetu ya leo shughuli zote zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika kwa hiyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.32 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*

*Tarehe 14 Agosti, 2007 saa tatu asubuhi)*